# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 11 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Nane, Kikao cha Kumi na Moja.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. JAFARI W. CHEGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo aulize swali lake.

Na. 178

**Ujenzi wa Chumba cha Upasuaji Hospitali ya Wilaya – Nsimbo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Chumba cha Upasuaji katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ilipokea jumla shilingi bilioni 2.94 na kujenga majengo 12 ya hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali itatenga shilingi milioni 265 kwa ajili ya ujenzi wa

jengo la upasuaji katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Natoa shukrani zangu kwa majibu mazuri ya Serikali. Pia, naomba niipongeze Serikali kwa kazi kubwa, kwa majengo yote hayo 12 yaliyojengwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Nsimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa wananchi wanapata shida sana hususani akinamama wajawazito, hawana mahali pa upasuaji wakati wa kujifungua. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kujenga jengo dogo la dharura kuhakikisha akinamama wale waweze kupona maisha yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa Serikali imefanya kazi kubwa katika Hospitali ya Wilaya ya Nsimbo na hatuna kabisa *theatre* ya magonjwa mbalimbali, wananchi wanatumia gharama kubwa kwenda katika maeneo mbalimbali hususani mikoa mbalimbali. Je, Serikali haioni kufanya dharura ya kujenga *theatre* katika Hospitali ya Halmashauri ya Nsimbo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Hospitali ya Halmashauri ya Nsimbo haina jengo la upasuaji na Serikali kwa kulitambua hilo katika bajeti ambayo sasa tumeanza mchakato wake ya mwaka 2025/2026 itatenga shilingi milioni 265 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji katika Hospitali ya Wilaya ya Nsimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hoja hiyo

imeshapokelewa na Serikali na tayari imeshaingizwa kwenye mpango na tutakwenda kujenga jengo la upasuaji mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kwamba tuna utaratibu wa kujenga majengo ya upasuaji na wodi ya akinamama pamoja; lakini pia tunayo mipango ya kujenga majengo ya upasuaji pekee yake kwa ajili ya magonjwa ya wanaume, wanawake na wagonjwa wengine. Katika mpango wa Serikali, tumeanza na utaratibu wa kukamilisha majengo ya upasuaji ya akinamama na wodi zao, na baadaye tutajenga majengo ya upasuaji *general*, pamoja na wodi za wanaume, wanawake na watoto. Hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa mama Lupembe kwamba, mpango huo upo na tutahakikisha kwamba tunajenga majengo hayo ili tupate huduma bora katika Wilaya ya Nsimbo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 179

**Upungufu wa Vifaa Tiba na Watumishi Nchini**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaipatia ufumbuzi changamoto ya upungufu wa vifaa tiba na watumishi kwenye baadhi ya vituo vya afya nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba pamoja na kuajiri na kuwapangia vituo vya kazi wataalam wa kada mbalimbali za afya katika ngazi ya msingi kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024, Serikali ilitoa shilingi bilioni 187.37 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi bilioni 66.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na hadi kufikia Disemba, 2024 jumla ya shilingi bilioni 43.13 zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kuajiri wataalam wa kada za afya ambapo katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2023/2024, jumla ya wataalam wa kada za afya 25,917 wameajiriwa na kupangiwa vituo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira na kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na juhudi kubwa ambazo zinafanywa na Serikali ya kuhakikisha kwamba wanaboresha huduma za afya kwa maana ya kuwepo na vifaa tiba vya kutosha bado kumekuwa kuna changamoto ya vifaa. Baadhi ya *dispensary* na vituo vya afya akinamama wajawazito wananunua vifaa kwa ajili ya kujifungulia na Sera ya Afya inasema mama mjamzito anatibiwa bure. Swali la kwanza; je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika Mkoa wa Shinyanga kuna changamoto kubwa ya watumishi: Msalala, Ushetu, Kahama, Shinyanga Vijijini, pamoja na Shinyanga *Municipal*. Kuna sehemu unakuta watumishi wengi, sehemu nyingine wachache. Je, ni nini kauli ya Serikali kwa vituo vya afya

na zahanati kufanya *reallocation* ya watumishi ili sehemu zingine ambazo hazina watumishi, ziweze kupata watumishi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna vituo vya afya ambavyo vinatoa huduma na Sera ya Afya inaelekeza kwamba, huduma kwa akinamama wajawazito, watoto wa umri chini ya miaka mitano na wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea ambao hawana uwezo wa kifedha, wanatakiwa kupata matibabu bure. Serikali imeendelea kutekeleza sera hii kwa ufanisi

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunafahamu kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava bado kuna changamoto kwenye baadhi ya vituo kuwatoza akinamama wajawazito wanapokwenda kupata huduma hususani za kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuelekeza halmashauri zote kote nchini kwamba ni maelekezo na kauli ya Serikali kwamba lazima wahakikishe vifaa vyote vya muhimu kwa ajili ya huduma za kujifungua zinapatikana vituoni. Akinamama wajawazito wakienda kupata huduma hizo wasitozwe fedha yoyote lakini *gloves* na vifaa vingine vyote lazima vipatikane. Kwa sababu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa mabilioni ya fedha kwa ajili ya dawa na vifaa tiba. Kwa hiyo, ni wajibu wao kuhakikisha kwamba vifaa hivyo vinapatikana katika vituo vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na upungufu wa watumishi kwenye Halmashauri ya Kahama, Msalala, Shinyanga Vijijini na *Municipal*, ni kweli lakini hii Serikali imeendelea kuajiri watumishi. Kwa kipindi cha miaka minne iliyopita zaidi ya watumishi 25,917 wameajiriwa na hivi karibuni watumishi

wameajiriwa na kupelekwa kwenye halmashauri zote zikiwemo hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, zoezi hili ni endelevu, tutaendelea kuajiri watumishi na kuwapeleka maeneo yote ya upungufu ili kuboresha huduma. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 180

**Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya Upuge – Uyui**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakipatia Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya cha Upuge – Uyui?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za rufaa za wagonjwa, ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025 Serikali imenunua na kusambaza magari 382 ya kubebea wagonjwa kwenye halmashauri kwa kuzingatia mahitaji, ambapo kila jimbo limepokea angalau gari moja la kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ilipokea magari matatu ya kubebea wagonjwa ambayo yamepangwa kutoa huduma katika Hospitali ya Wilaya, Kituo cha Afya Igalula na Loya. Aidha, Kituo cha Afya Upuge - Uyui kina gari la wagojwa ambalo ni chakavu hali inayopelekea kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa magari ya wagonjwa na kuyapeleka kwenye vituo vyenye uhitaji zaidi kikiwemo Kituo cha Afya cha Upuge – Uyui, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; Kituo cha Afya cha Upuge hakijapata kuwa na gari la wagonjwa, isipokuwa gari bovu la halmashauri, ambalo walienda wakali-*pack* pale na kituo kile kinahudumia kata tatu. Je, Serikali sasa iko tayari kutambua kituo kile hakina gari la wagonjwa wala hakijawahi kupata gari la wagonjwa linalofanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa vile Kituo cha Afya cha Upuge kinahudumia watu zaidi ya 30,000 na hakina huduma ya *X-ray* wala *Ultrasound*, isipokuwa zinapatikana katika hospitali ya wilaya ambayo ipo kilometa 15 hadi 20 kutoka pale. Je, Serikali iko tayari kupeleka gari la wagonjwa katika mgao unaoendelea? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Almas Maige amekuwa akifuatilia mara kadhaa kuhusiana na uhitaji wa gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Upuge na mara kadhaa tumekaa naye na tumekubaliana kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu, kwamba tayari tumeingiza kwenye orodha ya vipaumbele, vituo vya afya vipaumbele, ambavyo vitapelekewa magari ya wagonjwa, ni pamoja na Kituo cha Afya cha Upuge, hatua za utekelezaji zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali imeweka mpango wa kukamilisha majengo ya huduma na kuweka vifaa tiba muhimu ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Nimhakikishie kwamba, katika kipindi cha miaka hii mitatu, Serikali imenunua *Digital X-Ray* zaidi ya 250 na kusambaza kwenye vituo vya afya na hospitali za halmashauri. Kituo hicho alichokitaja Mheshimiwa Mbunge kitapewa kipaumbele ili kipate mashine ya *Digital X-Ray* ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba.

Na. 181

**Kutofautisha Kaya Maskini Vijijini na Mjini katika Kuunganisha Umeme Nchini**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, Serikali inatofautishaje Kaya Maskini Vijijini na Mijini katika kuwaunganishia umeme nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* na *EWURA* imeweka mwongozo wa gharama za kuunganisha umeme kwa wateja, ambapo gharama hizo hutofautiana kulingana na hali ya eneo. Kulingana na mwongozo huo, maeneo yanayotambuliwa kama miji na vijiji miji, gharama ya kuunganisha umeme ni shilingi 320,960 na kwa maeneo ya vijiji gharama ya kuunganisha umeme ni shilingi 27,000, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru Serikali kwa majibu iliyotoa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni kutofautisha maskini hawa wa mijini na vijiji miji ni kutowapatia haki maskini ile fursa ya kujiinua kiuchumi kwa kupata nishati ya umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa maskini hawa katika pande zote za vijijini na mijini pia wanatambuliwa katika mpango wa Serikali unaoitwa *TASAF* na fedha nyingi zinatumika katika kuwalipa. Je, Serikali haioni sasa kupitia *TASAF* iendelee kuwapa ile hali na haki ya kutumia shilingi 27,000 kuwaunganishia umeme hawa wanaoishi kwenye miji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge na naomba niyajibu kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kupeleka umeme inatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha kwa *category* tofauti tofauti. Miradi ambayo tunapeleka kwa 27,000, ni miradi ambayo imekuwa *categorized* kwa ajili ya miradi ya vijijini, ni miradi ambayo Serikali inaweka ruzuku ili hawa wananchi waweze kupata umeme kwa gharama nafuu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maeneo ya miji na vijiji miji tuna miradi mingine ya *peri-urban*, namna ambavyo tunawasaidia wananchi ambao uwezo wao wa kuunganisha umeme ni kidogo ni kupitia kupeleka miradi kwa karibu. Kwa mfano maeneo ya miji, tunapeleka miradi ya *peri-urban* na wanaunganishiwa kwa shilingi 27,000, lakini ni lazima aunganishe katika kipindi ambacho miradi hii inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata kwenye maeneo ya miji tunapeleka miradi hii, hususani kwa maeneo ya pembezoni ili

wananchi na wenyewe waweze kupata umeme kwa gharama ambayo ni himilivu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hii miradi tunaitekeleza kwa aina tofauti tofauti kulingana na maeneo ili kuendelea kumpa ahueni mwananchi katika kuunganisha umeme. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga aulize swali lake.

Na. 182

**Lango la Kaskazini la Hifadhi ya Taifa Mkomazi kuanza Kutumika**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafungua rasmi na kuanza kutumika Lango la Kaskazini la Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi lililojengwa katika eneo la Ndea Wilayani Mwanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufunguzi wa Lango la Kaskazini la Hifadhi ya Taifa Mkomazi lililojengwa katika eneo la Karamba – Ndea, Wilayani Mwanga ulipangwa kufanyika tarehe 27 Disemba, 2024 pindi matengenezo ya kuiboresha barabara ya kuingilia kwenye lango hilo kwa kiwango cha changarawe kukamilika mwezi Novemba, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kufuatia mvua kubwa zilizokuwa zikinyesha hifadhini na kwenye maeneo

yanayozunguka Hifadhi ya Taifa Mkomazi, matengenezo ya kuiboresha barabara kwa kiwango cha changarawe ili iweze kutumika kwa shughuli za utalii yalishindikana kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa matengenezo ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 4.5 kutoka Lango la Ndea hadi mpakani mwa Hifadhi ya Taifa Mkomazi upande wa Wilaya ya Mwanga, yanaendelea. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari, 2025 na mara baada ya kukamilika kwa matengenezo hayo Wizara imepanga ufunguzi rasmi wa Lango la Karamba – Ndea ufanyike mwezi Machi, 2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, sehemu anayoizungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo inatengenezwa sasa hivi na ni kweli mkandarasi yuko *site* hata jana nimepata uthibitisho huo ni kutoka pale kwenye lango mpaka kufika mpakani mwa Wilaya ya Mwanga na hifadhi. Sasa, kipo kipande cha kutoka pale kwenye mpaka kufika sehemu inaitwa Nadung'oro ambapo ndiyo ndani ya Kijiji cha Ndea ni kama kilometa nne, ilishatengenezwa lakini kwa sababu haijatumika muda mrefu ina maeneo korofi. Je, Serikali inatuambia nini juu ya ukamilishaji wa kipande hicho kutoka pale kwenye mpaka wa hifadhi mpaka kufika Nadung'oro ili wananchi wa Mwanga waweze kufika kwa urahisi kwenye lango hilo litakapofunguliwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kipande anachokizungumzia, kimsingi siyo kilometa nne tu ni kilometa 13.5

ambazo zinasimamiwa na wenzetu wa *TARURA* kwa upande wa Mwanga. Taarifa tulizonazo ni kwamba kipande kile kilifanyiwa kazi mwaka 2024, lakini kwa sababu barabara ile ilikuwa haitumiki imeota majani na haiwezi kutumika kiurahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa sababu sisi tuna *interest* na eneo hilo ili kuweza kuingia kwenye hifadhi na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameomba tuone jinsi ambavyo tunaweza kushughulikia kipande hicho, tumelichukua wazo lake tutawasiliana na wenzetu wa *TARURA* ili waweze kutupa kibali tuweze kukwangua na kusafisha eneo lile ili barabara iweze kupitika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, aulize swali lake.

Na. 183

**Hitaji la Kituo cha Forodha Kijiji cha Muhange, Nyabibuye na Malenga**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuweka Kituo cha Forodha katika Kijiji cha Muhange, Nyabibuye na Malenga ili kuongeza kipato kupitia forodha mipakani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Serikali inatatua changamoto ya kukosekana kwa huduma za kiforodha katika Vijijiji vya Muhange, Nyabibuye na Malenga imepeleka Maafisa wa Forodha wawili eneo la Muhange kwa ajili ya huduma za forodha. Maafisa wanaohudumia Kituo cha Nyaronga wataanza kuhudumia Nyabibuye kwa awamu kabla ya kufungua

ofisi ya huduma na eneo la Malenga litahudumiwa na maafisa kutoka Muhange.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili modogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kukosekana kwa watumishi katika maeneo ya mpakani hasa katika mipaka ya Muhange, Nyabibuye na Malenga kunapelekea Serikali kupoteza fedha nyingi kwa sababu hazina wakusanyaji. Sasa, katika majibu yake ametaja watumishi wawili kwenda kuhudumia maeneo matatu tofauti ambayo yako mbali. Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi ili waweze kutosheleza kwa kila eneo ambalo nimelitaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ili watumishi waweze kufanya kazi vizuri ni pamoja na uwepo wa ofisi, nyumba pamoja na huduma kama ya usafiri; je, ni lini sasa Serikali itajenga ofisi za forodha na nyumba za watumishi ikiwa ni pamoja na uwepo wa magari katika mipaka ya Muhange, Nyabibuye na Malenga? Ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alilolisema ni kweli kwamba watumishi wawili watakuwa kidogo kwa maeneo matatu, lakini tumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni ametoa kibali cha watu zaidi ya 1,000 ambao wapo katika mchakato wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato huu wa ajira utakapokamilika tutapeleka vijana hao (watumishi) katika

maeneo hayo matatu aliyoyataja wa kutosha kabisa ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kwenye vituo hivyo hatuna ofisi, lakini ninatoa maelekezo kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania apeleke vijana wafanye *survey* mwaka ujao wa fedha tuanze kujenga walau kituo kimoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi.

Na. 184

**Namna Zanzibar Inavyonufaika na Ufadhili Kimataifa**

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM K.n.y. MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza:-

Je, ni miradi gani ya umwagiliaji inayofadhiliwa na mashirika ya kimataifa ambayo Zanzibar inanufaika nayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imenufaika na ufadhili wa mashirika ya kimataifa katika miradi ya umwagiliaji inayolenga kuongeza uzalishaji wa kilimo na kuboresha maisha ya wakulima wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa miradi inayotekelezwa ni Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Zanzibar, ambao unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya *Exim* ya Korea ambapo umefadhiliwa kupitia mkopo wa awali wa Dola za Kimarekani 50,000,000 na mkataba wa nyongeza wa Dola za Kimarekani 18,100,000. Utekelezaji wa mradi huu umefikia 98% na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 8 Juni, 2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimeridhika na majibu ya serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 185

**Waliopoteza Maisha kwa Ajali ya Pikipiki 2022-2024**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Je, wananchi wangapi wamepoteza maisha kutokana na ajali za pikipiki kati ya mwaka 2022 hadi 2024?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2022-2024 jumla ya wananchi 1,113 wamepoteza maisha kutokana na ajali zilizosababishwa na pikipiki kwa mchanganuo ufuatao: madereva wa pikipiki waliopata ajali na kufariki ni 759; abiria waliopanda pikipiki na kupata ajali zilizosababisha vifo vyao ni 283; na wananchi waliokuwa wanatembea kwa miguu kandokando ya barabara au njiani, ama waliokuwa wanavuka barabara na kupata ajali ya kugongwa na pikipiki na kufariki dunia ni 71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa madereva wote wanaoendesha pikipiki kuzingatia sheria ya usalama barabarani ili

kupunguza ajali zinazoathiri wananchi wengi na kupunguza nguvu kazi katika Taifa letu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; idadi ya wananchi 1,113 ni kubwa sana, je, ni nini mkakati wa Serikali kuzuia ili vifo hivi ambavyo vinazuilika visitokee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; baadhi ya waendesha bodaboda wamekuwa wakipakia abiria zaidi ya mmoja kwa jina maarufu la mshikaki na hivyo kusababisha wale ambao wamepanda katika bodaboda hizo inapotokea ajali inawezekana kama ni wanne au watano wote wanaweza wakapoteza maisha. Je, Serikali haioni umefika wakati wa kupiga marufuku upandaji wa mishikaki ili kunusuru wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, suala la ajali ni kweli linaumiza Watanzania wengi na kupunguza nguvu kazi. Ninatoa wito kwa Kamanda wa Usalama Barabarani kuzingatia kusimamia Sheria za Usalama Barabarani. Pia, madereva wote kuhakikisha kwamba wanasimamia Sheria za Usalama Barabarani na kuzifuata. Vilevile, abiria, watembea kwa miguu na wadau wote wanaotumia barabara wahakikishe kwamba wanasimamia Sheria za Usalama Barabarani ili kuepuka ajali ambazo siyo za lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu abiria zaidi ya mmoja, ninamwelekeza Kamanda wa Polisi wa Usalama Barabarani kusimamia sheria. Pili, wadau wote, watembea kwa

miguu, abiria wote na Watanzania tusikubali kupanda pikipiki zaidi ya mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila mtu achukue hatua za tahadhari kwa sababu mnapokuwa zaidi ya mmoja inapotokea ajali mnafariki wote. Kwa hiyo, ninatoa wito kwa abiria wote, unapoona kuna abiria kwenye pikipiki, basi usipande na wewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 186

**Kurudisha Somo la *Domestic Science* Shule za Msingi Nchini**

**MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarudisha Somo la *Domestic Science* katika Mtaala wa Elimu ya Shule za Msingi Nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, somo la sayansi kimu (*domestic science)* lilianzishwa baada ya mitaala kubadilishwa mwaka 1979 kufuatia Azimio la Musoma ikiwa ni kutekeleza kauli mbiu ya siasa ni kilimo na elimu kwa wote. Somo hili la sayansi kimu liliboreshwa zaidi na maudhui yake kuingizwa katika somo jipya la stadi za kazi mwaka 1997.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilikuwa ni pamoja na kupunguza wingi wa masomo kutoka masomo 13 hadi masomo saba kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mtaala ulioboreshwa mwaka 2023 maudhui yanayoshabihiana na somo la sayansi kimu yameboreshwa zaidi kwa kuzingatia mahitaji ya jamii, kukua kwa sayansi na teknolojia pamoja na soko la ajira. Hivyo, maudhui hayo kwa ngazi ya elimu ya msingi yapo kwenye somo la sanaa na michezo, ambalo ni somo la lazima na linafundishwa kuanzia darasa la tatu hadi la sita. Aidha, kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne kuna mkondo maalum unaofundishwa masuala ya chakula na lishe ambao umejikita kuendelea kujenga maarifa katika eneo hili. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ninaomba nichukue nafasi hii kulipongeza sana Azimio la Musoma. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kama Azimio la Musoma lilikuwa ni zuri sana lenye kuelimisha, wanafunzi walikuwa na uwezo wa kujua kupika, usafi na hata kujishonea nguo zao wenyewe tofauti na sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami tuanzishe shamba darasa kwa kuteua shule moja pale Tabora ili kuweka mtaala kama huu wa Azimio la Musoma ili kuwa mfano kwa shule nyingine ili vijana wetu warudi kule tulikotoka sisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Aziza Sleyum na nitajibu yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la masomo pamoja na mitaala ni suala ambalo ni *dynamic* siyo *static* kwa maana kwamba ni lazima kufanya maboresho na marekebisho mara kwa mara. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maazimio yote au mitaala yote ni bora au mizuri kulingana na muda ambao mitaala hiyo imeweza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninamweleza katika mfumo wa sasa ambao tumefanya maboresho ya sera pamoja na mitaala inafanya elimu yetu ya lazima iwe ni ya miaka 10. Miaka sita shule za msingi na miaka minne katika shule za sekondari. Kwa hiyo, katika mfumo wetu huu wa sasa, wanafunzi wote watakaomaliza watapata ujuzi utakaowawezesha kujitegemea. Katika, darasa la kwanza na la pili, watoto watajifunza hayo masuala ya kushona, kufuma pamoja na mitindo na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la pili alilolizungumza kuhusu Tabora kwamba tutengeneze *pilot,* ninadhani baada ya maswali tunaweza tukakutana na Mheshimiwa Mbunge, tukaangalia hilo wazo lako na ushauri wako, ni namna gani tunaweza kutekeleza kwa wakati. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 187

**Ujenzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Mwalimu Nyerere – Pemba**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia wapi katika mpango wa ujenzi wa Chuo Kikuu kishiriki cha Mwalimu Nyerere pamoja na hosteli Pemba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2022, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikipa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere eneo lenye ukubwa wa hekta 11.2 katika eneo la Mtumbi Pujini, Chakechake, Pemba kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kampasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 Serikali ilianza ujenzi kwa kuanza na madarasa 10 yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,800 ambapo ujenzi wake ulishakamilika. Serikali inaendelea na ujenzi wa awamu ya pili unaohusisha ujenzi wa jengo la utawala ambao umefikia 95% na ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara lenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,000 kwa mara moja ambao umefikia 60%. Serikali inatarajia kukamilisha ujenzi huu mnamo Aprili, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kukamilika kwa baadhi ya majengo, chuo kimeshaanza shughuli za utoaji wa mafunzo na ujifunzaji. Aidha, katika awamu zijazo Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa hosteli na miundombinu mingine katika chuo hiki. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini ninaomba nipate ufafanuzi. Swali la kwanza; huo utekelezaji wa hayo mafunzo upoje na umeanza vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali haioni haja sasa ya kutoa orodha yote ya hivi vyuo vikuu vipya ilivyovianzisha ili tujue vimefikia kiwango gani cha utekelezaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba Serikali tayari imefanya ujenzi na baadhi ya majengo yamekamilika na mengine yanaendelea kukamilika. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeanza kutoa mafunzo katika chuo hiki katika Kampasi yetu ya Pemba na mpaka tunavyozungumza sasa hivi kuna jumla ya wanafunzi 218 kwa mgawanyo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi 218 ni wa astashahada; 145 ni wa stashahada; na 30 ni wa shahada. Aidha, wahadhiri waliokuwepo katika kampasi ile ni 24 na watumishi wa kawaida ni 14. Kwa hiyo, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ipo kazini nimwondoe wasiwasi na kazi kule inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu orodha, ninaomba Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu liridhie kwamba tuandae orodha hii na miradi hii ya vyuo vikuu katika maeneo yote inakotekelezwa na kujua *status* yake katika kila eneo kuna asilimia ngapi za utekelezaji katika ujenzi wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 188

**Kuanzisha Mfuko Maalum wa Mikopo wa Elimu ya Juu**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itaanzisha Mfuko Maalum wa Mikopo ya Elimu ya Juu *(Revolving Fund)* ili kuongeza idadi ya wanufaika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu inatolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliyoanzishwa mahsusi kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wa Kitanzania wenye uhitaji na wanaostahili kupata mikopo na ruzuku ili kumudu gharama za masomo ya elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inatumia fedha zinazokusanywa kutoka kwa warejeshaji walionufaika kama Mfuko wa Mzunguko ili kuwezesha wanafunzi wenye uhitaji waweze kupata mikopo. Hata hivyo, Serikali ipo katika mpango wa kufanya mapitio ya kina *(comprehensive review)* ya Bodi ya Mikopo ili kuwezesha wahitimu walionufaika kurejesha mikopo yao kwa urahisi. Mapitio haya yakikamilika yataimarisha mifumo ya urejeshaji mikopo na kuifanya Bodi ya Mikopo kuwa stahimilivu katika kujiendesha na kuongeza mapato pamoja na kuongeza idadi ya wanufaika kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini hii *comprehensive review* inayofanyika itakamilika na kuleta majawabu katika Bunge hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni kwa namna gani hii *comprehensive review* imezingatia uhitaji wa wanafunzi wote wanaonufaika na mikopo hii katika kuhakikisha kwamba wote wananufaika na wanapata mikopo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna Sekiboko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *comprehensive review* kwa upande wa Bodi ya Mikopo tumeshakamilisha mwezi huu wa Februari kwa ujumla wake na kwa sasa tunafanya mapitio ya Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mapitio ni kwa sababu shughuli za *TEA* na Bodi ya Mikopo zilikuwa kama zinalingana au zinafanana. Tumeona ni vyema vilevile tufanye mapitio ya Mamlaka ya Elimu ili kuweza kubaini zile shughuli ambazo zinashabihiana kuweza kuona kama tunaweza tukaziunganisha zikafanyika kwa pamoja. Kwa hiyo, mapitio haya ya Bodi ya Mikopo pamoja na *TEA* yatasaidia kuwa na muundo na utaratibu mzuri wa kuendesha Mfuko wetu huu wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mapitio yote haya mawili yatakapokamilika sasa, kwa maana ya *TEA* na yale ya Bodi ya Mikopo, lengo kuu ni kubainisha vile vyanzo vya mapato. Tutakapobainisha vyanzo vya mapato, tafsiri yake ni kwamba, tutaongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato pamoja na urejeshaji wa ile mikopo ambayo imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, mapato yote yatakuwa yameongezeka. Tunaamini kabisa baada ya mapitio haya na kubaini vyanzo vya mapato na kuongezeka kwa vyanzo vya mapato yetu, tafsiri yake ni kwamba, tunaenda kuongeza wigo wa wale ambao watakuwa wananufaika na mikopo hii au watakaokuwa wanapata mikopo kwa kiasi kikubwa sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, aulize swali lake. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, hayupo! Kwa niaba, yupo.

Na. 189

**Matumizi Mabaya ya Laini za Simu za *TTCL***

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la laini za simu za *TTCL* kutumika zaidi kutapeli wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha tatizo la matumizi mabaya ya laini za simu, ikiwemo laini za *TTCL*, linamalizika. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Usajili wa laini kwa alama za vidole. Mfumo wa usajili wa laini kwa alama za vidole umelenga kudhibiti laini za simu zinazotumika kwa udanganyifu kwa kuhakikisha kila laini inahusishwa moja kwa moja na mmiliki wake halali;

(ii) Kufuatilia na kufungia laini zinazotumika kwa uhalifu. Serikali kupitia *TCRA* imeweka mifumo ya kufuatilia matumizi ya laini za simu na kuzifungia zile zinazobainika kutumika kwa ulaghai;

(iii) Kutoa elimu kwa umma. Serikali na wadau mbalimbali wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu jinsi ya kutambua ujumbe wa kitapeli na kuripoti matukio hayo kupitia namba 15040; na

(iv) Ushirikiano na watoa huduma za mawasiliano. *TTCL* na watoa huduma wengine wanashirikiana na Serikali kuhakikisha kuwa, laini zinazotumika kwa ulaghai zinadhibitiwa mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na kwa kweli, niseme tu kwamba, Serikali imekuwa inajitahidi sana kwenye eneo hili. Swali la kwanza; sasa, *concern* yetu kubwa ilikuwa ni pamoja na kuzifungia *line*, kwa nini hao matapeli ambao wanatapeli wananchi kwa kutuma ujumbe mfupi "tuma, halafu jina litatokea fulani", wasikamatwe na kushtakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni kwa nini mitandao mingine, kama *Vodacom*, *Airtel,* wamefanikiwa wao wenyewe kudhibiti hali hiyo? Kwa nini *TTCL line* zake ndiyo zinatumika zaidi kwenye utapeli wa aina hiyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napokea shukrani zako na kukiri kwamba, sisi kama Serikali, tunafanya kazi kubwa sana kuhakikisha utapeli mitandaoni unakwisha. Vilevile kukamatwa na kushtakiwa, tayari wenzetu wa *TCRA* wameweza kudhibiti kwa sehemu kubwa, wachache wameweza kufikishwa kwenye vyombo vya dola na sheria imeendelea kuchukua mkondo wake. Hatutangazi kwa sababu, zoezi linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwa nini *TTCL* inatumika zaidi; Mheshimiwa Mbunge nadhani ni *experience* yako binafsi, lakini ni mitandao yote ya watoa huduma inatumika na laini nyingi tunazozikamata siyo za *TTCL* peke yake ila hata watoa huduma wengine. Laini hizo zinaendelea kudhibitiwa, hivyo ninakutoa hofu na kwa kuzingatia *TTCL* ni taasisi ya Serikali, iko moja kwa moja ndani ya Wizara, tutaendelea kuweka nguvu na *TCRA* tutahakikisha tatizo hili la utapeli, kama tulivyoongea wiki iliyopita,

Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa alisimama hapa, tutaendelea kulishughulikia kuhakikisha linakoma kabisa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, aulize swali lake.

Na. 190

**Ujenzi wa Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Omugakorongo – Kigarama hadi Murongo utaanza baada ya kutangazwa upya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni ya ujenzi wa Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (kilometa 110); Sehemu ya Murongo hadi Businde kilometa 53.4 imetangazwa upya baada ya zabuni ya awali kukosa Wakandarasi wenye sifa. Zabuni mpya ilitangazwa tarehe 6 Oktoba, 2024 na kufunguliwa tarehe 12 Desemba, 2024. Kwa sasa kazi ya uchambuzi wa zabuni inaendelea na inatarajiwa kukamilika katikati ya mwezi Februari, mwaka huu wa 2025 na baadaye hatua za kumkabidhi mkandarasi zitaendelea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; mlisema Barabara hiyo ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo inajengwa kwa awamu

mbili, awamu ya kwanza umesema imeshatangazwa, awamu ya pili ambayo inatoka Omugakorongo – Businde itatangazwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo, mkandarasi alishalipwa tangu mwezi Septemba na alikabidhiwa ile barabara, lakini mpaka sasa hivi bado hajaanza, hatujamwona *site*. Shida iliyosababisha asianze kazi hiyo ni nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza, ni kweli kwamba, Barabara ya Murongo – Omugakorongo ndiyo barabara kuu ambayo inaunganisha Tanzania na Uganda kupitia Kyerwa. Tayari tumeshatangaza kipande cha kwanza ambacho tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipande cha pili, tumeshakamilisha usanifu na tunaendelea kutafuta fedha ili tuweze kukamilisha kilometa zote 110 tukiamini kwamba, baada ya kukamilisha, basi upande huo tutakuwa tumekamilisha *trunk road* kama ilivyo sera yetu ya kuunganisha kwa kiwango cha lami barabara zinazounganisha nchi na nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara aliyoitaja ya pili, ya Omurushaka – Nkwenda. Tayari tumeshamlipa mkandarasi na taarifa nilizonazo ni kwamba, mkandarasi yuko kwenye hatua za maandalizi ya awali, kwa maana ya *mobilization*. Kama kutakuwa na changamoto ya kuchelewa kwa sababu, tulishamlipa basi, Mheshimiwa Mbunge, tuweze kuonana naye, ili tuhakikishe kwamba, tunamsimamia. Ameshalipwa, aweze kwenda *site* na kuanza kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, aulize swali lake.

Na. 191

**Ujenzi wa Daraja la Kisorya – Lugezi**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, ni hatua ipi imefikiwa na Serikali kuanza ujenzi wa Daraja la Kisorya – Lugezi linalounganisha Wilaya ya Ukerewe na Bunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kwa ajili ya Daraja la Kisorya – Lugezi na Barabara unganishi ya Nansio – Rugezi yenye urefu wa kilometa 11. Ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara unganishi kutoka Nansio hadi Rugezi, yenye urefu wa kilometa saba umeanza mwezi Februari, 2024. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua iliyokwishachukua ya ukamilishaji wa kivuko, pamoja na hatua hiyo ya upembuzi na upembuzi yakinifu kwenye daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kutokana na umuhimu wa daraja hili wa kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Ukerewe, Serikali iko tayari sasa kuweka kwenye bajeti ya mwaka ujao 2025/2026 ili ujenzi wa daraja hili uweze kuanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mkataba wa Barabara Unganishi kati ya Rugezi – Nansio ulitakiwa kukamilika tarehe 4 mwezi wa Pili na mkandarasi huyo alishafika *site* akaanza kazi, akaharibu madaraja na barabara ile, hali ambayo imesababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wa Ukerewe. Sasa,

napenda Serikali iwaambie wananchi wa Ukerewe, nini hatma ya Barabara hii ya Kisorya – Rugezi? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe kwa pongezi kwa Serikali, lakini pia, namhakikishia kwamba, daraja hili, kama nilivyosema, tulishalisanifu. Ni daraja refu ambalo linavuka Ziwa Victoria, lenye zaidi ya kilometa 100. Serikali kwa kuona kwamba, itachukua muda ndiyo maana iliamua kujenga kivuko kipya, kikubwa ambacho kiko kwenye hatua za mwisho kabisa, kwa ajili ya kuunganisha Ukerewe na Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumekuwa tunatenga. Hata mwaka unaokuja tutatenga kwenye bajeti fedha ya kuanza ujenzi wa daraja hili la Kisorya – Rugezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ni kwamba, ni kweli mkandarasi na bahati nzuri ni mkandarasi mzawa ambaye amefanya kazi nzuri, ameshaleta maombi ya malipo yake ya fedha, hati za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu na tunafanya jitihada tumlipe ili aweze kuendelea na kuikamilisha hiyo kazi ambayo ameshaianza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 192

**Mfuko wa Kuimarisha Bei ya Mazao Nchini**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Mfuko wa kuimarisha bei za mazao, ili kusaidia wakulima wa pamba na mazao mengine bei inaposhuka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo kupitia Tangazo la Serikali, Na. 22 la Tarehe 20 Januari, 2023, baada ya kuidhinishwa na Waziri wa Fedha. Mfuko huo umelenga kuchochea ukuaji wa maendeleo ya Sekta ya Mazao ya Kilimo, kupunguza ukali wa bei ya mazao inaposhuka, kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo (mbegu bora, mbolea pamoja na viuatilifu), kuchochea uwekezaji katika shughuli za utafiti wa kilimo na kuwajengea uwezo wakulima, wasindikaji, Maafisa Ugani na watafiti wa kilimo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa bei ya mazao haya mwaka jana, hasa pamba, ilikuwa iko chini na mwaka huu 2025 wakulima hawana uhakika wa bei ya mazao hayo. Je, Mfuko huu wa Serikali ambao tayari umeanzishwa, unawasaidiaje wakulima kuwa na uhakika wa bei ya mazao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa huko nyuma tulikuwa na bei elekezi ya pamba, ikitangazwa na Serikali mwezi

wa Septemba ama wa Oktoba ili kuwahamasisha wakulima waweze kulima kwa wingi na kwa tija mwaka unaofuata. Je, Serikali inaonaje kurudisha utaratibu huo ili kuwahamasisha wakulima waweze kulima pamba kwa wingi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mawili mazuri kabisa kwa wakulima wa pamba. Jambo moja ambalo namhakikishia ni kwamba, endapo bei ya pamba mwaka huu itashuka chini ya kile kiwango ambacho kinatarajiwa, maana yake ni moja ya kazi ya huu Mfuko ni kutoa ruzuku kwa wakulima wa pamba, ili kuhakikisha wanapata bei nzuri. Kwa hiyo, Mfuko utafanya kazi yake kama ambavyo umeundwa kwa kusudi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kurejesha ule mfumo wa awali wa kuweka bei elekezi kati ya Mwezi Septemba na Oktoba, sisi huwa tunapokea maoni ya wadau na tukishayapokea tunayafanyia kazi. Kwa hiyo, kama watakuwa wameachana na soko huru, maana yake ni sasa sisi tutarudi tuzungumze nao. Kama wao watakubali, maana yake ni Serikali tutarudi katika mfumo wa awali. Kwa hiyo, kwa sasa tunapokea kama maoni ambayo tunaweza kwenda kuyafanyia kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 193

**Kufufua Skimu ya Umwagiliaji Kata ya Chela, Msalala**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Chela, Halmashauri ya Msalala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Chela ina skimu ndogo ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 100 ambayo chanzo chake cha maji ni chemchemi ya asili. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la watu, mwaka 2022, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala iligharamia upembuzi yakinifu na usanifu wa awali, kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na skimu ya umwagiliaji ya ukubwa wa hekta 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Halmashauri ya Msalala ipo kwenye mipango ya kutafuta fedha za kuwafidia wananchi wa maeneo ambayo bwawa hilo litajengwa. Aidha, skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Chela imewekwa katika mpango wa bajeti wa mwaka 2025/2026, kwa ajili ya kufanyiwa upembuzi na usanifu wa kina, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, lakini pia, ninaishukuru kwa ujenzi wa Skimu ya Mtambo ambao unaendelea. Swali langu la kwanza; Serikali iliahidi kufanya upembuzi yakinifu kwenye bajeti iliyopita katika Skimu ya Metrom, Longoi, Makeresho, Bwawa la Borutu, Skimu ya Ismail na Kikafu Chini. Je, ni lini sasa upembuzi yakinifu utafanyika kwenye skimu hizi, ili ujenzi uanze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tuna mifereji ambayo ni muhimu sana kwenye kilimo cha Wilaya ya Hai. Ni lini sasa Serikali itaanza kujenga mifereji hii ifuatayo, muhimu sana, kwenye Wilaya ya Hai; Mfereji wa Bwana Mganga, Toweru, Shombole, Sonu, Maseti, Mriri, Indindi, Mwasha, Mpendaroho, Isawero, Johari na Magadini Kati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Hai kwa kazi nzuri anayoifanya katika jimbo lake na kuwatetea wananchi, lakini namhakikishia tu kwamba, hizi skimu alizozitaja, Skimu ya Metrom, Longai, Makeresho, Kikafu Chini, zote tunaziingiza katika Mpango wa mwaka wa fedha 2025/2026, ili ziweze kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kwa ajili ya kupata gharama halisi tutafute mkandarasi na zianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, waambie wananchi wa Hai watakavyoendelea kukuchagua kuwa Mbunge, maana yake ni wawe na uhakika kwamba, skimu hizi zitakamilika kwa wakati, lakini vilevile, mifereji ambayo ameiainisha, tulishaipa kazi Tume ya Umwagiliaji kuifanyia vilevile upembuzi yakinifu, ili kupata gharama halisi tuweze kuwasaidia wananchi kwa kuijenga, waweze kutoa huduma kwa wakulima wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ndiyo majibu ya msingi ambayo sisi Serikali tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Hai, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya maswali.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujamalizia maswali yaliyobaki, kuna taarifa maalumu ya kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa nje ya Mkoa wa Dodoma kwa shughuli za kikazi kuanzia tarehe 10 Februari, 2025. Wakati ambao hatakuwepo, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Kazi Maalum, atakaimu nafasi hiyo ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi hapo atakaporejea Mheshimiwa Waziri Mkuu au atakaporejea Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, aulize swali lake.

Na. 194

**Kuanza Kutumika kwa Bandari ya Kwala, Kibaha Vijijini**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, lini Bandari ya Kwala itaanza kutumika kwa uhakika Kibaha Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala. Miradi mbalimbali imetekelezwa na kukamilika ikiwemo ujenzi wa reli mchepuko yenye urefu wa kilometa 1.3, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha zege yenye urefu wa kilometa 15.5 kutoka eneo la Kwala hadi Barabara Kuu ya Morogoro, ujenzi wa uzio wa eneo lenye ukubwa wa hekta 60, ambapo kati ya hizo hekta tano zimewekwa sakafu ngumu *(pavements),* kwa ajili ya kuweza kupokea makasha 3,500 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi wa Bandari Kavu ya Kwala, kumeiwezesha bandari hii kuanza kutumika rasmi kuanzia mwezi Agosti 2023, ambapo hadi mwezi Disemba, 2024 jumla ya makasha 684 yamepokelewa. Kati ya hayo, makasha 406 yamekwishakabidhiwa kwa wateja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, aulize swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru na pia naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa umuhimu wa Mji wa Kwala ambao una bandari kavu, una kongani kubwa ya viwanda, una Mji wa Magindu unakua kwa kasi, Mji wa Chalinze unakua kwa kasi. Je, Serikali haioni sasa ni muda sahihi wa kujenga kituo cha treni ya *SGR,* mahali ambapo treni zinapishana ili wananchi wa maeneo hayo wanaotaka kuingia kwenye Mji la Kwala waingie kirahisi na kupata huduma zinazostahili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Bandari Kavu ya Kwala kazi yake ni kupokea mizigo inayotoka kwenye bandari zingine na inayoingia pale kwa njia ya treni. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuiunganisha Bandari ya Kwala na Bandari ya Bagamoyo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwakamo kwa maswali yake ya msingi ambayo ameendelea kuyafuatilia na jinsi ambavyo anatusaidia kama sekta kuona umuhimu mkubwa wa eneo la Kwala pamoja na Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimhakikishie kwamba, tayari Serikali imekwishaona umuhimu mkubwa wa kuunganisha Bandari ya Kwala pamoja na reli zote tatu, kwa maana ya *Meter Gauge* ya *TAZARA* pamoja na *Meter Gauge* ya *TRC, Cape Gauge* ya *TAZARA* na *SGR*. Tayari kituo kimeshawekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kilometa 1.3 ya reli ya *meter gauge* imeshaunganishwa na katika eneo hilo husika. Hivyo, basi tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba eneo hili la Bagamoyo, eneo hili la Pwani ambalo ni kongani ya viwanda na linakwenda kuwa na uchumi mkubwa, linakuwa linaunganishwa moja kwa moja na reli hii ili kutoa mizigo sehemu moja kupeleka mizigo sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ya pili ni kuhusiana na bandari ya Bagamoyo namna gani inaweza kuunganishwa pamoja na Kwala. Moja, nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge, jinsi ambavyo Serikali imefanya kazi kubwa kuendelea kuboresha bandari nchini na hii inafanyika kwa sababu ya *potential* ya mizigo mingi iliyopo katika nchi jirani, ambapo ni muhimu tuboreshe bandari zetu ili tuweze kufikia masoko ya nchi zote zinazotuzunguka ikiwa ni pamoja na *central corridor,* nchi za kusini, kanda ya ziwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo pamoja na maboresho ya bandari zetu mbalimbali ambayo tumefanya ikiwemo Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mtwara, Tanga pamoja na bandari zilizopo katika Maziwa ya Tanganyika na Nyasa, Serikali imeona umuhimu wa Bandari ya Bagamoyo kwa sababu pamoja na kazi hiyo kubwa meli kubwa za *maximum* zinazoweza kutua katika bandari zetu ikiwemo Dar es Salaam ni za mita 320.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Bandari ya Bagamoyo ndiyo yenye uwezo mkubwa ya kuweza kupokea meli kubwa zaidi kwenda mpaka mita 400. Katika kutimiza hilo Serikali ina mpango wa kuunganisha Bandari ya Bagamoyo, Kwala na Bandari Kavu ya Kwala ili mizigo inayotoka sehemu mbalimbali duniani, ikitua pale Bagamoyo iweze kuunganisha moja kwa moja Kwala na kwenda sehemu mbalimbali inakohitajika ndani ya nchi yetu na nje ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini.

Na. 195

**Mnara wa Kuongozea Ndege Kiwanja cha Ndege – Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, lini mnara wa mawasiliano wa kuongozea ndege utajengwa katika Uwanja wa Ndege Mpanda?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kiwanja cha ndege kiwe na mnara wa kuongozea ndege kinahitaji kukidhi matakwa makubwa manne ambayo ni kuwa na ndege za ratiba maalum, kuwa na idadi kubwa ya miruko na mituo ya ndege, kuwa katika eneo lenye hali mbaya ya hewa hasa ambayo inaleta uono hafifu kwa rubani na sababu nyingine za msingi kama itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa Kiwanja cha Ndege Mpanda hakijaweza kukidhi matakwa yaliyoainishwa na hivyo huduma za kuongoza ndege zinazotua katika kiwanja hicho hutolewa kutokea mnara uliopo katika Kiwanja cha Ndege cha Tabora kama ilivyokasimiwa na kituo kikuu cha kuongozea ndege kilichopo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninalo swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Mpanda uko katika eneo zuri la kimkakati, kwa maana ya uchumi mpana ikiwa ni jirani na nchi ya DR-Congo. Serikali inasema nini kwa maana ya kuweka kwenye mipango yake uboreshaji wa Uwanja wa Ndege wa Mpanda, ikiwa ni pamoja na miruko na mituo sambamba na ujenzi huo wa mnara wa mawasiliano? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kulingana na uhitaji wa mara kwa mara, Serikali imeendelea kujenga minara ya

ndege katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ikiwa ni pamoja na Viwanja vya Julius Nyerere, KIA, Arusha, Dodoma, Mwanza, Iringa, Tabora, Tanga, Mtwara, Songea na maeneo mengine, lakini kulingana na uhitaji mkubwa minara mbalimbali inajengwa kwa sababu ikiwa ni pamoja na Shinyanga, Sumbawanga, Kigoma, Tabora, Msalato na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yako maeneo mengine ambayo tutaanza ujenzi sio muda mrefu, ikiwa ni pamoja na Tanga, Mtwara, Kigoma, Lindi na Lake Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge, Serikali imetumia fedha bilioni 1.4 katika Kiwanja cha Mpanda ambapo tumejenga *runway,* tumejenga jengo la abiria, tumejenga jengo la zimamoto na bado *control tower*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ambao ametimiza jukumu lake la msingi la Kibunge ambalo ni kuishauri na kuisimamia Serikali na kwamba ushauri wake na hoja yake, itafanyiwa kazi kulingana na mahitaji, kama ambavyo nimeainisha hapo juu ikiwemo ni pamoja na miruko ya ndege, ratiba maalum zilizoko, tukiona inafaa kwa wakati husika tutalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tumekamilisha maswali yetu kwa siku ya leo na sasa hivi nina matangazo hapa. Kwanza, nina tangazo la wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliokaa kwenye Jukwaa la Spika ambao ni wageni watatu wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia amabo ni Profesa Carolyne Nombo - Katibu Mkuu; Daktari Lyabwene Mutahabwa - Kamishna wa Elimu na wageni

wengine saba ni Wakurugenzi kutoka Wizara hiyo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni viongozi wa Wizara, yuko Ndugu Methusela Ntonda - Naibu Katibu Mkuu; Daktari Dkt. Emmanuel Ishengoma - Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa na wageni wengine 22 ambao ni maafisa, wahudumu na madereva kutoka Wizara hiyo, karibuni sana wageni toka Wizara hiyo. *(Makofi)*

Tuna wageni pia wa Waheshimiwa Wabunge; wageni watano wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed Mbunge ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoka Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Ibrahim Mpwapwa - Katibu wa CCM Wilaya ya Chamwino, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Mkoa wa Singida, wakiongozwa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Manyoni, Mwalimu James Mchembe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani ambao ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Singida Vijijini na Ndugu William Mwang'imba ameambatana na mke wake, Ndugu Juliana Missanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Ndugu Yohana Francis kutoka Wilaya ya Biharamulo Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Samahani nimeruka wageni wa Mheshimiwa Esther, kuna wageni sita wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni viongozi wa Bunge la Jumuiya ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*, karibuni sana, siwaoni wako wapi? Inawezekana hawajaingia.

Kuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kuna Ndugu Yohana Francis kutoka Wilaya ya Biharamulo Mkoa wa Kager ana tuna Ndugu Jeremiah Andrea kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 70 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Epiphany ya Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 32 na walimu wawili kutoka Chuo cha *St. Augustine,* Tawi la Arusha, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Arusha. *(Makofi)*

Wanafunzi 60 wanaosomea Udaktari kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* karibuni sana wanafunzi kutoka Chuo cha Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni wetu kwa leo asubuhi hii. Katibu tuendelee.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**MWENYEKITI:** Haya, tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kusoma taarifa,

naomba taarifa yangu hii iingie kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo wa Taarifa; Muundo wa taarifa hii umezingatia Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa sababu hiyo taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumiwa na Kamati kutekeleza majukumu yake pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja. Sehemu ya Pili, inafafanua kuhusu shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji, mafanikio na changamoto zilizojitokeza. Sehemu ya Tatu, inatoa maoni ya jumla na mapendekezo, ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi; na Sehemu ya Nne, ni hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa shughuli za Kamati na Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati. Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Kanuni ya 142(a) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 na kwa hiyo Kamati ilitumia njia kuu tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara pamoja na Taasisi inazozisimamia. Pili, kusoma na kuchambua taarifa za utekelezaji wa majukumu zilizowasilishwa na Wizara na Taasisi zilizo chini yake; na tatu kuandaa na kutoa maoni na ushauri kuhusu yatokanayo na taarifa za Wizara na Taasisi inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madhumuni ya Taarifa; kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Madhumuni ya Taarifa hii ni kubainisha mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Lengo ni kuonesha mambo yanayohitaji kuboreshwa ili Bunge liyajadili kwa kuzingatia majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Shughuli za Kamati. Kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge kwa niaba ya wananchi, lina jukumu kubwa la kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba inaweka utaratibu na msingi wa uwepo wa Kamati za Bunge na utekelezaji wa majukumu ya Kamati ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kanuni ya 137 kwa pamoja na Nyongeza ya Nane zinaweka msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 5(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake. Aidha, Nyongeza ya Nane, 7(1) (a) – (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hii ipo katika taarifa kamili iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili; Shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyobainika. Katika kipindi cha mwaka 2024/2025, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni ya 137 na Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1) (a) mpaka (d) ya Kanuni za

Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza ni pamoja na:-

(i) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara na taasisi inazozisimamia; na

(iv) Kushiriki semina za mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya ziara za ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipata wasaa wa kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Taasisi inazozisimamia. Aidha, Kamati ilifanikiwa kufanya ziara katika mikoa 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi 14; Mkoa wa Dar es Salaam miradi minne, Mkoa wa Singida miradi 10, Mkoa wa Morogoro miradi mitatu, Mkoa wa Dodoma miradi 12, Mkoa wa Iringa miradi tisa, Mkoa wa Njombe miradi mitatu, Mkoa wa Pwani miradi sita, Mkoa wa Rukwa miradi mitano, Mkoa wa Katavi miradi miwili, Mkoa wa Songwe miradi mitatu, Mkoa wa Manyara miradi minne, Mkoa wa Arusha, miradi minne minne Mkoa wa Kilimanjaro miradi miwili, na Mkoa wa Tanga, miradi miwili. Kama inavyoonekana kwenye oradha katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyotajwa baadhi yake ilitolewa taarifa wakati wa vikao vya Bunge la Bajeti. Aidha,

miradi iliyosalia ilitembelewa na kukaguliwa wakati wa vikao vingine vya Kamati vilivyofanyika baada ya Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Miswada na Maazimio. Katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 Kamati haikushughulikia Muswada wowote wa Sheria wala maazimio ya kuridhiwa na Bunge yanayotokana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushughulikia bajeti; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, mara baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilipata wasaa wa kupokea, kuchambua, kuhoji na kujadili taarifa za utekelezaji wa maoni ya Kamati na utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na kuchambua, kuhoji, kujadili na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara inayoisimamia kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya kina ya Uchambuzi wa Bajeti inayosimamiwa na Kamati pamoja na maoni na ushauri wa Kamati viliwasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bajeti uliomalizika mwezi Juni, 2024. Aidha, kwa maoni yale ambayo hayakutekelezwa, Kamati itaendelea kuyasisitiza maoni hayo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Agosti, 2024; Oktoba 2024; na Januari, 2025 Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa mbalimbali za Utendaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na taasisi zilizo chini yake. Taarifa zilizowasilishwa na kuchambuliwa na Kamati zimeelezwa kwa kina katika taarifa iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Disemba, 2024, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetekeleza shughuli zake kwa ufanisi, Wizara imefanikiwa katika uratibu wa masuala ya utekelezaji wa bajeti

katika halmashauri pamoja na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti za Mikoa yote 26 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabarani Vijijini na Mijini *(TARURA)*; wakati wa uchambuzi wa taarifa ya *TARURA* kuhusu utekelezaji wa majukumu yake ya kuboresha miundombinu ya Barabara nchini Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Barabara zilizoharibiwa na mvua za *El-Nino* kutofanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizoharibiwa na mvua za *El Nino* bado hazijafanyiwa matengenezo, wakati huo huo mvua zinazoendelea sasa na zinazotarajiwa kunyesha kipindi cha Februari – Mei, zinaweza kuongeza uharibifu wa miundombinu mbalimbali ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya *TARURA* inaonesha kuwa tathmini iliyofanyika juu ya uharibifu wa miundombinu uliosababishwa na mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya ilihitaji bilioni shilingi bilioni 883 ili kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mvua za *El-Nino*. Kamati imetaarifiwa kuwa Serikali imetenga na kutoa kiasi cha shilingi bilioni 83 kwa ajili ya urejeshaji wa miundombinu hiyo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga na kutoa fedha hiyo kwa ajili ya urejeshaji wa miundombinu ya barabara inayosimamiwa na *TARURA*. Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa fedha za dharura kwa wakati ili kuondoa uwezekano wa barabara hizo kuharibiwa zaidi na hivyo kuweza kuisababishia Serikali kutumia fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mabasi yaendayo kasi *(DART);* Kamati ilipokea taarifa mbalimbali za utendaji wa Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka *(DART)* ili kuweza kung'amua ufanisi wake katika kutatua changamoto za usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Katika uchambuzi wa taarifa hizo Kamati imebaini kuwa Wakala imeendelea kufanya vyema kwa kiwango chake kutoa

huduma kwa wananchi na vilevile kwa kuchangia fedha za mapato ya ndani kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa *DART* inakutana na changamoto ya kutokupelekewa fedha za makusanyo na *UDART*. Hivyo kupelekea kuwepo kwa mgogoro wa kimalipo kati ya *DART* na *UDART*. Katika mkataba wa uendeshaji wa Mradi wa Mabasi ya Mwendo Kasi ulioingiwa kati ya *DART* na *UDART* walikubaliana kuwa *UDART* atakusanya nauli na kutoa gawio kwa *DART*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kuna changamoto ya utekelezaji wa mkataba kwa *UDART* kutokupeleka gawio kwa *DART* kwa mujibu wa sheria kama ilivyo sehemu ya makusanyo. Hali hii inaathiri utekelezaji wa bajeti kwa upande wa *DART*. Kamati inaishauri Serikali kuzikutanisha pande hizi mbili na kukaa pamoja ili kutatua mgogoro huo ili kutekeleza Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2024 kama ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Jiji la Dar es Salaam. Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu utendaji wa Shirika la Maendeleo la Uchumi la Jiji la Dar es Salaam *(DDC)*. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa, *DDC* ni taasisi muhimu yenye majengo mengi na vitega uchumi vingi ambavyo huenda Serikali haivitilii maanani, kama vile majengo ya *DDC Keko*, *DDC Magomeni* na *DDC* Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa Shirika linatekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la biashara kwa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(PPP)* lenye urefu wa ghorofa sita. Kamati inapongeza juhudi hizi kwani zina lengo la kuongeza vyanzo vya mapato kwa shirika hilo. Kamati inashauri Shirika la *DDC* kuendeleza miradi yake kwa kutumia *(PPP)* ili kuendeleza maeneo yao kwa ajili kuongeza mapato ya shirika hilo. Kamati vilevile inaendelea kuishauri Serikali kuwa karibu na kuongeza usimamizi kwa Shirika hilo ili liweze kuteleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Masoko Kariakoo; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika la Masoko Kariakoo liliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 13.7. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 11 ni kutoka mapato ya ndani na shilingi bilioni 1.8 ni ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati kuhusu upokeaji wa fedha inaonesha kuwa hadi Disemba, 2024 Shirika lilipokea jumla ya shilingi milioni 738.8, sawa na asilimia 5.4 ya fedha zote za bajeti ambapo shilingi milioni 419.6 ni mshahara sawa na 25% na shilingi 208.3 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upelekaji huu wa fedha kwenda Shirika la Masoko ya Kariakoo hauoneshi hali nzuri kwa kuwa Shirika haliwezi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha kama ilivyopangwa kwenye bajeti na kwa wakati ili kuliwezesha Shirika hili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fedha kupelekwa kwa kiwango kidogo Shirika hili limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kiwango inachostahili kulingana na upatikanaji wa bajeti. Kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa Soko la Kariakoo Kamati ilibaini kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2024 Shirika limefanikiwa kuandaa mpangilio bora wa maeneo ya biashara katika soko linalokarabatiwa na linalojengwa tofauti na hapo awali kwa kuzingatia aina ya biashara zinazofanana kuuzwa katika eneo moja *(market segmentation)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa mradi huu ulitarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, mwaka 2023. Hata hivyo mradi huu haukuweza kukamilika kwa wakati kama ilivyokuwa imepangwa. Hadi kufikia Disemba, 2024 utekelezaji wa mradi ulifikia 93.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Serikali za Mitaa; katika uchambuzi wa Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati mwezi Agosti, 2024, Kamati imebaini chuo kinakabiliwa na changamoto

kadhaa ikiwa ni pamoja na upungufu wa watumishi, wingi wa wanafunzi usioendana na miundombinu hasa ya maradhi, ufinyu wa jengo la utawala pamoja na usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya kina kuhusu Chuo cha Serikali za Mitaa inapatikana katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; Bodi hii imepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na utoaji wa mikopo kwa halmashauri mbalimbali nchini. Kamati imebaini kuwa pamoja na Bodi hii kuwa na umuhimu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini mamlaka hizo hazichangii bodi hii sehemu ya amana zao. Aidha, Kamati imebaini pia kuwa halmashauri nyingi zinazokopa kwenye bodi hii hazirejeshi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu; katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuhudumia jumla ya walimu 273,736 wa shule za msingi na sekondari waliopo kwenye utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa taarifa ya Tume ya Utumishi wa Walimu iliyowasilishwa mbele ya Kamati Januari, 2025, Kamati imebaini kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu haitekelezi majukumu yake kama ilivyoelekezwa kwenye sheria iliyounda Tume hiyo kwa kuwa majukumu mengi ya Tume hiyo yanatekelezwa na taasisi nyingine za umma. Kamati inashauri Serikali kupitia upya Sheria iliyokiunda chombo hiki na kukiwezesha chombo hiki kutekeleza majukumu yake iliyopewa kisheria ili kiweze kuwa na tija kwa walimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utekelezaji wa Miradi na Programu mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari Nchini *(SEQUIP)*. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza Mradi wa

Kuboresha Elimu ya Sekondari *(SEQUIP)* kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Mkopo huu ni wa fedha za Kimarekani dola milioni 500 sawa na fedha za Kitanzania shilingi trilioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Kuboresha Elimu ya Sekondari *(SEQUIP)* ni Ujenzi wa Shule mpya za Sekondari za Bweni za Wasichana katika Mikoa yote nchini. Ujenzi wa shule hizi ulianza Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kamati inapongeza Serikali kwa ujenzi wa shule hizi ambazo ni ukombozi kwa mtoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya afya ya uzazi ya mama na mtoto katika Mikoa na Halmashauri. Awali ya yote Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutunukiwa Tuzo ya Heshima inayoitwa *The Global Goalkeeper Award* inayotolewa na *Gates Foundation* kama kuutambua mchango wa Tanzania kwenye mafanikio katika kutokomeza vifo vinavyotokana na ujauzito, vifo vya watoto wachanga, pamoja na lishe afya kwa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa za kidemografia ya viashiria vya afya na malaria ya mwaka 2022, vifo vya wajawazito nchini vimepungua kutoka 556 kwa kila vizazi 100,000 kwa mwaka 2015/2016 hadi vifo 104 katika kila vizazi 100,000 kwa mwaka 2021/2022. Hiyo ni sawa na upungufu wa vifo 76. Aidha, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vinaendelea kupungua ambapo kwa mwaka 2015/2016 vilikuwa 67 kwa kila vizazi 1,000 na mwaka 2021/2022 vilikuwa 43 kwa kila vizazi hai 1,000, sawa na kupungua kwa 36%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utengaji wa matumizi ya mapato ya ndani katika Sekta ya Kilimo na Mifugo. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikadiria kukusanya shilingi bilioni 215.1 katika vyanzo vya ushuru wa mazao ya kilimo na mifugo. Makadirio ya fedha zilizotakiwa kutolewa kuendeleza Sekta ya Kilimo ni shilingi bilioni 43.2. Hali halisi ya makusanyo kutoka vyanzo hivyo ni shilingi 226.8. Kutokana na

makusanyo hayo halisi na fedha ambazo zilitakiwa kutengwa kwa ajili ya kilimo ni bilioni 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30, Juni shilingi bilioni saba sawa na 16.41% zilitumika kuendeleza Sekta ya Kilimo na hivyo kutofikiwa lengo lililowekwa. Kamati inaona kuwa mamlaka hazijafanya juhudi za kutosha za kupeleka fedha hizo kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo. Kamati inashauri halmashauri zihakikishe kuwa fedha zinazopaswa kutengwa na kupelekwa ajili ya kilimo na mifugo zinapelekwa kwa utimilifu wake na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Maagizo ya Bunge. Kamati ilipokea na kujadili taarifa za Wizara inayoisimamia kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya Kamati ya mwaka 2023/2024 iliyosomwa na kujadiliwa na Bunge tarehe 13 Februari, 2024. Maazimio hayo yaliyotolewa kwa msingi wa matarajio ya wananchi kuhusu shughuli za umma na ustawi wa wananchi nchini. Kilichofanyika ni kuonesha matarajio na kuacha uhuru kwa utekelezaji ndani ya kipindi cha Februari, 2024 – Januari, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa kwa asilimia kubwa maazimio hayo yametekelezwa na yaliyobaki Kamati imefahamishwa kuwa mchakato wa utekelezaji wake unaendelea. Aidha, kwa maoni yale ambayo hayakutekelezwa Kamati itaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati: Maoni ya Jumla; kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizobainika katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Upungufu wa watumishi katika Sekta ya Elimu na Afya ni changamoto kubwa kwenye halmashauri nyingi. Kamati inashauri, Serikali kuendelea na utaratibu wa

kutoa ajira kwa watumishi wa kada za afya na elimu kwenye halmashauri nchini ili kupunguza tatizo hili; *(Makofi)*

(ii) Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha kina miundombinu chakavu ambayo yanakifanya chuo hiki kushindwa kutekeleza jukumu lake ipasavyo na hivyo kuleta athari kwa wanafunzi wanaosoma katika chuo hicho. Kamati inashauri kuwa Serikali itafute na kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya chuo hicho ambacho ni muhimu sana kwa utoaji wa elimu ya afya kwa Watanzania;

(iii) Bajeti zinazopitishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa shule, barabara, vituo vya afya, zipelekwe kwa wakati ili kuleta tija katika uendelezaji wake. Aidha, Serikali inapaswa kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wazembe wanaoshindwa kusimamia matumizi ya fedha zilizopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mahsusi; Uimarishaji wa Sekretarieti za Mikoa:

Kwa kuwa, Ofisi nyingi za Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo havina vitendea kazi;

Na kwa kuwa kutokuwepo kwa vitendea kazi katika ofisi za Waheshimiwa Wabunge majimboni kunasababisha Ofisi za Wabunge kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kuwaletea maendeleo wananchi wao;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itenge bajeti kwa ajili ya kununua vitendea kazi kwa ajili ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge zisizo na vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa Shirika la Elimu Kibaha.

Kwa kuwa, Serikali iliazimia kuvunja mashirika ya umma yasiyo na tija likiwemo Shirika la Elimu Kibaha;

Na kwa kuwa, Shirika la Elimu Kibaha bado ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu; na kwamba Shirika hili halikuundwa kwa lengo la kutengeneza faida;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Shirika la Elimu Kibaha liimarishwe ili liweze kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa katika sheria ya uundwaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaji wa fidia kwa ajili ya upishaji Miradi ya Mabasi ya Mwendokasi Dar es Salaam:

Kwa kuwa, ujenzi wa miundombinu ya *BRT* awamu ya tano na sita inachelewa kuanza kutekelezwa kutokana na wananchi walio kwenye maeneo ya ujenzi wa miundombinu hiyo kutokulipwa fidia;

Na kwa kuwa, kuchelewa huko kunasababisha gharama za utekelezaji wa miradi kuongezeka kutokana na mabadiliko ya kiuchumi nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe kulipa fidia katika maeneo yote yanayotakiwa kujengwa miundombinu ya *BRT* ambazo hazijalipwa ili miradi hiyo ijengwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutatua Mgogoro wa utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo kasi kati ya *DART* na *UDART*:

Kwa kuwa, mgogoro uliopo kati ya *UDART* na *DART* unasababisha ugumu wa utekelezaji wa Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2024;

Na kwa kuwa, kutokutekeleza sheria hiyo ni kosa kisheria;

Na kwa kuwa, kutokutekeleza sheria hiyo kunasababisha uendeshaji wa shughuli za *DART* kukwama na hivyo kuathiri mipango ya uboreshaji wa usafiri katika Jiji la Dar es Salaam na ucheleweshwaji wa mabasi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itatue mgogoro huo haraka ili kuiwezesha *DART* kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya udumavu nchini:

Kwa kuwa, kwenye baadhi ya mikoa ya Tanzania bado kuna kiwango kikubwa cha udumavu;

Na kwa kuwa, hali ya udumavu inahatarisha ustawi wa taifa hapo baadaye;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze kampeni na kuanzisha programu mahsusi kwa ajili ya kuhakikisha kuwa udumavu unatokomezwa nchini na kupima hatua za utekelezaji wa kampeni hiyo kwa kipindi kitakachofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri kutumia mapato ya ndani kwa ajili ya utengenezaji wa Barabara: -

Kwa kuwa, mvua zinazoendelea kunyesha nchini zinaendelea kuharibu miundombinu ya barabara;

Na kwa kuwa, kuharibika kwa barabara nyingi kunasababisha usumbufu kwa abiria na kwa wananchi kusafirisha bidhaa mbalimbali kwenda kwenye masoko;

Na kwa kuwa, *TARURA* ina bajeti isiyotosheleza kuharakisha utekelezaji wa urejeshaji wa miundombinu ya barabara iliyoharibika na mvua mbalimbali na Kimbunga Hidaya kwa wakati;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Halmashauri za Wilaya nchini ambazo zinatakiwa kuchangia 10% kwa kutumia mapato yao ya ndani wasaidiane na *TARURA* ili kurejesha barabara zilizoharibiwa na mvua nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kutenga na kupeleka fedha *TARURA* kama zilivyopitishwa na Bunge:-

Kwa kuwa, upelekaji wa fedha kwenda *TARURA* unasuasua hata kama fedha hizo zinatengwa;

Na kwa kuwa, kutokupeleka fedha hizo kwa wakati kunaendelea kuifanya miundombinu ya barabara kuendelea kuharibika zaidi;

Na kwa kuwa, hali hiyo inaendelea kuleta usumbufu kwa wananchi nchini na kurudisha nyuma ustawi wa wananchi hao;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba fedha zote zinazotengwa kwenye bajeti ya *TARURA* ziende kama zilivyotengwa na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Mfumo wa Manunuzi wa *NeST*:

Kwa kuwa, watendaji wengi katika Halmashauri nchini bado hawana uelewa wa ndani kuhusiana na matumizi ya Mfumo wa Manunuzi wa *NeST;*

Na kwa kuwa, kuwepo kwa uelewa mdogo wa watendaji katika halmashauri nchini kuhusiana na matumizi ya mfumo wa manunuzi wa *NeST* kunasababisha miradi mingi kukwama ama kuchelewa, ama kutekelezwa kwa kiwango cha chini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itafute njia bora ya kuhakikisha kwamba tatizo la mfumo wa manunuzi linatatuliwa ili shughuli za manunuzi zifanyike kwa wakati na kwa ufanisi unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo:-

Kwa kuwa, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo hakina hosteli za kutosha kwa ajili ya wanafunzi wa chuo na hivyo kufanya wanafunzi wengi kuishi kwenye nyumba za watu binafsi;

Na kwa kuwa, wanafunzi hao kuishi kwenye nyumba za watu ambazo usalama wake ni mdogo kunasababisha wanafunzi hao kutokuwa salama, hali inayotishia kushuka kwa uwezo wao wa kujifunza na hivyo kupunguza kiwango cha ufaulu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iharakishe mchakato wa ujenzi wa hosteli kwa mfumo *PPP* ili kujenga hosteli zitakazosaidia kuwafanya wanafunzi wote kuishi ndani ya chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa wimbi kubwa la watumishi wa Afya na Elimu kuhama maeneo ya vijijini hasa yenye mazingira magumu:-

Kwa kuwa, kumekuwa na wimbi kubwa la watumishi katika kada za afya na elimu kuhama maeneo ya halmashauri yenye mazingira magumu;

Na kwa kuwa, kuhama kwa watumishi hao kunaacha ombwe la upungufu wa watumishi katika Sekta za Afya na Elimu katika maeneo yenye mazingira magumu, hasa ya vijijini;

Na kwa kuwa, upungufu huo unazidisha ugumu na ustawi hafifu wa maisha na huduma kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iboreshe mazingira na kutoa kipaumbele katika uboreshaji wa huduma kwa watumishi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri kuchangia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa:-

Kwa kuwa, chanzo kimojawapo cha bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ni michango kutoka halmashauri zote nchini;

Na kwa kuwa, halmashauri nyingi hazitekelezi jukumu hilo la kuchangia Bodi ya Serikali za Mitaa;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa michango kutoka Halmashauri kinasababisha Bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake kama ipasavyo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mkakati wa kuzilazimisha halmashauri kuchangia na kulipa malimbikizo ya madeni ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilishaji wa maboma ya afya, elimu na vyoo katika halmashauri nchini:-

Kwa kuwa, kuna maboma mengi yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na kwa ajili ya huduma za afya na elimu na vyoo yamebaki bila kukamilishwa kwa sababu ya halmashauri kukosa fedha;

Na kwa kuwa, kuendelea kuwepo kwa maboma hayo kunanyima utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, kunasababisha maboma hayo kuchakaa hata kabla ya kuisha;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itafute fedha za dharura kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Kamati ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Naibu Mawaziri Mheshimiwa

Dkt. Festo Dugange pamoja na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Adolf Ndunguru kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, kwa ushirikiano walionipatia wakati wa kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninatambua na kuthamini michango yao adhimu na kujitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu. Kwa maslahi ya muda, ninaomba orodha yao iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee pia ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake, pamoja na Sekretarieti ya Kamati hii, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2024 HADI JANUARI, 2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa** Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, na kwa sababu hiyo taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: -

i) **Sehemu ya Kwanza**, inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumiwa na Kamati kutekeleza majukumu yake pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

ii) **Sehemu ya Pili,** inafafanua kuhusu shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji, mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

iii) **Sehemu ya Tatu,** inatoa maoni ya jumla na mapendekezo, ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi; na

iv) **Sehemu ya Nne,** ni hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

**1.3 Msingi wa shughuli za Kamati na Njia zilizotumika kuteleleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Kanuni ya 142(a) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, na kwa hiyo Kamati ilitumia njia kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara pamoja na Taasisi inazozisimamia;

(ii) Kusoma na kuchambua taarifa za utekelezaji wa majukumu zilizowasilishwa na Wizara na Taasisi zilizo chini yake; na

(iii) Kuandaa na kutoa maoni na ushauri kuhusu yatokanayo na taarifa za Wizara na Taasisi inazozisimamia.

**1.4 Madhumuni ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Madhumuni ya Taarifa hii ni kubainisha mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Lengo ni kuonesha mambo yanayohitaji kuboreshwa ili Bunge liyajadili kwa kuzingatia majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba.

## 1.5 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge kwa niaba ya wananchi, lina jukumu kubwa la kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba inaweka utaratibu na msingi wa uwepo wa Kamati za Bunge na utekelezaji wa majukumu ya Kamati ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kanuni ya 137 kwa pamoja na Nyongeza ya Nane zinaweka msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 5(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake. Aidha, Nyongeza ya Nane, 7(1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa ni pamoja na: -

a) Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

**Mheshimiwa Spika,** katika Kipindi cha Mwaka 2024/2025, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni ya 137 na Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza ni pamoja na:-

(i) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia; na

(iv) Kushiriki Semina za mafunzo.

### 2.1 Kufanya ziara za ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipata wasaa wa kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Taasisi inazozisimamia. Aidha, Kamati ilifanikiwa kufanya ziara katika mikoa kumi na tano (15) ambayo ni Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Njombe, Songwe, Rukwa, Katavi, Tabora, Singida na Dodoma na kukagua jumla ya miradi 81.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi 14 Mkoa wa Dar es Salaam, miradi minne (4) Mkoa wa Singida, miradi 10 Mkoa wa Morogoro, miradi mitatu (3) Mkoa wa Dodoma, miradi 12 Mkoa wa Iringa, miradi tisa (9) Mkoa wa Njombe, miradi mitatu (3) Mkoa wa Pwani, miradi sita(6) Mkoa wa Rukwa, miradi mitano (5) Mkoa wa Katavi, miradi miwili (2) Mkoa wa Songwe, miradi mitatu (3) Mkoa wa Manyara, miradi minne (4) Mkoa wa Arisha, miradi minne (4) Mkoa wa Kilimanjaro, na miradi miwili (2) Mkoa wa Tanga. Oradha ya miradi iliyotembelewa na Kamati kwa kipindi cha Februai, 2024 hadi Januari, 2025 ni kama inavyoonekana hapa chini:-

(i) Mradi wa Kituo cha Kisasa cha Mabasi Mwenge – Kindoni, Dar es Salaam.

(ii) Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni (KMC) – Dar es Salaam;

(iii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Jamirex (Msikitini) KM 0.2 na Kimbiji Km. 0.2 kwa kiwango cha zege Pamoja na Barabara ya Zahanati (Mwaifuge) Km. 0.2 na Nakiete 0.2 Km kwa kiwango cha lami – Kinondoni, Dar es Salaam;

(iv) Mradi wa Ujenzi wa Vyumba Kumi vya Madarasa katika Shule ya Sekondari ya Songolo Mnyonge – Kinondoni, Dar es Salaam;

(v) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Kibada – Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam;

(vi) Mradi wa Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa Bamba katika Halmashauri ya Wilya ya Kigamboni, Dar es Salaam;

(vii) Mradi wa Ukarabati na Ujenzi wa Soko la Kariakoo, Dar es Salaam;

(viii) Mradi wa ujenzi wa miundombinu na uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam;

(ix) Mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi - Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Singida;

(x) Mradi wa Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondali ya Wasichana ya Mkoa wa Morogoro - Bwakila Chini, Morogoro;

(xi) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Homboza, Morogoro;

(xii) Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Shule ya Sekondari ya Bunduki katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Morogoro;

(xiii) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Utumishi wa Walimu, Njedengwa, Dodoma;

(xiv) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mninga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Iringa;

(xv) Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Ihegela katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Iringa;

(xvi) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Huduma za Dharula katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Makambako, Njombe;

(xvii) Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Ngamanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Njombe;

(xviii) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Wanging'ombe, Njombe;

(xix) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Wanging'ombe katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Njombe;

(xx) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Muungano – Kifanya katika Halmashauri ya Mji Njombe;

(xxi) Mradi wa Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Mji Njombe (KIBENA);

(xxii) Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Mdasi – Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Njiombe;

(xxiii) Mradi wa uboreshaji wa Hospitali ya Mji Mafinga, Iringa;

(xxiv) Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Rungemba katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Iringa;

(xxv) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mtwango katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Njombe;

(xxvi) Ujenzi wa Barabara ya Nyombo - Welela (km 13) kwa kiwango cha changarawekwab katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Njombe;

(xxvii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Itipingi – Kichiwa (kilometa 8), Kidegembye – Msima (kilometa 5) na Msima – Matiganjora (kilometa 5.6) kwa kiwango cha changarawe katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Njombe;

(xxviii) Mradi wa Uondoaji Vikwazo katika Barabara ya Ilula – Ilambo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Iringa;

(xxix) Mradi Ujenzi wa Barabara ya Makondeko – Ndolezi (Km. 1.7) kiwango cha Lami katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Iringa;

(xxx) Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mwamkoa – Mbagala (Km 0.50), Mdeka-Rift Valley (Km. 0,37) na Msangarufu (Km. 0.19) kwa Kiwango cha Lami katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Iringa;

(xxxi) Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mji wa Igowele Km. 1 kwa kiwango cha Lami katika Halmashauri ya Wialaya ya Mufindi, Iringa;

(xxxii) Mradi wa Ufunguzi wa Barabara za Maduma – Iyayi (Km. 13.90) na Ihowanza – Idope (Km. 6.80) Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Iringa;

(xxxiii) Mradi wa Ujenzi Shule Mpya ya Bweni ya Wasichaana ya Mkoa wa Iringa;

(xxxiv) Mradi wa Ujezi wa Kituo cha Afya Nyalumbu katika Hamashauri ya Wilaya ya Kilolo, Iringa;

(xxxv) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Ilula katika Hamashauri ya Wilaya ya Kilolo, Iringa;

(xxxvi) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya kuelekea Ofisi za Halmashauri ya Kibaha Vijijini yenye urefu wa 600M kwa kiwango cha Lami katika Halmashauri ya Kibaha Vijijini, Pwani;

(xxxvii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Visiga – Zegereni (12.5KM) kwa kiwango cha Lami katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Pwani;

(xxxviii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Picha ya Ndege – Bokotimiza Km. 1.25KM kwa kiwango cha Lami katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Pwani;

(xxxix) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Biashara na Usafirihaji cha Afrika Mashariki katika Ubungo, Dar es Salaam;

(xl) Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Afya Mpui katika halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Rukwa;

(xli) Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga – ISOFU, Rukwa;

(xlii) Ujenzi wa Shule Mpya ya Mkondo Mmoja (Shule ya Msingi Kituku) katika halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Rukwa;

(xliii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara mpya ya Chala – Ifundwa kwa kiwango cha changarawe katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Rukwa;

(xliv) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nkasi, Rukwa;

(xlv) Mradi wa Ujenzi wa madaraja matatu barabara ya Laela – Kavifuti – Miangalua katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Rukwa;

(xlvi) Mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Barabara katika Barabara ya Stand kwa kiwango cha lami (double surface dressing) 1.275km katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Rukwa;

(xlvii) Mradi wa Utanuzi wa Barabara za Mpanda Manispaa kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Katavi;

(xlviii) Ujenzi wa Shule Mpya ya Wavulana ya Katavi kupitia Mradi wa Sequip;

(xlix) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Ifinsi – Bugwe (Km21) kwa kiwango cha Changarawe;

(l) Mradi wa Ujenzi Wa Daraja La Kigamboni *(Arch Bridge)* wenye namba ya Mkataba AE.092/WB-RISE.P164920/378969/2023/2024/W/01-LOT1 katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Katavi;

(li) Mradi wa Ujenzi wa jengo la Ghorofa sita katika hospitali ya Mbagala Rangi Tatu katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam;

(lii) Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mbagala Zakheem katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam;

(liii) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Mangaya katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam;

(liv) Mradi wa Ujenzi wa Mfereji wa Serengeti na Bwawa kuhifadhia maji ya Mvua kwa muda katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam;

(lv) Mradi wa Ujenzi wa Bweni na Bwalo katika Shule ya Sekondari Kibasila katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam;

(lvi) Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Samia katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Tabora;

(lvii) Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Igunguli Katao katika halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Tabora;

(lviii) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Shule ya Sekondari Ntahondi katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Tabora;

(lix) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Msingi mpya ya Mbugani yenye mikondo miwili katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora;

(lx) Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya Kidatu yenye mikondo miwili Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Tabora;

(lxi) Mradi wa Ujenzi wa Majengo Mapya Shule ya Msingi Mabatini katika Halmashauri ya Wilaya ya Tabora;

(lxii) Mradi wa Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 3 ya vyoo Shue ya Msingi Kalunde Halmashauri ya Wilaya ya Tabora;

(lxiii) Mradi wa Ujenzi wa Madarasa 3 na matundu 3 ya vyoo Shule ya Msingi Kizigo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tabora;

(lxiv) Mradi wa Ujenzi wa madarasa 2 na matundu 3 ya vyoo Shule ya Msingi Chemchem katika Halmshauri ya Manispaa ya Tabora;

(lxv) Mradi wa Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari ya Kakola katika Halmashauri ya Wilaya ya Tabora;

(lxvi) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Solya katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Singida;

(lxvii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Ikungi – Ihanja Mita 750 kwa kiwango cha Lami nyepesi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Singda;

(lxviii) Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Minyughe katika Halmshauri ya Wilaya ya Ikungi, Singida;

(lxix) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mugabe 0.6 Km kwa kiwango cha lami (DSD) (**Mradi Namba 4170 (10/011/2023/2024/W/17**) – Manyara;

(lxx) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Nakwa 0.65 Km kwa kiwango cha lami (DSD)**Mradi Namba 4170 (S10/011/2023/2024/W/21) – Manyara;**

(lxxi) Mradi wa Ujenzi wa shule mpya ya Mkoa ya Wasichana wa Manyara (Babati) **Mradi Namba 4390 – Manyara;**

(lxxii) Ujenzi wa jengo la OPD, Ujenzi wa jengo la X-ray, Ujenzi wa Jengo la maabara, na ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha; **Mradi Namba 6212 – Arusha;**

(lxxiii) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la OPD, Ujenzi wa kichomea taka, Ujenzi wa Maabara, Ukarabati wa majengo ya Hospitali katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Meru, **Mradi Namba 6212 – Arusha;**

(lxxiv) Mradi wa Kuboresha barabara ya RHM-Oltrumet Hospital kwa kiwango cha lami Ngumu mita 500, **Mradi Namba 4170 (S10/001/2023/2024/W/43) – Arusha**;

(lxxv) Mradi wa Ujenzi wa barabara ya Longido Sekondari - Kanisa la KKKT kwa kiwango cha lami **Mradi Namba 4170 (S10/001/2023/2024/W/69) – Arusha;**

(lxxvi) Mradi wa Marekebisho ya sehemu korofi katika Barabara ya Ndesingawa na Mahakama Abumalya hadi mzunguko wa sabasaba katika Manispaa ya Moshi **Mradi Namba 4170 S10/009/2023/2024/W/09) – Kilimanjaro;**

(lxxvii) Mradi wa Ujenzi wa jengo la Utawala, Mionzi, jengo la kufulia na jengo la dawa katika Hospitali ya Wilaya – Moshi (**Mradi Namba 5401) – Kilimanjaro;**

(lxxviii) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya sekondari Saasisha (Halmashauri ya Wilaya ya Hai) **Mradi Namba 4390 – Kilimanjaro;**

(lxxix) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Makoye – Mferejini (Halmashauri ya Wilaya ya Hai **Mradi Namba 4170 (AE/092/2022/2023/KLM/W/54) – Kilimanjaro;**

(lxxx) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Viongozi (Rest House) (**Mradi Namba 6212) – Tanga;**

(lxxxi) Mradi wa Ujenzi wa miundombinu shule mpya ya Sekondari Kiomoni (**Mradi Namba 4390) – Tanga;**

**Mheshimiwa Spika,** miradi iliyotajwa baadhi yake ilitolewa taarifa wakati wa vikao vya Bunge la Bajeti. Aidha, miradi iliyosalia ilitembelewa na kukaguliwa wakati wa vikao vingine vya Kamati vilivyofanyika baada ya Bunge la Bajeti.

## 2.2 Uchambuzi wa Miswada na Maazimio

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 Kamati haikushughulikia muswada wowote wa Sheria wala maazimio ya kuridhiwa na Bunge yanayotokana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

## 2.3 Kushughulikia Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, mara baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilipata wasaa wa kupokea, kuchambua, kuhoji na kujadili taarifa za utekelezaji wa maoni ya Kamati na utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na kuchambua, kuhoji, kujadili na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara inayoisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya kina ya Uchambuzi wa Bajeti inayosimamiwa na Kamati pamoja na maoni na ushauri wa Kamati viliwasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kwa maoni yale ambayo hayakutekelezwa, Kamati itaendelea kuyasisitiza maoni hayo katika Taarifa hii.


### 2.3.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara inayosimamiwa na Kamati pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2024)

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2024), napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa hali ya utolewaji wa fedha kwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa si wa kuridhisha, hasa kwenye fedha za miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake ilitengewa kiasi cha **Shilingi 1,109,934,983,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2024, jumla ya **Shilingi 429,457,065,818.22** kilikuwa kimepokelewa, sawa na **asilimia 38.7** tu ya fedha zilizotengwa na zilizoidhinishwa. Aidha, kiasi kilichopaswa kuwa kimekwishakutolewa hadi Disemba, 2024 ni **Shilingi 554,967,491,500,** kiasi ambacho hakijapelekwa ni **Shilingi 125,510,425,682.** *(Tazama mchanganuo kielelezo Na. 1).*

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utolewaji wa fedha kwa Wizara hii si ya kuridhisha kwani Kamati imebaini fedha zilizotolewa kwa Wizara ni asilimia 38 tu badala ya walau asilimia 50 iliyotarajiwa kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2025). **Kamati inaishauri Serikali kupelea fedha kwenye Wizara hii ili iweze kuwahudumia wananchi vile inavyopaswa.**

*Kielelezo Na. 1 – Ulinganisho wa utolewaji wa Bajeti kwa OR-TAMISEMI kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2024*




*Chanzo: Taarifa za Wizara na Usanifu wa Kamati*

## 2.4 Utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulizingatia Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais TAMISEMI wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/2025, Sheria ya Bajeti Sura 439, Sera za Kisekta, Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo yaliyomo katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Agenda Afrika 2063.

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti, 2024; Oktoba 2024; na Januari, 2025 Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa mbalimbali za Utendaji wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na taasisi zilizo chini yake. Taarifa zilizowasilishwa na kuchambuliwa Kamati ni kama ifuatavyo:-

(i) Taarifa ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikail za Mitaa kuhusu utendaji wa Wizara hiyo;

(ii) Taarifa ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utendaji wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA);*

(iii) Taarifa ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utendaji wa Taasisi ya Wakala wa Mabasi yaendayo Kasi Dar es Salaam *(The Dar es Salaam Rapid Transport);*

(iv) Taarifa ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utendaji wa Shirika la Masoko la Kariakoo;

(v) Taarifa ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utendaji wa Tume ya Walimu;

(vi) Taarifa ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utendaji wa Shirika la Maendeleo la Jiji la Dar es Salaam *(Dar es Salaam Development Cooperation - DDC);* na

(vii) Taarifa ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utendaji wa Shirika la Elimu Kibaha.

**2.4.1 Shughuli zilizotekelezwa na Wizara na taasisi zilizo chini yake na yaliyobainika wakati wa kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli hizo**

**2.4.1.1 Makao Makuu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, na kujadili taarifa za utendaji za Wizara hiyo kwa upande wa Makao Makuu kwa kuzingatia vipaumbele tisa vilivyowekwa na Wizara hiyo. Aidha, Taarifa za Utendaji za Wizara hiyo zilijadiliwa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya Serikali kwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Disemba, 2024 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza shughuli zake kwa ufanisi ambapo kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Wizara imeimarisha rasilimaliwatu kwa kujaza nafasi 530 kati ya 1,210 za Wakuu wa Idara na Vitengo.

Aidha Wizara imefanya uhamisho mbalimbali wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mkakati wa kuweka msawazo stahiki kulingana na mahitaji ya watumishi katika Mamkala za Serikali za Mitaa. Wizara imefanikiwa katika uratibu wa masuala ya utekelezaji wa bajeti katika halmashauri ambapo, umefanyika uchambuzi wa bajeti ya

mwaka 2024/2025 kwa Halmashauri 184 na kuingiza katika matumizi ya mifumo mbalimbali kama vile TAUSI, MUSE na FFARS.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanikiwa kuratibu shughuli za O&OD *(Opportunities and Obstacles to Development)* ikiwemo kuwajengea uwezo waratibu wa Mikoa 26 na wataalamu wa Halmashauri 596 wa mfumo wa O&OD juu ya kuainisha vipaumbele vinavyoibuliwa na jamii. Wizara imefanikiwa kuratibu biashara na uwekezaji kwa Wamachinga nchini. Hadi Disemba, 2024 kazi za utambuzi na ukusanyaji wa takwimu zimefanyika kwa mafanikio. Aidha, uratibu wa masuala ya Wamachinga umefanyika kwa mafanikio kufuatilia ujenzi wa ofisi 26 za wafanyabiashara ndogondogo ambazo zinajengwa katika kila Mkoa. Wizara inaendelea na maandalizi ya uimarishaji wa ukusanyaji wa kodi ya majengo *(Property Tax)* kwa kutumia mfumo wa TAUSI ambapo Halmashauri 47 zimeshafikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na kusimamia utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake Vijana na wenye Ulemavu ambapo uratibu wa masuala ya huduma ndogo za fedha umefanyika na jumla ya vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha 4,073 vimetambuliwa na kusajiliwa na hivyo kuwezesha kufikia vikundi 56,645.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti za Mikoa yote 26 nchini. Wizara imefanikiwa kuratibu ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri, katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, 2024 ambapo jumla ya shilingi bilioni 43.48 zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo hayo, sawa na asilimia 77 ya shilingi bilioni 56.16 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo 78 ya utawala.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanikiwa kuratibu shughuli za mipango miji na vijiji ambapo upembuzi yakinifu *(feasibility studies)* kwenye masoko 8 ya mradi wa SASA *(Green and Smart Cities)* umefanyika.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kusimika mfumo wa "*Online Geo Data Base*" kwenye Halmashauri 10 ambazo ni Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke, Ubungo, Jiji la Mbeya, Mwanza, Ilemela, Tanga, Arusha na Dodoma kupitia mradi wa SASA. Mageuzi haya ni muhimu katika kufikia ndoto ya kuwa *GIS Metro Hub* ambayo itaingiza taarifa za Kijiografia ikiwemo za majengo, na vibali vya ujenzi. Aidha, mradi wa TACTIC unashirikiana na mradi wa SASA katika kuwezesha mfumo huo kwenye Halmashauri 47 za mradi wa TACTIC, Wizara imefanikiwa kusimamia uendelezaji na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya Nchi na kukamilisha Sheria ya Uendeshaji wa Makao Makuu. Aidha, Ofisi inashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau wengine kukamilisha ujenzi wa Mnara wa Mashujaa, Mnara wa Makao Makuu, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano na maboresho mengine kwenye upangaji wa Mji wa Serikali - Mtumba.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanikiwa kusimamia ujenzi wa shule mpya za kata 234 zenye thamani ya shilingi 134,180,899,303.00, shule mpya za sekondari za amali 103 zenye thamani ya shilingi 88,849,305,125.00, shule saba za bweni za wavulana zenye thamani ya shilingi 28,700,000,000.00, awamu ya pili ya ujenzi wa shule 16 za sekondari za bweni za wasichana zenye thamani ya shilingi 17,600,000,000 na ujenzi wa mabweni 526 yenye thamani ya shilingi 67,988,000,000, madarasa 596 yenye thamani ya shilingi 14,600,000,000 na matundu ya vyoo 3,186 yenye thamani ya shilingi 2,491,800,000, nyumba za walimu 229 zenye thamani ya shilingi 22,741,000,000 na

umaliziaji mabwalo katika shule za bweni za wasichana za mikoa yenye thamani ya shilingi 5,600,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imetekeleza jukumu lake la uratibu na usimamizi wa mafunzo ya usimamizi wa shughuli za ujenzi na mfumo wa NeST kwa maafisa manunuzi na timu za usimamizi wa miradi, mafunzo ya utekelezaji wa mpango wa shule salama kwa wenyeviti wa bodi za shule 1001, maafisa maendeleo ya jamii kata 500, maafisa usatawi wa jamii mikoa 26, maafisa maendeleo ya jamii mikoa 26, waratibu wa mpango wa shule salama 210 na waratibu wa mradi wa SEQUIP katika kanda 10.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kipindi cha mwaka 2024 imetekeleza jukumu la **uratibu na usimamizi wa shughuli za afya ambapo** uratibu, ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Msingi katika mikoa 10 ya kipaumbele kwenye Mikoa ya Kagera, Geita, Mbeya, Njombe, Kigoma, Tabora, Tanga, Lindi, Songwe na Pwani umefanyika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kufanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha kuridhisha katika kipindi cha mwaka 2024 Kamati imebaini changamoto kadhaa zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Wizara imepata changamoto ya ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na majukumu yake. Aidha, bajeti kubwa kutoka Wizara za Kisekta, kutengwa Wizarani badala ya kwenye Halmashauri na kusababisha miradi kuchelewa kutekelezwa kutokana na kuhitaji uhamisho wa fedha.


**Kamati inashauri Serikali kuangalia namna nzuri ya upelekaji wa bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwezesha utekelezaji wa miradi na shughuli nyingine za Mamlaka hizo kufanyika kwa wakati**.

### 2.4.1.2 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA)

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA)* ambaye ana jukumu la kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini na mijini ana mtandao wa barabara za Wilaya wenye jumla ya kilometa 144,429.77.

Kati ya barabara hizo, kilometa 3,337.66 sawa asilimia 2.31 ni barabara za lami, kilometa 42,059.17 sawa na asilimia 29.12% ni barabara za Changarawe na kilometa 99,032.93 sawa na asilimia 68.57 ni barabara za udongo. *(Tazama kielelezo Namba 2)*.

Kielelezo Namba 2: Mgawanyo wa Barabara zinazosimamiwa na TARURA




*Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** kielelezo cha hapo juu kinaonesha kuwa TARURA ina Barabara nyingi za vumbi ambazo uhai wake ni mdogo kutokana na ubora kuwa wa chini. Hivyo kwa sura

hiyo Kamati inaona kuwa TARURA ana kazi kubwa ambayo inahitaji fedha nyingi ili kuongeza walau kiwango cha Barabara za changarawe na kupunguza uwepo mkubwa wa Barabara za vumbi.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi wa taarifa ya *TARURA* kuhusu utekelezaji wa majukumu yake ya kuboresha miundombinu ya Barabara nchini Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

**a) Barabara zilizoharibiwa na mvua za El-Nino kutofanyiwa matengenezo**

**Mheshimiwa Spika,** barabara zilizoharibiwa na mvua za El Nino bado hazijafanyiwa matengenezo, wakati huo huo mvua zinazoendelea sasa na zinazotarajiwa kunyesha kipindi cha Februari – Mei, 2025 zitaongeza uharibifu wa miundombinu mbalimbali ya Barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya *TARURA* inaonesha kuwa tathmini iliyofanyika juu ya uharibifu wa miundombinu uliosababishwa na mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya ilihitaji bilioni **Shilingi bilioni 883** ili kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mvua za El Nino.


Kamati imebaini kuwa Serikali imetenga na kutoa kiasi cha **Shilingi Bilioni 83** kwa ajili ya urejeshaji wa miundombinu hiyo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga na kutoa fehda hiyo kwa ajili ya urejeshaji wa miundombinu ya Barabara inayosimamiwa na TARURA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa TARURA imetekeleza jukumu lake la urejeshaji wa miundombinu iliyoharikiwa na mvua za El Nino pamoja na Kimbunga Hidaya kwa asilimia 28 tu, hivyo asilimia 72 bado hazijatengenezwa kutokana na Serikali kutokutoa fedha zinazotosha kwa ajili ya ukarabati huo.

**Kamati inashauri Serikali kutoa fedha hizo za dharura kwa wakati ili kuondoa uwezekano wa Barabara hizo kuharibiwa zaidi na hivyo kuweza kuisababishia Serikali kutumia fedha nyingi zaidi.**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lilipitisha bajeti ya Shilingi 886,303,266,000.00 katika bajeti ya *TARURA* kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake kwa mwaka 2024/2025. Matajio hadi mwezi Disemba, 2025 *TARURA* iwe imekwishakupelekewa kiasi cha **shilingi 443,151,633,000.00.** Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Disemba, 2024 *TARURA* ilipokea kiasi cha **shilingi 92,497,494,532.18** sawa na **asilimia 20** tu ya matarajio. Kamati inasikitika kwa uwasilishaji mdogo wa fedha kwa *TARURA* ambao haukufikia hata nusu ya matarajio kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024; kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Namba 3.**

Kielelezo Namba 3: Upelekaji wa bajeti kwa TARURA kutoka Hazina.




*Chanzo: Taarifa za Wizara na Usanifu wa Kamati*

### 2.4.1.3 Wakala wa Mabasi yaendayo Kasi Dar es Salaam (DART)

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilipokea taarifa mbalimbali za utendaji wa Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka *(DART)* ili kuweza kung'amua ufanisi wake katika kutatua changamoto ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Katika

uchambuzi wa taarifa hizo Kamati imebaini kuwa Wakala imeendelea kufanya vyema kwa kiwango chake kutoa huduma kwa wananchi, na vilevile kwa kuchangia fedha za mapato ya ndani kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo kwa miaka takriban minne Wakala ameweza kuchangia Kiasi cha shilingi 723,748,525.25. Hii inaonesha uendelevu *(sustainability)* wa Wakala.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo Kamati imebaini kuwa *DART* inakutana na changamoto ya kutokupelekewa fedha za makusanyo na *UDART* na hivyo kupelekea kuwepo kwa mgogoro wa kimalipo kati ya DART na UDART. Kamati inatambua kuwa Bunge lilipitisha Sheria ya Fedha mwezi Juni, 2024 ili kuipa uwezo *DART* kutekeleza shughuli zake kwa kuitekeleza bajeti kisheria. Katika Sheria hiyo ya Bajeti Bunge lilipitisha sehemu ya mapato ya *DART* kuwa ni makusanyo yanayotokana na nauli zinazokusanywa na *UDART*. Katika mkataba wa uendeshaji wa mradi wa mabasi ya mwendo kasi ulioingiwa kati ya *DART* na *UDART* walikubaliana kuwa UDART atakusanya nauli na kutoa gawio kwa DART. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kuna changamoto ya utekelezaji wa mkataba kwa *UDART* kutokupeleka gawio kwa DART kwa mujibu wa sheria kama sehemu ya makusanyo. Hali hii inaathiri utekelezaji wa bajeti kwa upande wa *DART*. **Kamati inaishauri Serikali kuzikutanisha pande hizi mbili na kukaa kwa pamoja ili kutatua mgogoro huo ili kutekeleza Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2024 ipasavyo.**

### 2.4.1.4 Shirika la Maendeleo la Jiji la Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Uchumi na Maendeleo la Jiji la Dar es Salaam (DDC) lilianzishwa Mwaka 1973 chini ya Sheria ya Mashirika ya Wilaya, Sura Namba 382 Marejeo ya Mwaka 2002, *(The District Development Corporation Act [CAP 382 R.E 2002].* Shirika lilianzishwa kupitia Oda ya Uanzishaji ya Mashirika ya Wilaya kwa Tangazo la Serikali Na.144 la mwaka 1974 *(The District Corporations (Establishment) Order, GN No.144 of 1974.)*. Shirika la DDC lilianzishwa kama

kitegauchumi cha Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kutoa burudani. Shirika hili lipo chini ya Jiji la Dar es Salaam. Shirika lilipewa majukumu ya jumla mbali mbali ikiwemo: -

(i) Kufanya uwekezaji wa kibiashara kwa kujenga majengo ya biashara kama masoko, mahoteli, migahawa, baa na kumbi za burudani;

(ii) Kufanya shughuli za uzalishaji ikiwemo uzalishaji wa viwanda na mashamba;

(iii) Kufanya biashara mbalimbali za jumla, rejareja na uwakala;

(iv) Kusimamia na kutoa huduma za burudani jijini Dar es salaam; na

(v) Kufanya shughuli yeyote ya kiuchumi na yenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa, *DDC* ina majengo mengi na vitega uchumi vingi ambayo huenda Serikali haivitilii maanani, kama vile majengo ya *DDC Keko*, *DDC Magomeni* na *DDC* Kariakoo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Shirika linatekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la biashara kwa ubia wa Serikali na Sekta Binafsi *(PPP)* lenye urefu wa ghorofa sita. Kamati inapongeza juhudi hizi kwani zina lengo la kuongeza vyanzo vya mapato kwa shirika hilo. Kamati inashauri Shirika la *DDC* kuendeleza miradi yake kwa kutumia PPP ili kuendeleza maeneo yao kwa ajili kuongeza mapato ya shirika hilo. **Hata hivyo inaendelea kuishauri Serikali kuwa karibu na kuongeza usimamizi kwa Shirika hilo ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

### 2.4.1.5 Shirika la Masoko la Kariakoo

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Masoko ya Kariakoo linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Sura 132 na kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (5) (*The Kariakoo Market Corporation Strategic Plan 2021/22 - 2025/26)* uliohuishwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mabadiliko yaliyofanyika yamezingatia uboreshaji wa utendaji kazi, mazingira ya kufanya biashara kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayotokea duniani, mazingira ya utoaji huduma, usimamizi thabiti wa rasilimali fedha kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu pamoja na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika makusanyo na matumizi ya fedha. Aidha, uhuishaji wa Mpango Mkakati umezingatia uwekezaji mkubwa uliyofanywa na Serikali katika ujenzi na ukarabati wa soko la Kariakoo pamoja na uwekezaji unaopangwa kutekelezwa katika maeneo mengine ya Shirika ya Mbezi Beach Makonde na Tabata Bima kuanzia mwaka 2024/25 ambapo kwa sasa maandalizi yapo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 Shirika liliidhinishiwa bajeti ya **shilingi bilioni 13,789,936,800.00.** Kati ya fedha hizo **shilingi 11,948,802,000.00** ni kutoka mapato ya ndani na **shilingi 1,841,134,800.00** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu**.** Kati ya fedha za ruzuku **shilingi 1,372,911,000.0** ni mishahara na **shilingi milioni 468,223,800.00** ni matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati kuhusu upokeaji wa fedha inaonesha kuwa hadi mwezi Disemba, 2024 Shirika lilipokea jumla ya Shilingi 738,899,430.23 sawa na asilimia **5.4** ya fedha zote za bajeti. Shilingi **419,642,059.64** ni Mishahara sawa na **asilimia 25.2** na **shilingi 208,318,485.67** ni matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** upelekaji huu wa fedha kwenda Shirika la Masoko ya Kariakoo hauoneshi hali nzuri kwa kuwa Shirika

haliwezi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. **Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha kama ilivyopangwa kwenye bajeti na kwa wakati ili kuliwezesha Shirika hili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na fedha kupelekwa kwa kiwango kidogo Shirika hili limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kiwango inachostahili kulingana na upatikanaji wa bajeti. Kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa Soko la Kariakoo Kamati ilibaini kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2024 limefanikiwa kuandaa mpangilio bora wa maeneo ya biashara katika soko linalokarabatiwa na linalojengwa tofauti na hapo awali kwa kuzingatia aina ya biashara zinazofanana kuuzwa katika eneo moja *market segmentation.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa mradi huu ulitarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, mwaka 2023. Hata hivyo mradi huu haukuweza kukamilika kwa wakati kama ilivyokuwa imepangwa. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2024 utekelezaji wa mradi ulifikia **asilimia 93.5**. ambapo jumla ya shilingi 21,346,443,150.96 zimekwishakutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kufahamu sababu za kutokukamilika kwa mradi huo na kuelezwa kuwa mradi huu haukuweza kukamilika ilipofika tarehe 5 Oktoba, 2024 kama ilivyokuwa kwenye Mkataba. Sababu zilizoelezwa kwa Kamati ni kwamba kumekuwa na kazi muhimu zilizoongezeka ambazo hazikuwa kwenye mkataba pamoja na mabadiliko ya usanifu katika mradi. Pamoja na sababu hizo Kamati bado inashauri Mradi huu ukamilike kwa wakati ili uweze kutoa huduma kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Shirika limeanza kutekeleza mchakato wa kuwarejesha wafanyabiashara waliokuwepo kabla ya tukio la moto na kuwaingiza wafanyabiashara wapya. **Kamati imebaini kuwa zoezi hili**

**linafanyika kwa utulivu na umakini. Kamati inalipongeza Shirika kwa hatua hii.**

#### 2.4.1.6 Chuo cha Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Serikali za Mitaa kinatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano (FYDP III 2021/22 – 2025/26), Mpango Mkakati wa Chuo 2021/2022 - 2025/2026, Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs) pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Serikali za Mitaa kilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Chuo cha Serikali za Mitaa, Sura 396, lengo likiwa ni kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma bora zitakazowajengea wananchi uwezo wa kuimarisha utawala bora, kuondokana na umaskini na kuboresha maisha yao. Aidha, majukumu Makuu ya Chuo ni kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa Kitaalamu.

#### 2.4.1.7 Shughuli zilizotekelezwa na Chuo cha Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2024 Chuo cha Serikali za Mitaa kimefanikiwa kusajili jumla ya wanafunzi 6,591 katika kozi mbalimbali pamoja na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa kutumia Mfumo wa Ujifunzaji Kielekitroniki (MUKI,) kuendesha mafunzo kwa wenyeviti wa vijiji na vitongoji katika Halmashauri 91 za Tanzania bara, kuendesha zoezi la mitihani ya wanafunzi 6,591 katika ngazi zote, na kuendeleza watumishi katika fani mbalimbali ambapo jumla ya watumishi 34 wapo katika mafunzo ya muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa masomo 2023/2024 Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 6,575 kwa ngazi za kuanzia cheti hadi shahada katika fani za Utawala katika Serikali za

Mitaa, Uhasibu na Fedha katika Serikali za Mitaa, Maendeleo ya Jamii, Menejimenti ya Rasilimali watu, Ununuzi na Ugavi na Utunzaji wa Nyaraka na Kumbukumbu.

**Mheshimiwa Spika,** chuo kimefanikiwa kujenga madarasa matatu (3) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250 kila moja; kununua basi moja kujenga nyumba mbili za watumishi *(two in one);* kufanya ukarabati wa miundombinu ya Chuo katika mabweni ya wanafunzi na nyumba za watumishi.

**2.4.1.8 Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za Chuo cha Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati mwezi Agosti mwaka 2024 Kamati imebaini chuo kukabiliwa na changamoto kadhaa kama ifuatavyo: -


**(i) Upungufu wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake ya msingi, Chuo kinahitaji kuwa na watumishi 348. Kwa sasa Chuo kina watumishi 267 na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 81.

**(ii) Wingi wa Wanafunzi Usioendana na Uwepo wa Miundombinu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika chuo hicho ni kubwa ukilinganisha na uwezo wa chuo kuwapatia huduma mbaalimbali wanafunzi hao, hasa wa malazi *(hostel)*. Kamati imebaini kuwa idadi ya wanafunzi wanaokaa hosteli ni 1200 tu kati ya wanafunzi 6,591. Tafsiri yake ni kwamba asilimia 82 ya wanafunzi wanaodahiliwa katika chuo hiki wanaishi nje ya chuo ambako usalama wao ni mdogo.

**Kielelezo Namba 4:** *Uwiano wa wanafunzi wanaoishi katika Hosteli za Chuo na wanaoishi kwenye nyumba za watu binafsi*




### (iii) Usafiri

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri Kamati imebaini kuwa Barabara Kuu ya Dodoma – Morogoro (maeneo ya Ihumwa) kwenda chuoni hapo haina barabara nzuri ya kuwezesha usafiri rahisi, bora na salama. Barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 24 ni ya changarawe iliyo na mawimbi makubwa. Kwa kuwa chuo cha Hombolo ni chuo muhimu kwa ajili ya uimarishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Kamati inaona kuwa kukiboresha chuo hiki kunapaswa kuendana na uboreshaji wa miundombinu ya Barabara inayoelekea chuoni hapo. **Kamati inashauri Serikali kuanza ujenzi wa Barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kurahisisha kukifikia chuo hicho kwa urahisi na haraka zaidi**.

### (iv) Jengo la Utawala

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini pia kuwa Chuo cha Serikali za Mitaa hakina jengo la utawala linalokidhi mahitaji kwa sasa kutokana na jengo lililopo kutokutosheleza mahitaji.

### 2.4.1.9 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** Historia ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa inaanzia mwaka 1953 wakati wa utawala wa kikoloni ulipoanzisha Taasisi ya Fedha ya Serikali za Mitaa iliyojulikana kama *"The Local Councils Board",* chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa *(The Local Government Ordinance, Cap 333)* ya mwaka 1953 ambapo moja ya madhumuni yake ilikuwa ni kuzikopesha Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Wenyeji *(Native Authorities)*.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 1965, Sehemu ya XIII ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Cap 333) ya mwaka 1953 iliyounda Bodi ilifanyiwa marekebisho yaliyowezesha kuundwa kwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa *(Local Government Loans Board)*. Mabadiliko hayo yaliwezesha pia Halmashauri za Miji kupata huduma ya mikopo kama ilivyokuwa kwa Halmashauri za Wilaya.

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa yalilenga katika kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapata chanzo mbadala cha fedha ambacho kinatumika kutoa mikopo yenye masharti na riba nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia mwaka 1965 mpaka 1972, Bodi ya Mikopo ilikuwa ikitoa huduma kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa malengo mbalimbali. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri za Majiji ya **Mwanza na Mbeya,** Manispaa za **Moshi na Morogoro**. Majengo mengine ya Utawala yaliyojengwa kwa fedha zilizokopwa kutoka katika Bodi ya Mikopo Serikali za Mitaa ni katika Halmashauri za Wilaya za **Arumeru, Mbulu, Lushoto, Nzega na Rungwe**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa pamoja na Bodi hii kuwa na umuhimu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa lakini mamlaka hizo hazichangii bodi hii sehemu ya amana zao.

Aidha, **Kamati imebaini pia kuwa Halmashauri nyingi zinazokopa mikopo kwenye bodi hii hazirejeshi kwa wakati. Kamati inashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kurejesha mikopo wanayokopa kutoka bodi hii kwa wakati, ikiwa ni pamoja na kuchangia bodi hii sehemu ya amana zao ili kuiwezesha bodi kutekeleza majukumu yake ipasavyo.**

### 2.4.1.10 Shirika la Elimu Kibaha

**Mheshimiwa Spika,** malengo ya kuanzishwa kwa Shirika la Elimu Kibaha ni kutoa elimu ya mapambano dhidi ya maadui watatu wa maendeleo ambao ni **Ujinga, Umaskini** na **Maradhi**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Tangazo la Serikali Na. 2/1970 aya ya 4, Shirika linatekeleza majukumu ya kukuza maendeleo ya kilimo ikiwa ni pamoja na kutoa taaluma na mafunzo ya kilimo kwa vitendo na uzalishaji wa chakula, kutoa mafunzo na zana za mafunzo kwa wanafunzi wa Uganga, Uuguzi, wasaidizi wa afya vijijini kuhusu madawa ya kinga na tiba, afya ya jamii na usafi wa mazingira, kutoa Elimu kwa Jamii juu ya afya ya jamii na usafi wa mazingira, kutoa Elimu ya Sekondari kwa mujibu wa Sera, Sheria na kanuni zinazosimamia Elimu na kufanya kila linalowezekana au kuingia makubaliano ambayo kwa maoni ya Bodi, inaona inawezesha uendeshaji sahihi na wenye ufanisi na utendaji bora wa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa dhima ya kuanzisha shirika ni kuondoa umasikini, ujinga na maradhi, na kwa sababu matatizo hayo bado yapo, **Kamati inaona kuwa kuendelea kuwepo kwa Shirika hilo ni muhimu.**

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa taasisi zinazosimamiwa na Shirika la Elimu Kibaha ni Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha. Katika uchambuzi wa taarifa ya Shirika kwa Kamati ilibainika kuwa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha kina uchakavu mkubwa wa miundombinu.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu ya kada ya kati, na kwamba Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha ambacho ni chuo cha kati, **Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti ya kuifanyia matengenezo miundombinu ya chuo hiki ili kiweze kutoa elimu kama ilivyokusudiwa.**

**2.4.1.11 Tume ya Utumishi wa Walimu**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Walimu *(Teachers Service Commission – TSC)* imepewa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 Kifungu Na. 5(i) – (xii). Kwa ujumla Tume ya Utumishi wa Walimu ina jukumu la kusimamia utendaji wa walimu nchini katika nyanja mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 Tume ya Utumishi wa Walimu iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 20,742,102,000.00.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 17,277,111,000.00** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi 3,464,990,667.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Desemba, 2024 Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 9,899,459,662.51** sawa na **asilimia 48** ya kiasi cha Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025. Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,159,270,278.00** ni Mishahara (PE), **Shilingi 3,247,204,249.33** ni matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 1,492,985,135.18** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Desemba, 2024 Tume ya Utumishi wa Walimu iliendelea kuhudumia jumla ya Walimu 273,736 wa shule za msingi na sekondari waliopo kwenye utumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa taarifa ya Tume ya Utumishi wa Walimu iliyowasilishwa mbele ya Kamati Januari, 2025 Kamati imebaini kuwa Tume ya Utumishi wa walimu haitekelezi majukumu yake kama ilivyoelekezwa kwenye sheria iliyounda Tume hiyo. Aidha, Kamati imebaini kuwa majukumu mengi ya Tume yanatekelezwa na taasisi nyingine za umma. Kwa mfano, suala la kuajiri walimu halitekelezwi tena na Tume, na kwamba hata mchakato wa ajira za walimu Tume haihusishwi. Aidha, kwa upande wa msawazo wa walimu kwenye halmashauri Tume haikutekeleza kutokana na msawazo huo kutekelezwa na taasisi nyingine ya umma. Kamati inaona kuwa hali hii inaondoa umaana na umuhimu wa Tume. **Kamati inashauri Serikali kuipitia upya Sheria iliyokiunda chombo hiki na ikiwezeshe chombo hiki kutekeleza majukumu yake iliyopewa kisheria ili kiweze kuwa na tija kwa walimu nchini.**

**2.4.2 Utekelezaji wa Miradi na Programu mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini**

***2.4.2.1 Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari Nchini (SEQUIP)***

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa mkopo wa fedha za Kimarekani **Dola milioni 500** sawa na fedha za Kitanzania **Shilingi Trilioni 1.2**. Lengo kuu la mradi huu ni kuhakikisha kuwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanaboreshwa katika shule za Sekondari ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana waliopo katika shule za sekondari, pamoja na kuhakikisha wanafunzi wote wanaoanza masomo ya sekondari wanamaliza Elimu ya Sekondari.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya shughuli zilizopangwa katika kutekeleza Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari

(SEQUIP) ni ujenzi wa Shule mpya za Sekondari za Bweni za Wasichana katika Mikoa yote nchini. Ujenzi wa shule hizi ulianza Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo kundi la kwanza lilihusisha ujenzi wa shule 10 katika mikoa ya Kagera, Shinyanga, Mwanza, Singida, Songwe, Njombe, Ruvuma, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Kundi la pili lilihusisha ujenzi wa shule 16 katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya, Mtwara, Katavi, Rukwa, Tabora, Mara, Geita, Simiyu, Kigoma, Tanga, Manyara, Arusha na Kilimanjaro kwa bajeti ya **Shilingi 4,100,000,000.00** kwa kila shule.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa hadi Disemba, 2024 kundi la kwanza la ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya Shule za Wasichana za Mikoa Nchini lilikuwa kati ya wastani wa asilimia 75 hadi 96 kulingana na utekelezaji kimikoa. Aidha, kundi la pili la awamu ya kwanza lilikuwa kati ya wastani wa asilimia 70 na 95.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa kundi la pili la shule mpya za Sekondari za bweni za Wasichana unafanyika katika mwaka 2024/2025 kupitia bajeti ya Mwaka 2023/2024 (bakaa) ambapo fedha kwa ajili ya utekelezaji zimekwishatumwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mwishoni mwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. **Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kutekeleza mradi huu ambao ni ukombozi mkubwa kwa mtoto wa kike wa Kitanzania.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi huu bado Kamati imebaini kuwa kumekuwa na changamoto kadhaa katika ukamilishaji wake, ikiwa ni pamoja na baadhi ya watendaji kushindwa kutekeleza jukumu la usimamizi wa ujenzi, kasi ndogo ya ujenzi ambayo husababisha hatua mbalimbali za ujenzi wa miundombinu kufanyika kwa muda mrefu, manunuzi ya vifaa vya ujenzi yasiyozingatia sheria na taratibu za ununuzi wa umma, kukosa

ushirikishaji wa jamii na kamati katika kufanya maamuzi hivyo kusababisha ucheleweshaji wa upatikanaji wa vifaa na kushindwa kufuata maelekezo na miongozo iliyotolewa na mamlaka husika. **Kamati inaishauri Serikali kuusimamia kwa ukaribu mradi huu ili uweze kufanyika kwa ubora zaidi.**

***2.4.2.2 Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto Katika Mikoa na Halmashauri***

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutunukiwa Tuzo ya Heshima inayoitwa *The Global Goalkeeper Award* inayotolewa na *Gates Foundation* kama kuutambua mchango wa Tanzania kwenye mafanikio katika kutokomeza vifo vinavyotokana na ujauzito, vifo vya watoto wachanga, pamoja na lishe afya kwa watoto.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zipo mstari wa mbele katika kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga ili kuweza kufikia Malengo ya Maendeleo endelevu *(Sustainable Development Goals (SDG 3)* ifikapo Mwaka 2030. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kitaifa ya Demografia ya Viashiria vya Afya na Malaria ya Mwaka 2022 *(TDHS- MIS 2022)* vifo vya wajawazito nchini vimepungua kutoka **556** kwa kila vizazi **hai 100,000 kwa mwaka 2015/2016** hadi **104** kwa kila vizazi **hai 100,000 kwa mwaka 2021/2022 ambayo ni sawa na upungufu wa vifo 76 kila mwaka.** Aidha, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimeendelea kupungua ambapo kwa mwaka 2015/2016 vilikuwa 67 kwa kila vizazi hai 1,000 na mwaka 2021/2022 vilikuwa 43 kwa kila vizazi hai 1,000, sawa na kupungua kwa asilimia 36. **Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi hizi za kupunguza vifo vya Mama na Mtoto. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka**

**mikakati ya kuwezesha vifo hivi kupungua zaidi na ikiwezekana visiwepo kabisa.**

***2.4.2.3 Uboreshaji wa Afya za Wananchi na Utekelezaji wa Miradi ya Afya ya Msingi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.***

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Juni, 2024 Serikali ilitumia kiasi cha **Shilingi bilioni 29.32,** fedha za ndani za maendeleo kwa ajili ya ujenzi miundombinu mipya ya vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Hospitali za Wilaya kwa lengo la kuboresha afya za wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukarabati wa hospitali kongwe katika halmashauri za Wilaya Serikali imeendelea na mkakati wake wa kuzikarabati hospitali hizo ambapo hadi kufikia Juni, 2024 jumla ya **Shilingi bilioni 27.9** fedha za ndani za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya zimetolewa. **Kamati inaipongeza sana Serikali kwa juhudi hizi za kukarabati hospitali kongwe.**

***2.4.2.4 Utekelezaji wa Huduma za Chakula na Lishe Shuleni kwa Shule za Elimu ya Msingi***

**Mheshimiwa Spika,** Huduma ya chakula na lishe ni ajenda muhimu katika masuala mbalimbali yatakayoisadia nchi kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu *(Sustainable Development Goals – SDG)* ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuifikia azma hii Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina wajibu wa kuhakikisha kwamba inasimamia Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimumsingi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa afua za lishe shuleni kutoka kwenye halmashauri mbalimbali

zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na mkakati wa kuelimisha umma kuhusiana na afua za lishe unaotekelezwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa taarifa kuhusu lishe Shuleni, ilyowasilishwa na Wizara Kamati imebaini kuwa bado suala la lishe limekuwa ni gumu kutekelezeka kwa baadhi ya shule nchini. Aidha, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya halmashauri zinazotoa chakula shuleni hutoa chakula cha aina moja tu, hasa ugali na kande. Kamati imebaini pia kuwa wazazi wengi hawaoni umuhimu wa kutoa chakula kwa ajili ya watoto wao kula wawapo shuleni. Aidha, shule nyingi zinazotoa lishe shuleni zina ukosefu wa miundombinu ya uchanganyaji wa chakula lishe. Changamoto hizi zinasababisha utolewaji wa lishe shuleni kuwa wa duni. **Kamati inashauri elimu na kampeni mbalimbali zitolewe kwa wananchi, hasa wazazi wenye watoto shuleni kuona umuhimu wa watoto kupata chakula shuleni na hivyo kushiriki kikamilifu katika kuchangia chakula shuleni. Aidha Kamati inashauri hamasa kubwa itolewe kwa wazazi, hasa wazazi wa kiume kujihusisha katika utolewaji wa lishe shuleni.**

***2.4.2.5 Ununuzi wa Vifaa na Vifaa Tiba kwa ajili ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali katika Halmashauri nchini***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/2024 kiasi cha **Shilingi bilioni 117.37** kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye vituo 678 vya kutolea huduma za Afya (Hospitali 32, Vituo vya Afya 278 na Zahanati 368). Aidha, katika kipindi hicho Serikali ilipeleka **Shilingi bilioni 114.27** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba vya vituo vya kutolea huduma za Afya ambapo **Shilingi bilioni 60.62** zimetumika sawa na asilimia 53. Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi hizi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo Kamati imebaini changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa

miradi yote inayohusu afya nchini. Moja ya changamoto kubwa iliyojitokeza ilikuwa ni kuhusiana na manunuzi kwa kutumia mifumo ya NeST ambao ulihitaji Maafisa Ununuzi wa Halmashauri kupatiwa mafunzo kabla ya kuanza kufanya ununuzi na hivyo kusababisha kuchelewa kuanza kutekelezwa kwa miradi. Aidha, Kamati imebaini kuwa pamoja na mafunzo hayo kutolewa bado kumekuwa na uelewa mdogo wa matumizi ya mfumo huo wa manunuzi. Wizara inaendelea na juhudi za kutoa elimu kwa watumiaji wote wa Mfumo wa Manunuzi wa NeST. **Kamati inashauri Serikali kendelea kutoa mafunzo juu ya manunuzi ya umma kwa kupitia mfumo huo ambao umeonesha mafanikio na ufanisi mkubwa.**

***2.4.2.6 Hali ya Udumavu nchini na mikakati ya kutokomeza udumavu***

**Mheshimiwa Spika,** udumavu ni hali ya ukuaji duni wa mtoto inayosababisha mtoto kuwa na kimo/urefu pungufu ukilinganisha na umri wake. Hali hii inajitokeza tangu kipindi cha ujauzito hadi kipindi cha miaka miwili mpaka kufikia umri wa miaka mitano baada ya kuzaliwa. Sababu kubwa za tatizo hili ni pamoja na hali duni ya lishe au magonjwa kwa mama mjamzito, taratibu duni za unyonyeshaji watoto maziwa ya mama, upungufu katika taratibu za ulishaji watoto vyakula vya nyongeza wanapofikia umri wa miezi sita na magonjwa yanayowakabili watoto katika kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI anayeshughulikia Afya Mheshimiwa Festo Dugange aliyoitoa katika hafla ya kusaini hati za makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa lishe unaofadhiliwa na Shirika la USAID iliyofanika Mei 7, 2024 katika ukumbi wa Sokoine Jijini Dodoma inaonesha kuwa kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano bado ni kikubwa ambapo kwa mkoa wa **Kigoma ni 27.1%, Katavi 32.2%, Njombe 50.4%, Songwe 31.9% Rukwa 49.8%, na**

**Iringa 56.9.** Kamati inaona kuwa kiwango hiki ni kikubwa na hivyo juhudi za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kupunguza ukubwa wa tatizo hili.

**Mheshimiwa Spika,** kulingana na Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya ya mwaka 2015 – 2016, takriban theluthi ya watoto wote chini ya miaka mitano wana udumavu na asilimia 14 wana upungufu wa uzito. Sababu kuu zinazoongoza kuleta utapiamlo pamoja na nyinginezo, ni mienendo duni ya lishe.

**Mheshimiwa Spika**, suala la udumavu ni suala ambalo si gumu kama nchi itakuwa na nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa tatizo hili linakwisha. Kamati inadhani kuwa bado Serikali haijafanya juhudi za kutosha katika kuhakikisha kuwa suala la udumavu linatokomezwa. Kamati inaamini kuwa kwa kiwango cha chini uchumi wa mtu mmoja mmoja kina nafasi ya kuwafanya Watanzania wasiathirike na udumavu. Kamati inaamini ni utamaduni wa ulaji na upangaji wa lishe ndivyo vinavyosababisha udumavu nchini kwa kuwa hakuna familia inayoshindwa kupata vyakula vya msingi vitakavyowezesha kuondokana na tatizo la uduma. **Kamati inashauri Serikali kuanzisha kampeni mbalimbali za kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kupangilia milo na kubadilisha mitindo ya maisha.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaridhishwa sana na baadhi ya mikakati ya Serikali kwa baadhi ya mikoa nchini katika juhudi zake za kupambana na udumavu nchini. Kwa mfano Mkoa wa Njombe Wilaya ya Makete miongoni mwa mikakati waliyonayo wameweka mkakati wa kugawa ng'ombe wawili wa maziwa wa kisasa ili watoto waweze kunywa maziwa shuleni. Kamati inashauri Serikali kuzishauri Halmashauri nyingine kuiga mfano huu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua kuwa Wanaume wana mchango mkubwa katika malezi na makuzi ya mtoto, Mkoa wa Iringa uliandaa kongamano la wanaume ambalo lilifanyika tarehe 19 Novemba, 2024 kwa kuwakutanisha

wanaume **1,325.** Lengo likiwa ni kuwashirikisha wanaume kwenye mambo mbalimbali ya Maendeleo.

### *2.4.2.7 Hali ya Mgawanyo wa Watumishi wa Afya na Elimu Katika Halmashauri nchini*

**Mheshimiwa Spika**, watumishi wa kada mbalimbali wa Sekta ya Afya ni nguzo muhimu katika utoaji wa huduma za afya zenye ubora unaotakiwa. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha kwamba kuna idadi ya kutosha ya rasilimaliwatu kwa kuajiri watumishi wenye sifa katika vituo vya kutolea huduma za afya katika halmashauri zote nchini. Kutokana na uendelezaji wa miundombinu unaoendelea katika Halmashauri mbalimbali nchini kote hivi sasa kumekuwa na ongezeko la uhitaji wa watumishi wa kada mbalimbali za sekta ya afya.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaonesha kuwa hadi kufikia Desemba, 2024 Tanzania ina vituo vya huduma za Afya 7,238 vinavyofanya kazi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kamati ilijulishwa kuwa ili kuweza kuvihudumia vituo hivi vyote wanahitajika watumishi 142,147 wa kada mbalimbali za afya ngazi ya msingi. Hata hivyo, taarifa hiyo inaonesha kuwa hadi mwezi Disemba 2024 vituo hivyo vilikuwa na watumishi 66,625 (sawa na asilimia 46.8) ya mahitaji watumishi. *(Tazama Jedwali Namba 2)*

| Na. | Idadi ya watumishi inayotakiwa | Idadi iliyopo | Upungufu | Asilimia ya upungufu |
|---|---|---|---|---|
| | 142,147 | 66,625 | 75,522 | 53.2 |

*Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi hapo juu **Kamati inaona kuwa watumishi wa afya kuwa asilimia 46.8, ambayo ni chini ya asilimia 50 ni hatari kwa uimarishaji wa afya kwa ajili ya kujenga taifa la watu wenye siha njema nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, katika uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kuhusiana na msawazo wa walimu nchini Kamati imebaini kuwa maeneo mengi ya vijijini yana hali ngumu sana ya maisha. Kutokana na ugumu wa maisha vijijini, hasa huduma za maji, umeme na Barabara (Usafiri) watumishi wengi wa sekta ya elimu na afya huhama ama kuhangaikia kuhama kutoka vijijini kwenda mijini. Kwa ujumla mazingira yasiyovutia yamekuwa yakisababisa watumishi wengi wa kada za afya na elimu katika halmashauri kuhama kwa kasi ama hata kuacha kazi wakati mwingine. **Kamati inashauri Serikali kuboresha mazingira ya kufanyia kazi katika halmashauri nchini hasa vijijini. Aidha, Serikali iweke motisha kwa walimu na watumishi wa kada ya afya wanaofanya kazi katika mazingira magumu.**

***2.4.2.8 Uboreshaji wa Mazingira, Upandaji miti na uwezekano wa kufaidika na biashara ya kaboni nchini***

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali za kutunza mazingira, hasa sekta ya upandaji na utunzaji wa miti.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mazingira bora, hasa miti na misitu kuongeza uboreshaji wa afya kwa jamii misitu pia imekuwa ikileta faida kubwa kwa upande wa uchumi baada ya miaka ya hivi karibuni kuibuka kwa biashara ya kaboni inayotokana na mkakati wa kutunza misitu kwa ajili ya kufidia uzalishaji wa kaboni duniani.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha usimamizi endelevu wa mazingira hapa nchini OR-TAMISEMI imeendelea kuhamasisha na kufanya ufuatiliaji wa miradi ya Kaboni katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kuwa biashara hiyo inaendeshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za nchi.

**Mheshimiwa Spika,** biashara ya kaboni kwa sasa inafanyika katika Halmashauri 16 za Tanganyika, Karatu, Mbulu, Kiteto, Muleba, Ngara, Misenyi, Bukoba Vijijini, Karagwe na Kyerwa. Aidha Halmashauri tano za Tunduru, Namtumbo, Longido, Monduli na Kilwa zipo katika hatua mbalimbali za maandalizi ya miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** mapato yatokanayo na uuzaji wa Kaboni (*Carbon Credit*) katika Halmashauri yameongezeka na kufikia kiasi cha **Dola za Kimarekani 12,630,350** sawa na **Shilingi bilioni 32** tangu biashara hii ilipoanza mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na utunzaji wa misitu kuleta faida kubwa, hasa ya kiuchumi Kamati inashauri Serikali kuweka mkakati maalum wa kuwezesha matumizi yatakayowezesha halmashauri kufaidika zaidi na biashara ya kaboni.

**Aidha, fedha zinazotokana na biashara hiyo ziwafaidishe wananchi moja kwa moja ili waweze kuona umuhimu wa kutunza mazingira yao.**

**Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kuimarisha shughuli za miradi ya biashara ya Kaboni OR-TAMISEMI imeweka mikakati mbalimbali ambayo inatarajia kuitekeleza, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuelimisha umma na kujenga uwezo wa Halmashauri na vijiji kuhusu taratibu, jinsi ya kushiriki na upatikanaji wa wawekezaji wa biashara hiyo, kujenga uwezo wa kuandaa miradi ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya usimamizi endelevu wa bioanuwai, kuendelea kuimarisha ushirikiano na Wizara, Taasisi na wadau wanaohusika na masuala ya uhifadhi wa mazingira, kukamilisha Mkakati wa ngazi ya kati na msingi unaohusu usimamizi jumuishi wa bioanuwai na mabadiliko ya tabianchi (*Intergrated Biodiversity Conservation Strategy for Local Government*), kukamilisha Mkakati wa Uongoaji wa Misitu inayomilikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wadau (*Forest restoration program for Local*

*Government Authority*), na kuratibu uanzishwaji wa miradi ya uchakataji wa mabaki ya bidhaa za kilimo kwa lengo la kuzalisha nishati ili kushiriki katika Biashara ya Kaboni.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, katika uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, imebainika kuwa miongoni mwa miradi inayoweza kuleta faida kama biashara ya kaboni ni uzalishaji na uchakataji wa taka ngumu.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa OR-TAMISEMI zilizowasilishwa mbele ya Kamati kuhusiana na uzalishaji wa taka nchini zilionesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa inazalisha kiasi cha tani milioni 12.1 hadi milioni 17.4 kwa mwaka ambapo kila Mtanzania anakadiriwa kuzalisha kiasi cha kilo 241 hadi kilo 347 kwa mwaka *(Atin & Siddharth, 2021)*. Aidha, Dar es Salaam pekee inazalisha taka tani 1,551,980 kwa mwaka na tani 4,252, sawa na asilimia 12.8 na asilimia 12.8 mtawalia. **Kamati inashauri Serikali kuanza kuangalia namna ya kutumia taka ngumu kwa ajili ya uanzishwaji wa miradi ya kaboni.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio na iliyopatikana **katika utunzaji wa mazingira na kanzishwa na kuendelea kwa biashara ya kaboni nchini,** zipo baadhi ya changamoto ambazo OR - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri imekabiliana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na: -

(i) Upungufu wa vitendea kazi, watumishi na uhaba wa fedha kwa ngazi ya OR - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri;

(ii) Kukosekana kwa mipango madhubuti ya pamoja inayohusu uratibu wa masuala yanayohusu uhifadhi, usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi baina ya wizara za uratibu na Wizara za kisekta.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuanzisha kitengo maalum ndani ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kukiwezesha ili kiweze kuratibu vyema masula yote yanayohusiana na mazingira na biashara ya kaboni nchini.

### *2.4.2.9 Upangaji wa Machinga Katika Maeneo Maalumu katika Halmashauri Nchini*

**Mheshimiwa Spika,** Wafanyabiashara ndogondogo nchini ni sehemu muhimu katika uendeshaji wa uchumi wa nchi kwa kuwa mchango wao kwenye mzunguko wa fedha na huduma ni mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikiweka juhudi mbalimbali za kuhakikisha kwamba Wamachinga wanapata maeneo mazuri ya kufanyia biashara zao kwa kuwatengea maeneo maalum katika miji na majiji nchini, na hivyo kurahisisha ufanyaji wao wa biashara. Serikali imejenga masoko kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kufanya biashara kwa utulivu katika maeneo maalum na si kupanga biashara Barabarani na maeneo yasiyoruhusiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano Serikali imeliboresha soko la Wamachinga la Old Airport lililopo Mkoa wa Mbeya kwa kujenga miundombinu muhimu kama vile vivuli kwa ajili wauza mitumba na chakula (Mama na Baba lishe). Zoezi la kujenga miundombinu kwa ajili ya kuwapanga wamachinga ambao hawakuwa katika maeneo rasmi ya kufanyia biashara Jiji la Dar es Salaam imefanyika katika masoko 10 kati ya masoko 31. Aidha, Jiji la Dodoma limejenga soko la kisasa la Wamachinga ambalo limeonesha mafanikio makubwa sana katika utekelezaji wake. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa ujenzi huu wa majengo ya masoko ya wamachinga nchini. **Kamati inashauri ujenzi wa masoko ya wamachinga nchini, kwa mfano wa Soko la Dodoma yajengwe nchi nzima kulingana na mahitaji.**

**Mheshimiwa Spika;** Kamati pia imebaini kuwa Mkoa wa Dar es Salaam una program ya uhamasishaji na usajili wa wafanyabiashara wadogo (wamachinga) ambayo ilianza rasmi tarehe 28 Februari, 2024. **Kamati inaupongeza Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuendelea kuwasajili wafanyabiashara wadogo ili kuwawezesha kwanza kutambulika kirahisi na pili kupata faidia ya kupata huduma mbalimbali za kiserikali.**

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kasi ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwa ajili ya wamachinga ni ndogo ukilinganisha na idadi ya wamachinga nchini na kasi ya kukua na kuongezeka kwa wafanyabiara ndogondogo.

Aidha, juhudi za kuwapanga Wamachinga zimekuwa zikionekana zaidi katika majiji na kuacha Halmashauri za Manispaa na miji bila mipango Madhubuti ya kuwapanga Wamachinga. Katika uchambuzi wa taarifa za Wizara zilizowasilishwa mbele ya Kamati, ilibainika kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikiweka mikakati mbalimbali ya kuwapanga Wamachinga ili kuondoa ukaaji holela unaofanywa na Wafanyabiashara hao katika miji na manispaa mbalimbali nchini. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa juhudi zinazowekwa na Serikali bado hazitoshelezi kuondoa changamoto za ukaaji holela wa Wamachinga nchini. **Kamati inashauri Serikali kuongeza juhudi katika kupanga na kujenga miundombinu kwa ajili ya wamachinga nchini katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji mbalimbali nchini.**

### *2.4.2.10 Utengaji na Matumizi ya Mapato ya Ndani Katika Sekta ya Kilimo na Mifugo kwa Mwaka 2023/2024*

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikadiria kukusanya shilingi **215,101,366,070.62** kutoka vyanzo vya ushuru wa mazao ya kilimo na mifugo. Makadirio ya fedha zilizotakiwa kutolewa kuendeleza sekta hizo ni shilingi **43,296,530,434.31.**

Hali halisi ya makusanyo kutoka vyanzo hivyo ni **shilingi 226,879,000,902.34.** Kutokana na makusanyo hayo halisi **Shilingi 45,213,513,666.59** zilitakiwa kutolewa na kutumika kwa ajili ya kuendeleza Sekta za Kilimo na Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 **shilingi 7,104,201,683.36** sawa na **asilimia 16.41** zilitumika kuendeleza sekta hizo na hivyo kutokufikia lengo lililowekwa.

Kamati inaona kuwa Mamlaka hazijafanya juhudi za kutosha za kupeleka fedha hizo kwa ajili ya kuendeleza sekta za kilimo na mifugo.


**Kamati inashauri halmashauri zihakikishe kuwa fedha zinazopaswa kutengwa na kupelekwa ajili ya kilimo na mifugo zinapelekwa kwa utimilifu na kwa wakati.**

*Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa makusanyo ya mapato ya ndani na utolewaji wa makusanyo kwa ajili ya maendeleo ya kilimo na mifugo*

| Na. | Kiasi kilichotengwa | Kiasi kilichokusanywa | Ongezeko | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 215,101,366,070 | 226,879,000,902 | 11,777,634,832 | 105.5 |

*Chanzo: Taarifa za Wizara na Usanifu wa Kamati*

Kielelezo Na 3: *Mchanganuo wa upangaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya kilimo na mifugo*




*Chanzo: Taarifa za Wizara na Usanifu wa Kamati*

### *2.4.2.11 Utekelezaji na Ukamilishaji wa Mradi wa Kitega Uchumi cha Usafirishaji na Biashara cha Afrika Mashariki (East African Commercial and Logistics Center – EACLC)*

**Mheshimiwa Spika;** Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inatekeleza uwekezaji wa Kitega Uchumi cha Mradi wa Uwekeza wa Kituo cha Usafirishaji na Biashara cha Africa Masharikia *(The East Africa Commercial and Logistics Center – EACLC)*. Mradi huu unatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na mwekezaji aitwaye Shanghai Linhang Group Ltd. Mradi huu unaotekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership – PPP)* unafanyika katika eneo la iliyokuwa stendi ya zamani ya mabasi Ubungo kwa gharama ya **Shilingi 303,300,000,000.00.** Gharama hii inajumuisha fedha za mwekezaji **shilingi 280,000,000,000.00** na Fedha za Manispaa kiasi cha **Shilingi 23,300,000,000.00.** Hadi kufikia Agosti, 2024 jumla ya **Dola za Kimarekani 95,000,000.00** sawa na **Shilingi za Kitanzania 242,250,000,000.00** zilikuwa zimetumika.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi kutekelezwa tarehe 1 Mei, 2023 na ulitarajia kukamilika mwezi Oktoba, 2024. Utekelezaji wa mradi umeshakamilika kwa awamu ya kwanza ya muundo wa jengo na kwa sasa awamu ya pili kazi ya umaliziaji inaendelea. Kamati ilielezwa

kuwa hadi kufikia Oktoba, 2024 mradi ungekuwa umekwishakukamilika na kuzinduliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa ubunifu huu wa uwekezaji kwa kutumia mfumo wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Hii ni dalili kuwa pamoja na kukua kwa biashara ndani ya nchi lakini pia biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine inaendelea kukua na kuimarika. Aidha, mradi huu utaongeza mapato kwa Serikali, kuimarisha uchumi kutokana na kuongezeka kwa mzunguko wa fedha kupitia wageni, kukuza uhusiano wa Kimataifa na kupendezesha Jiji. **Kamati inapongeza kwa juhudi za Serikali kuongeza idadi ya masoko ya kimataifa nchini na hususan katika Jiji la Dar es Salaam. Kamati inashauri Serikali kuutekeleza mradi huu kwa uangalifu ili soko hili likishafunguliwa lisiathiri Soko la sasa la Kimataifa la Kariakoo.**

## 2.5 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa za Wizara inayoisimamia kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Mwaka 2023/2024 iliyosomwa na kujadiliwa na Bunge Februari 13, 2024. Maazimio hayo yalitolewa kwa msingi wa matarajio ya wananchi kuhusu shughuli za umma na ustawi wa wananchi nchini. Kilichofanyika ni kuonesha matarajio na kuacha uhuru kwa utekelezaji ndani ya kipindi cha Februari, 2024 – Januari, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa kwa asilimia kubwa maazimio hayo yametekelezwa, na yaliyobaki Kamati imefahamishwa kuwa michakato ya utekelezaji wake inaendelea. Taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo ni kama ifuatavyo: -

**2.5.1 Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali**.

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa azimio hili Serikali imeieleza Kamati kuwa imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za mitaa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Kanuni zake katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara haikuwasilisha kwa Kamati waraka, barua ama mwongozo wa maelekezo uliotolewa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za mitaa hali iliopelekea Kamati kushindwa kupata Ushahidi wa utekelezaji wa azimio hili.

**2.5.2 Utaratibu wa Halmashauri Nchini kutumia asiliia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa Makundi Maalum.**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilipitisha azimio la kuitaka Serikali kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni juu ya utaratibu mzima wa Halmashauri Nchini kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani ili mfuko huo uweze kukidhi makundi yote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kuwa pamoja na mambo mengine Serikali imeshaanza mchakato wa kutekeleza maagizo hayo, ambapo mpaka sasa wameshaunda timu ya kuandaa Rasimu ya marekebisho ya Sheria ili yaweze kuzingatiwa wakati wa kuandaa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023.

**2.5.3 Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Haraka Dar es Salaam (DART)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika azimio hili la Bunge, Bunge iliitaka Serikali kuandaa Mswada wa Sheria utakaoweka mfumo mzuri utakaosimamia Usafiri wa Umma Mijini.

Wizara imeieleza Kamati kuwa Serikali imekamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu pendekezo la kutungwa kwa Sheria ya Usafiri wa Umma Mijini. Waraka huo kwa sasa upo kwenye ngazi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, baada ya kupita ngazi mbalimbali mswada utawasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeahidi kuuleta Mswada huo Bungeni mapema iwezekanavyo.

### 2.5.4 Uendeshaji wa Masoko Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Katika azimio hili la Bunge, Bunge iliitaka Serikali iweke utaratibu Madhubuti wa kisheria utakaobainisha ufanyaji kazi wa wahusika wote wa usimamizi wa masoko wakiwemo watu wa kati pamoja na kubainisha bei elekezi ya upangishaji wa vizimba vya sokoni.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imefanya uchambuzi wa changamoto zilizobainishwa na Bunge na kubaini chanzo cha changamoto hii ni Sheria zinazosimamia masoko Nchini. Aidha, uchambuzi umefanyika ili kubaini mapungufu katika Sheria ndogo zinazosimamia uendeshaji wa masoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uchambuzi huu utaiwezesha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuandaa Sheria ndogo ya Mfano itakayozingatia masuala ya bei na upangishaji wa vizimba na uwepo wa madalali katika masoko ili itumike na Halmashauri zote Tanzania Bara kuandaa Sheria zao ndogo za usimamizi na uendeshaji wa Masoko Nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imetoa ahadi (*commitment*) kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2025 itakuwa imekamilisha maandalizi ya Sheria Ndogo ya Mfano kwa ajili ya kutumika na Halmashauri kuandaa Sheria Ndogo za kusimamia uendeshaji wa masoko yao. Aidha, Wizara imeahidi kuuleta Mswada wa marekebisho ya Sheria Bungeni.

### 2.5.5 Shirika la Masoko ya Kariakoo

**Mheshimiwa Spika**, Katika azimio hili Serikali ilielekezwa kufanya mambo yafuatayo: -

(i) Serikali iliongezee mtaji Shirika la Masoko Kariakoo ili limudu majukumu yake kikamilifu na kuchangia pato la Taifa na ustawi wa Maisha ya Wananchi; na

(ii) Serikali iandae mapendekezo ya marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo ili kusahihisha upungufu katika Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeieleza Kamati kuwa michakato mbalimbali ili kutekeleza maagizo hayo tayari imeshaanza ambapo hatua iliyofikiwa sasa ni uchambuzi wa Sheria Sura 132 ya Shirika la Masoko ya Kariakoo na kubainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho ya Sheria hiyo. Aidha, ukamilishaji wa hatua zinazofuata za kurekebisha Sheria utaenda sambamba na mwongozo wa mabadiliko utakaotolewa na Serikali.

### 2.5.6 Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maazimio mengine kuhusu TARURA Bunge lilitoa azimio la kuitaka Serikali kutafuta utaratibu endelevu utakaoiwezesha TARURA kupata fedha za kutosha ili iweze kutekeleza kazi zake za kukarabati na kujenga barabara mpya. Kamati ilijulishwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi imeanzisha Hati Fungani ya Samia Infrastucture Bond ambayo itasaidia katika upatikanaji wa fedha kwa lengo la kukusanya zaidi ya **Shilingi 150,000,000,000** zitakazotumika katika miradi ya ujenzi wa miundombinu ya Barabara. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuanzisha hati fungani hiyo

### 2.5.7 Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati Katika Halmashauri Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia kuwa Serikali ifanye marekebisho katika Mwongozo wa Miradi ya Kimkakati utakaotoa fursa sawa kwa Halmashauri zote nchini ili kukidhi azma ya Serikali ya kuongeza mapato ya Halmashauri na kuwezesha ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kwamba Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) tayari wameshaandaa mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji na Ugharamiaji wa Miradi ya Kuongeza Mapato.

## 2.6 Kushiriki katika Semina

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali zilizoandaliwa na Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Aidha, semina hizo zililenga kuwaelimisha Wajumbe wa Kamati ili kuwaongezea ujuzi na uelewa kuhusiana na masuala mbalimbali ya kiutekelezaji ndani ya Wizara na taasisi zake pamoja na kuwakumbusha kuhusu wajibu na majukumu ya Kibunge ambayo wanayatekeleza katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 3.1 MAONI YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Mafanikio na Changamoto zilizobainika katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Upungufu wa watumishi katika sekta ya elimu na afya ni changamoto kubwa kwenye halmashauri nyingi nchini, **Kamati inashauri,** Serikali kuendelea na utaratibu wa kutoa Ajira kwa watumishi wa kada za afya na elimu kwenye halmashauri nchini ili kupunguza tatizo hili;

(ii) Tatizo za msawazo wa walimu nchini limeonekana kuleta changamoto kwa maeneo mengine, hasa ya mijini, kuwa na mrundikano wa watumishi hao ilihali maeneo ya vijijini yanakosa walimu. Kamati inashauri Serikali iiwezeshe Tume ya Utumishi wa Walimu kushughulikia suala la usambazaji wa walimu nchini;

(iii) Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha kina miundombinu chakavu ambayo yanakifanya chuo hiki kushindwa kutekeleza jukumu lake ipasavyo na hivyo kuleta athari kwa wanafunzi wanaosoma katika chuo hicho. Kamati inashauri kuwa Serikali itafute na kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya chuo hicho ambacho ni muhimu sana kwa utoaji wa elimu ya afya kwa Watanzania;

(iv) Bajeti zinazopitishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa shule, barabara na vituo vya afya, zipelekwe kwa wakati ili kuleta tija katika uendelezaji wake. Aidha, Serikali

inapaswa kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wazembe wanaoshindwa kusimamia matumizi ya Fedha zilizopelekwa kwaajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali; na

(v) Uharibifu wa miundombinu ya barabara iliyosababishwa na mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya haikuweza kukarabatiwa kutokana na fedha ndogo zilizopelekwa kwa TARURA. Kamati inaona kuwa uharibifu unaweza kuwa mkubwa zaidi kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na mvua za masika zinazotarajiwa kunyesha hivi karibuni.

**Kamati inaishauri** Serikali kutafuta fedha za dharura na kuzipeleka TARURA ili ziweze kusaidia ukarabati wa miundombinu hiyo ya Barabara.

## 3.2 MAONI MAHSUSI

### 3.2.1 Uimarishaji wa Sekretarieti za Mikoa

**KWA KUWA,** Ofisi nyingi za Waheshimiwa Wabunge majimboni hazina vitendea kazi;

**NA KWA KUWA**, kutokuwepo kwa vitendea kazi katika ofisi za Waheshimiwa Wabunge majimboni kunasababisha Ofisi za Wabunge kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kuwaletea maendeleo wananchi wao;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itenge bajeti kwa ajili ya kununua vitendea kazi kwa ajili ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge zisizo na vitendea kazi.

### 3.2.2 Uimarishaji wa Shirika la Elimu Kibaha

**KWA KUWA,** Serikali iliazimia kuvunja mashirika ya uma yasiyo na faida likiwemo Shirika la Elimu Kibaha;

**NA KWA KUWA,** Shirika la Elimu Kibaha bado ni muhimu kwa maendeleo ya taifa letu; na kwamba Shirika hili halikuundwa kwa lengo la kutengeneza faida;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Shirika la Elimu Kibaha liimarishwe ili liweze kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa katika sheria ya uundwaji wake.

**3.2.3 Ulipaji wa fidia kwa ajili ya upishaji wa Mradi wa Mabasi ya Mwendokasi Dar es Salaam**

**KWA KUWA**, ujenzi wa miundombinu ya BRT awamu ya tano na sita inachelewa kuanza kutekelezwa kutokana na wananchi walio kwenye maeneo ya ujenzi wa miundombinu hiyo kutokulipwa fidia;

**NA KWA KUWA**, kuchelewa huko kunasababisha gharama za utekelezaji wa mradi kuongezeka kutokana na mabadiliko ya kiuchumi nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe kulipa fidia katika maeneo yote yanayotakiwa kujengwa miundombinu ya BRT ambazo hazijalipwa ili miradi hiyo ijengwe kwa wakati.

**3.2.4 Kutatua Mgogoro wa utekelezaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo Kasi kati ya DART na UDART**

**KWA KUWA**, mgogoro uliopo kati ya UDART na DART unasababisha ugumu wa utekelezaji wa Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2024;

**NA KWA KUWA**, kutokutekelezwa kwa sheria hiyo ni kosa kisheria;

**NA KWA KUWA**, kutokutekelezwa kwa sheria hiyo kunasababisha uendeshaji wa shughuli za DART kukwama,

na hivyo kuathiri mipango ya uboreshaji wa usafirishaji katika Jiji la Dar es Salaam na ucheleweshwaji wa mabasi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itatue mgogoro huo haraka ili kuiwezesha *DART* kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 3.2.5 Changamoto ya Udumavu Nchini

**KWA KUWA,** kwenye baadhi ya mikao ya Tanzania bado kuna kiwango kikubwa cha udumavu,

**NA KWA KUWA**, hali ya udumavu inahatarisha ustawi wa taifa hapo baadaye;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba; Serikali iongeze kampeni na kuanzisha program mahsusi ya kuhakikisha kuwa udumavu unatokomezwa nchini na kupima hatua za utekelezaji wa kampeni hiyo kwa kipindi kitakachofaa.

### 3.2.6 Halmashauri Kutumia Mapato ya Ndani kwa ajili ya Utengenezaji wa Barabara

**KWA KUWA,** mvua zinazoendelea kunyesha nchini zinaendelea kuharibu miundombinu ya Barabara;

**NA KWA KUWA, kuharibika kwa Barabara nyingi** kunasababisha usumbufu kwa abiria na kwa wananchi kusafirisha bidhaa mbalimbali kwenda kwenye masoko;

**NA KWA KUWA,** TARURA ina bajeti isiyotosheleza kuharakisha utekelezaji wa urejeshaji wa miundombinu ya Barabara iliyoharibika na mvua mbalimbali na Kimbunga Hidaya kwa wakati;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Halmashauri za Wilaya nchini ambazo zinatakiwa kuchangia asilima 10 kwa

kutumia mapato yao ya ndani waisaidiane na TARURA ili kurejesha Barabara zilizoharibiwa na mvua nchini.

**3.2.7 Kuhusu Serikali kutenga na kupeleka fedha TARURA kama zinavyopitishwa na Bunge**

**KWA KUWA,** upelekaji wa fedha kwenda TARURA unasuasua hata kama fedha hizo zinatengwa;

**NA KWA KUWA,** kutokupeleka fedha hizo kwa wakati kunaendelea kuifanya miundombinu ya Barabara kuendelea kuharibika zaidi;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inaendelea kuleta usumbufu kwa wananchi nchini na kurudisha nyuma usitawi wa wananchi hao;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba fedha zote zinazotengwa kwenye bajeti ya TARURA ziende kama zilizvyotengwa na kwa wakati.

**3.2.8 Matumizi ya Mfumo wa Manunuzi wa NEST**

**KWA KUWA,** watendaji wengi katika Halmashauri nchini bado hawana uelewa wa ndani kuhusiana na matumizi ya mfumo wa manunuzi wa NEST;

**NA KWA KUWA** kuwepo kwa uelewa mdogo wa watendaji katika Halmashauri nchini kuhusiana na matumizi ya mfumo wa manunuzi wa NEST kunasababisha miradi mingi kukwama ama kuchelewa, ama kutekelezwa kwa kiwango cha chini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali itafute njia bora ya kuhakikisha kwamba tatizo la mfumo wa manunuzi linatatuliwa ili shughuli za manunuzi zifanyike kwa wakati na kwa ufanisi unaotakiwa.

### 3.2.9 Ukosefu wa hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo

**KWA KUWA** Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo hakina hosteli za kutosha kwa ajili ya wanafunzi wa chuo hicho na hivyo kufanya wanafunzi wengi kuishi kwenye nyumba za watu binafsi;

**NA KWA KUWA** wanafunzi hao kuishi kwenye nyumba za watu ambazo usalama wake ni mdogo kunasababisha wanafunzi hao kutokuwa salama, hali inayotishia kushuka kwa uwezo wao wa kujifunza na hivyo kupunguza kiwango cha ufaulu;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iharakishe mchakato wa ujenzi wa hosteli kwa mfumo wa Ushirika kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership – PPP)* ili kujenga hosteli zitakazosaidia kuwafanya wanafunzi wote kuishi ndani ya chuo;

### 3.2.10 Uwepo wa wimbi kubwa la watumishi wa Afya na Elimu kuhama maeneo ya vijijini, hasa yenye mazingira magumu kwenda mijini

**KWA KUWA** kumekuwa na wimbi kubwa la watumishi katika kada za afya na elimu kuhama maeneo ya halmashauri yenye mazingira magumu kuishi;

**NA KWA KUWA** kuhama kwa watumishi hao kunaacha ombwe la upungufu wa watumishi katika Sekta za Afya na Elimu katika maeneo yenye mazingira magumu, hasa ya vijijini;

**NA KWA KUWA upungufu huo unazidisha ugumu usitawi** hafifu wa maisha na huduma kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo;

**KWA HIYO** BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali iboreshe mazingira kwa kutoa kipaumbele katika uboreshaji wa huduma za watumishi katika maeneo hayo.

### 3.2.11 Halmashauri kuchangia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

**KWA KUWA** chanzo kimojawapo cha bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ni michango kutoka halmashauri zote nchini;

**NA KWA KUWA** halmashauri nyingi nchini hazitekelezi jukumu hili la kuchangia Bodi ya Mikopo ya Serikali ya Mitaa;

**NA KWA KUWA** kukosekana kwa michango kutoka katika Halmashauri kunasababisha Bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mkakati wa kuzilazimisha Halmashauri kuichangia na kulipa malimbikizo ya madeni ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;

### 3.2.12 Ukamilishaji wa Maboma ya Afya na Elimu na vyoo katika Halmashauri nchini

**KWA KUWA** kuna maboma mengi yaliyojengwa kwa kwa nguvu za wananchi kwa ajili ya huduma za afya, elimu na vyoo yamebaki bila kumaliziwa kwa sababu ya Halmashauri kukosa fedha;

**NA KWA KUWA kuendelea kuwepo kwa maboma hayo** kunanyima utoaji wa huduma kwa wananchi, aidha kunasababisha maboma hayo kuchakaa hata kabla ya kwisha;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali itafute fedha za dharura kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Mawaziri Mhe. Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) pamoja na Mhe. Zainab Katimba kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndg. Adolf Ndunguru kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Jafari Wambura Chege, kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, ninatambua na kuthamini michango yao adhimu na kujitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu. Orodha ya majina ya Wajumbe wa Kamati ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb. – **Mjumbe**
4. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb. “
5. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb. “
6. Mhe. Zacharial Paulo Issaay, Mb. “
7. Mhe. Salome Wycliff Makamba, Mb. “
8. Mhe. Mwita Mwikabe Waitara, Mb. “
9. Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb. “
10. Mhe. Amandus Julius Chingulile, Mb. “
11. Mhe. Doroth George Kilave, Mb. “
12. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb. “
13. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb. “

14. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb. “
15. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mb. “
16. Mhe. Erick James Shigongo, Mb. “
17. Mhe. Ameir Abdalla Ameir, Mb. “
18. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb. “
19. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, Mb. **“**

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee pia ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Baraka Idelphonce Leonard** kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake, pamoja na Sekretarieti ya Kamati hii, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Justin Lazaro Nyamoga (Mb),
**MWENYEKITI**
**KAMATI YAKUDUMU YA BUNGE YA TAWALA**
**ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
11 Februari, 2025

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hoja imeungwa mkono, ninashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, ili aweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati kwa Kipindi cha Februari 2024 – Januari 2025. Karibu Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kwa kipindi cha mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka, 2024. Taarifa hii imejikita katika kuelezea shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Taarifa yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muundo na majukumu ya Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii imeundwa na Sehemu Kuu Nne kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

(ii) Sehemu ya Pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyotekelezwa wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

(iii) Sehemu ya Tatu inatoa maoni na mapendekezo, ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi; na

(iv) Sehemu ya Nne inatoa hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo ni miongoni mwa Kamati 11 za kisekta kwa mujibu wa Kifungu cha 6(8) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia Wizara mbili; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujielekeza katika wigo wa shughuli za Wizara hizo, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimebainisha mambo makuu manne ambayo ni majukumu ya Kamati hii. Mambo hayo ni:

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za Utekelezaji za kila Mwaka za Wizara inazozisimamia; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Katika kuhakikisha shughuli za Kamati zinatekelezwa kikamilifu kwa ufanisi na kwa mujibu wa Katiba huku tukizingatia masharti ya kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kuhakikisha ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupokea na Kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara inazozisimamia pamoja na Idara, Taasisi na Mamlaka mbalimbali zilizo chini ya Wizara;

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iii) Kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara inazozisimamia;

(iv) Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ya Wizara inazozisimamia;

(v) Kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Desemba, 2024); na

(vi) Kufuatilia Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa ya Mwaka kama Kamati ilivyowasilisha kwa Mwezi Februari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu njia na mbinu zilizotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilitekeleza majukumu yake kwa kutumia mbinu na njia zifuatazo:-

(i) Vikao vya kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kujua utendaji wao, mafanikio, changamoto na namna ya kutatua changamoto hizo;

(ii) Ziara ya kukagua maeneo mbalimbali kwa lengo la kujionea utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara na

Taasisi zake na kuzilinganisha na taarifa zilizochambuliwa na Kamati;

(iii) Kufanya uchambuzi wa Taarifa za Bajeti za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi, Asasi za Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyobainika. Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2024 hadi Februari, 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilipata fursa ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2023. Shughuli ambazo zimetekelezwa kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio;

(ii) Kufanya ziara za kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Kupokea uchambuzi na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2024); na

(v) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Taasisi inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupokea Taarifa za utekelezaji wa maazimio. Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa za utekelezaji wa Mazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Lengo la kupokea taarifa hizi lilikuwa ni kufuatilia iwapo Serikali imezingatia Maazimio ya Bunge na kama imezingatia ni kwa kiasi gani yametekelezwa katika kuleta ustawi kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Taarifa za Serikali umeonesha kuwa, Bunge lilipitisha maazimio kumi na moja (11) kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo maazimio nane (8) utekelezaji wake unaridhisha na unaendelea, maazimio matatu (3) utekekelezaji wake si wa kuridhisha. Maazimio hayo ni pamoja na upungufu wa walimu nchini, uchakavu wa miundombinu na upungufu wa wahadhiri Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa Vyuo vya Ufundi usioendana na mahitaji ya wakufunzi na vitendea kazi. Hata hivyo, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo maazimio kumi na tatu (13) yaliyopitishwa na Bunge yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Pamoja na utekelezaji wa maazimio hayo kuendelea, Kamati imebaini kuwa, yapo baadhi ya maazimio utekelezaji wake unahitaji kuwekewa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maazimio hayo ni pamoja na Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha Viwanja vya Arusha na Dodoma, fedha kwa ajili ya ukarabati na uendelezaji wa miundombinu ya viwanja kama Kiwanja cha Benjamin Mkapa na Serikali kuweka utaratibu wa sehemu ya makusanyo kubaki kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa *(Retention)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilitekeleza takwa la kufanyia kazi na ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizo zilifanyika katika Mikoa miwili ambayo ni Arusha na Dar es Salaam kuanzia tarehe 11 – 20 Machi, 2024. Taarifa ya kina kuhusu yaliyobainika katika ziara hizo pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa katika Taarifa ya Bajeti mnamo mwezi Aprili na Juni, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kamati ilitekeleza jukumu la kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46), Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18) na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za kina za uchambuzi wa Bajeti za Wizara hizo, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge uliomalizika Mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2024). Kamati ilipata fursa ya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2024), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46), Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18) na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96).

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha shilingi 1,965,330,380,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2024 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 842.09 sawa na 43% ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 545.72 sawa na 41% ya lengo. Kamati imebaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha si wa kuridhisha kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwani upo chini ya 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18) iliidhinishiwa jumla ya kiasi cha shilingi 2,882,154,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, hadi kufikia Disemba, 2024 Tume ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha shilingi 1,409,540,390.72 sawa na 49%. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa upatikaji wa fedha ni wa kuridhisha kwa upande wa Tume ya Taifa *UNESCO* (Fungu 18).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha shilingi 285,318,387,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba, 2024, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 145.64, sawa na 51% ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 128.71, sawa na 49.8% ya fedha zilizotengwa. Kamati imebaini kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa upande wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni wa kuridhisha kwa sababu upo kwa 49.4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa, baadhi ya miradi ya maendeleo haijatolewa fedha na Serikali. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali itoe fedha katika Wizara hii kama ilivyoidhinishiwa na Bunge ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Kwa kuzingatia matakwa ya Nyongeza ya Kanuni ya 7(1)(d), Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; kwa upande wa hii Kamati ilifuatilia utekelezaji wa mambo yafuatayo:-

(i) Hali ya utolewaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2023/2024;

(ii) Utekelezaji na utoaji wa mikopo kwa Vyuo vya Kati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Hali ya udahili wa wanafunzi wa Vyuo vya Kati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Programu ya Lipa kulingana na Matokeo *(EP4R);*

(v) Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo *(IPOSA);*

(vi) Utekelezaji wa Mitaala mipya katika Programu za Shule za Amali;

(vii) Ujenzi wa Vyuo 64 wa Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)*;

(viii) Utekelezaji wa Tahasusi mpya kwa Kidato cha Tano;

(ix) Namna Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU),* Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(NACTVET)* zilivyoshirikishwa katika kuboresha tahasusi;

(x) Kushughulikia malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa Kada za Afya katika vyuo vya kati; na

(xi) Hali ya upatikanaji wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Kamati ilifuatilia malengo na mikakati ya uendelezaji na uhimizaji wa matumizi ya Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi, ujenzi wa Miundombinu ya Akademia ya Chuo cha Michezo Malya, Maaandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Mataifa ya Afrika *(AFCON, 2027)* na Mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ligi za Ndani ya Nchi *(CHAN, 2025)* hususan ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na ujenzi wa Viwanja katika Mikoa ya Arusha na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu taarifa za utekelezaji uliofanywa na Wizara hizo pamoja na uchambuzi uliofanywa na Kamati, yanapatikana katika Sehemu ya Pili ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ni maoni na mapendekezo ya Kamati. Maelezo ya jumla; baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 pamoja uchambuzi wake, Kamati ina maoni kwa mambo 10 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kuhusu changamoto za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu:

Kwa kuwa, uchambuzi umeonesha kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inakabiliwa na changamoto kama vile: -

(i) Upungufu wa bajeti unaosababisha idadi kubwa ya wanafunzi ambao wanastahili mikopo, kushindwa kumudu gharama za masomo yao; na

(ii) Ukosefu wa vyanzo mbadala vya mapato kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kusaidia idadi kubwa zaidi ya wanafunzi wanaostahili mkopo,

Na kwa kuwa, mfumo wa urejeshaji wa mikopo haujaimarika ipasavyo kutokana na:-

(i) Ukosefu wa mfumo rafiki wa ukusanyaji wa madeni;

(ii) Utaratibu wa ukusanyaji wa madeni kutoka kwa walionufaika na mkopo kutohusisha baadhi ya mifumo kama *NIDA;*

(iii) Uelewa mdogo wa umma kuhusu umuhimu wa kurejesha mikopo, jambo linalosababisha upotevu wa fedha zinazopaswa kurudi kwenye mfuko wa mikopo,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iongeze Bajeti ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ili kuhakikisha wanafunzi wote wanaostahili wanapata mikopo ipasavyo; *(Makofi)*

(ii) Serikali ifanye mabadiliko ya muundo wa Bodi ya Mikopo, ili ifanye kazi kwa muundo wa Mfuko Endelevu wa Fedha *(Revolving Fund)* kwa lengo la kuwa na uhakika wa fedha kwenye Mfuko huo; *(Makofi)*

(iii) Serikali ianzishe mfumo madhubuti wa urejeshaji wa mikopo ambao utaunganishwa na mifumo ya *NIDA*

pamoja na wadau wengine kwa lengo la kupata taarifa za wanufaika kwa wakati na kwa usahihi;

(iv) Serikali iwezeshe vyanzo mbadala vya mapato kwa ajili ya ugharamiaji wa Elimu ya Juu kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na wadau wengine; na

(v) Serikali kongeza juhudi za utoaji wa elimu kwa umma kuhusu wajibu wa urejeshaji wa mikopo kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji endelevu wa fedha za mikopo kwa wanaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa walimu na miundombinu ya kufundishia hasa kwa Mkondo wa Amali:

Kwa kuwa, Shule za Amali nchini zinakabiliwa na chagamoto ya: -

(i) Uhaba wa Walimu wa Amali wenye sifa na weledi na ukosefu wa vyuo maalum kwa Mafunzo ya Ualimu wa Amali, ambapo mahitaji ni walimu 620, waliopo 62 na upungufu ni walimu 558;

(ii) Uhaba wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia; na

(iii) Ukosefu wa miundombinu stahili kama vile maabara na warsha za vitendo.

Na kwa kuwa, hali hiyo inaweza kukwamisha na kuzorotesha Elimu ya Amali nchini pamoja na utekelezaji wa mtaala na mafunzo ya amali katika Shule za Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze bajeti ya kutosha kuajiri walimu wenye sifa na weledi wa masomo ya amali kulingana na mahitaji;

(i) Serikali iwezeshe upatikanaji wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kujifunzia katika shule za amali, Serikali iboreshe vifaa na miundombinu muhimu katika shule za Serikali, ambazo zimeanza utekelezaji wa Mitaala katika Mkondo wa Amali. *(Makofi)*

(ii) Serikali iweke mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya kuandaa walimu wa masomo ya amali, ili kuwezesha wahitimu wa mafunzo hayo kusoma kozi hizo na kuajiriwa kama walimu, na ipange vyuo maalumu kwa ajili ya mafunzo ya ualimu na amali.

(iii) Kutenga vyuo maalumu kwa ajili ya mafunzo ya ualimu wa amali ili kuanzisha walimu wenye ujuzi wa kutosha katika Sekta ya Amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu shuleni:-

Kwa kuwa, uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu vya shule unatekelezwa na Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET)*, lakini utaratibu uliopo sasa, Wizara ya Fedha inapeleka fedha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambao nao wanapeleka fedha hizo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambapo inasababisha ucheleweshaji wa fedha, na inaongeza urasimu wa kiutawala na kupunguza ufanisi wa utekelezaji wa jukumu hilo;

Na kwa kuwa, ucheleweshaji wa fedha na urasimu huo unasababisha upungufu wa vitabu shuleni, hali ambayo inaathiri ubora wa elimu, inaongeza mzigo kwa walimu na wanafunzi, na inachelewesha utekelezaji wa sera za elimu nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ipeleke moja kwa moja fedha za uchapishaji wa vitabu kwa Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET)*, ili kuongeza ufanisi, kasi, na uwajibikaji katika uandaaji na usambazaji wa vitabu shuleni kwa wakati unaofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji usioridhisha wa miradi ya vyuo 64 vya *VETA*:-

Kwa kuwa, ujenzi wa vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi ni muhimu katika kukuza maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, lakini utekelezaji wake katika vyuo 64 vya *VETA* hauridhishi;

Na kwa kuwa, ucheleweshaji wa ukamilishaji miradi hii unaleta athari kwa maendeleo ya ufundi stadi nchini unasababisha usumbufu kwa wanafunzi na watumishi katika vyuo hivyo, na unachelewesha manufaa yaliyokusudiwa kwa Taifa kutokana na ujenzi wa vyuo vya veta;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa fedha za ujenzi wa vyuo hivi zinatolewa zote ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze juhudi za kuweka huduma muhimu za miundombinu kama maji, umeme, barabara, kwa wanafunzi katika maeneo yote yenye vyuo vya *VETA* vinavyoendelea kujengwa, na ichukue hatua za haraka kuhakikisha maeneo yote ya vyuo vya *VETA* ambayo hayana hati yanapatiwa hati kwa kufuata utaratibu stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kwanza, ukosefu wa vyanzo vya fedha vya uhakika, toshelevu na endelevu kwa ajili ya uwekezaji na uendeshaji wa miundombinu ya utangazaji *TBC*:-

Kwa kuwa, kukosekana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya kuongeza usikivu wa redio, ujenzi wa *studio* mpya za redio na televisheni, na watumishi wenye weledi na vipaji wanaoendana na teknolojia;

Na kwa kuwa, hali hiyo inaweza kukwamisha lengo la Serikali kuwa na chombo bora cha utangazaji chenye manufaa kwa nchi na kupunguza uwezo wa *TBC* kufikia malengo yake ya kuwa

chombo cha Taifa kinachoelimisha, kinachochochea maendeleo na kinachowakilisha wananchi wote kwa njia bora;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye mambo yafuatayo: -

(i) Kutoa fedha za kutosha kwa wakati ili kuiwezesha *TBC* kujiendesha kibiashara, kupambana na ushindani wa kibiashara;

(ii) Kuhakikisha kuwa minara ya mawasiliano kwenye maeneo yote yenye changamoto za usikivu, hasa mipakani mwa nchi na maeneo hatarishi, inajengwa ili kuhakikisha huduma za utangazaji zinawafikia wananchi wote;

(iii) Kuwezesha ushirikiano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na *TBC*, katika kuimarisha maudhui ya vipindi vya *Safari Channel*, ili kuboresha utoaji wa maudhui na kuongeza ufahamu wa watalii na maliasili ya nchi; na

(iv) Kuendelea kuajiri watumishi wenye vipaji maalumu ili kuifikia jamii kwa urahisi, na kuhakikisha chombo cha utangazaji kinakuwa na uwezo wa kutoa huduma bora zenye ubora kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa fedha kwa watumishi wa BAKITA:-

Kwa kuwa, BAKITA inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wataalamu wa Lugha ya Kiswahili wenye ujuzi wa lugha nyingine, jambo linalokwamisha juhudi za kuongeza kasi ya ukuaji wa Lugha Sanifu ya Kiswahili na kufanya kuwa Lugha ya Kimataifa katika sekta mbalimbali;

Na Kwa Kuwa, tatizo hili linachelewesha juhudi za kuhakikisha Kiswahili kinakuwa na hadhi ya Kimataifa na

kuimarisha matumizi yake katika nyanja za elimu, biashara, na utamaduni;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iwezeshe BAKITA kuajiri wataalamu wa Lugha ya Kiswahili wenye ujuzi wa lugha nyingine ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Lugha Sanifu ya Kiswahili; pia izingatie ahadi iliyotolewa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, aya ya 283(d), kuhusu kuimarishwa kwa mila, desturi, na tamaduni nzuri zinazojenga Utaifa, kwa kuiwezesha BAKITA kuongeza wigo wa kuelimisha Umma kuhusu Kiswahili na utamaduni wetu; na vile vile Serikali iwezeshe BAKITA kufanya utafiti katika nchi ambazo Kiswahili kinabidhaishwa ili kubaini fursa, manufaa, na namna ya kuongeza ushawishi wa Kiswahili Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya makusanyo ya tozo ya hakimiliki kutokuwasilishwa *COSOTA*:-

Kwa kuwa, Serikali inakutana na changamoto ya kutokutolewa kwa fedha zote za makusanyo ya tozo za hakimiliki kwa wakati, jambo linalosababisha ucheleweshaji katika utekelezaji wa malengo ya kuanzishwa kwa tozo hii;

Na kwa kuwa, athari ya changamoto hii ni kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa, na kukuza na kulinda hakimiliki, jambo linaloharibu Sekta ya Sanaa na kupunguza fursa za ajira kwa wasanii, wabunifu, na kuathiri maendeleo ya utamaduni na ubunifu nchini;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa fedha zote za makusanyo ya tozo ya hakimiliki zitatolewa kikamilifu na kwa wakati ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, na kukuza Sekta ya Sanaa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokamilika kwa ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa:-

Kwa kuwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa ni moja ya miundombinu muhimu ya michezo nchini inayotumika kwa matukio ya Kitaifa na Kimataifa, lakini unakabiliwa na changamoto za matengenezo na usimamizi endelevu;

Na kwa kuwa, uwanja huu pamoja na viwanja vingine vya michezo unahitaji matengenezo ya mara kwa mara ili kudumisha ubora wake wa Kimataifa na kuimarisha maendeleo ya Sekta ya Michezo nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inakarabati Uwanja wa Benjamin Mkapa ifikapo Aprili, 2025; Serikali iandae mkakati wa kuanzisha chombo maalumu cha usimamizi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na viwanja vingine vinavyojengwa na Serikali ili kuhakikisha vinatunzwa na vinakuwa katika ubora wa Kimataifa; Serikali iweke utaratibu wa sehemu ya makusanyo ya uwanja na kubaki kwa matumizi ya uwanja huo *(retention)* ili kurahisisha matengenezo na dharura zinazoweza kujitokeza; na Serikali iandae mkakati wa kuboresha viwanja vingine vya michezo ili kupunguza mzigo wa matumizi makubwa kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusuasua kwa ujenzi wa *hostel* na miundombinu ya Chuo cha Akademia ya Michezo Maya:-

Kwa kuwa, taarifa za Serikali zimeonesha kuwa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kinakabiliwa na changamoto ya ucheleweshaji wa fedha, jambo linalosababisha miradi kutokukamilika kwa wakati;

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha kutokukamilika kwa mradi huo kwa wakati na kutokutimia kwa azma ya Serikali ya kuendeleza michezo nchini, hivyo kuathiri maendeleo ya michezo na vijana katika maeneo husika;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa fedha zote zinazohusiana na mradi huu zipelekwe kikamilifu na kwa wakati ili kuwezesha kukamilika kwa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele yako. Aidha, nakupongeza kwa kazi kubwa unayofanya ya kuliongoza Bunge. Pia nampongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru Mawaziri katika Wizara mbili zinazosimamiwa na Kamati hii, ambao ni Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Mbunge na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Aidan Kabudi, Mbunge na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati, ambao ni Mheshimiwa Omary Juma Kipanga, Mbunge na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge na Naibu Waziri wa Habari Utamaduni, Sanaa, na Michezo, kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara hizi mbili kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati na kurahisisha utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge, kwa ushirikiano wake kwangu na Kamati. Kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ya Elimu, Utamaduni, na Michezo, kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru sana kwa michango yao mikubwa katika Kamati, na hivyo kurahisisha majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa, naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Wakurugenzi Wasaidizi, na Sekretarieti, kwa kuisaidia Kamati wakati wote wa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, na hatimaye likubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni, na Michezo, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2024 HADI JANUARI 2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka, 2024. Taarifa hii imejikita katika kuelezea shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha mwaka mmoja.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Taarifa hii imeundwa na sehemu kuu nne kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

(ii) Sehemu ya Pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

(iii) Sehemu ya tatu inatoa maoni na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi; na

(iv) Sehemu ya nne inatoa hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

## 1.3 Muundo na Majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo ni miongoni mwa Kamati kumi na moja za kisekta kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (8) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia Wizara mbili: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kujielekeza katika wigo wa shughuli za Wizara hizo, Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimebainisha mambo makuu manne ambayo ni majukumu ya Kamati hii. Mambo hayo ni:-

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara na Taasisi inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara inazozisimiamia; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati yangu imetekeleza kikamilifu wajibu wake katika kuzingatia matakwa ya Kanuni hiyo.

**1.4 Msingi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati.**

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati umejengwa katika dhana ya Kikatiba kupitia ibara ya 8 (1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inaelezea kuwa, lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi wake. Aidha, Ibara ya 63 (2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi. Katika ibara ya 96, Katiba inaelezeka Bunge kuunda Kamati mbalimbali ili kurahisisha majukumu yake ya kusimamia na kuishauri Serikali. Hivyo, basi Kamati inapotekeleza majukumu yake inafanya kwa niaba ya Bunge zima na wananchi kwa ujumla katika uhakikisha Serikali inatimiza wajibu wa kuleta ustawi wa watu wake.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati hii yamefafanuliwa kwenye Kifungu cha 6(7) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

Katika utekelezaji wa shughuli zake Kamati ilizingatia Mpango wa Tafa wa Maendeleo wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 na mapitio ya bajeti kama ilivyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha shughuli za Kamati zinatekelezwa kikamilifu, kwa ufanisi na kwa mujibu wa Katiba, huku tukizingatia masharti ya Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 na kuhakikisha ustawi wa wananchi, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupokea na Kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara inazozisimamia pamoja na Idara, Taasisi na Mamlaka mbalimbali zilizo chini ya Wizara hizo;

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka 2024/2025;

(iii) Kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara inazozisimamia;

(iv) Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025 za Wizara inazozisimamia;

(v) Kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Desemba, 2024);

(vi) Kufuatilia Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Mwezi Februari, 2024.

### 1.5 Njia na mbinu zilizotumika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia mbalimbali Ili kuhakikisha inapata wigo mpana wa upataji taarifa na ufanyaji wa tathmini na kukidhi matarajio yaliyokusudiwa kutokana na Ilani ya uchaguzi kama ifuatavyo: -

(i) Vikao vya kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kujua utendaji wao, mafanikio, changamoto na namna ya kutatua changamoto hizo;

(ii) Ziara za ukaguzi wa maeneo mbalimbali kwa lengo la kujionea utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake na kuzilinganisha na taarifa iliyochambuliwa na Kamati;

(iii) Kufanya uchambuzi wa Taarifa za Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Kushiriki mafunzo, Semina na Warsha mbalimbali kwa lengo kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taassi, Asasi za Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Maelezo ya Shughuli

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari,2025 Kamati ya Elimu,Utamaduni na Michezo ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika kifungu 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Miongoni mwa Shughuli zilizo tekelezwa na Kamati ni pamoja na:-

(i) Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio;

(ii) Kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Kupokea, Kuchambua na Kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai– Disemba, 2024);

(v) Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Taasisis zinazozisimamia.

**2.1.1 Kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa za utekelezaji wa Mazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kuanzia Februari 2024 hadi Januari, 2025. Lengo la kupokea taarifa hizi lilikuwa ni kufuatilia iwapo Serikali imezingatia Maazimio ya Bunge na Kama imezingatia ni kwa kiasi gani yametekelezwa katika kuleta ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa za Serikali umeonesha kuwa Bunge lilipitisha maazimio kumi na moja (11) kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Maazimio nane (8) utekelezaji wake unaridhisha na unaendelea, maazimio matatu (3) utekekelezaji wake si wa kuridhisha. Maazimio hayo ni pamoja na upungufu wa walimu nchini, uchakavu wa miundombinu na upungufu wa wahadhiri Chuo Kikuu cha Dodoma UDOM na ujenzi wa Vyuo vya mafunzo ya ufundi usioendana na mahitaji ya wakufunzi na vitendea kazi. Hata hivyo, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa maazimio.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo maazimio kumii na tatu (13) yaliyopitishwa na Bunge yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Pamoja na utekelezaji wa maazimio hayo kuendelea, Kamati imebaini kuwa, yapo baadhi ya maazimio utekelezaji wake unahitaji kuwekewa

nguvu zaidi, Maazimio hayo ni pamoja na Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha Viwanja vya Arusha na Dodoma, Fedha kwa ajili ya ukarabati na uendelezaji wa miundombinu ya Uwanja wa Benjamin Mkapa na Serikali kuweka utaratibu wa sehemu ya makusanyo kubaki kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa (Retention).

**Mheshimiwa Spika,** Maazimio yaliyofikiwa na Bunge yalilenga kuongeza tija katika shughuli za Wizara hizi ili kuweza kufikiwa kwa ustawi wa wananchi.

### 2.1.2 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilitekeleza takwa la kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo iliyotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96). Lengo la ziara hizo ni kujiridhisha juu ya tija inayopatilkana katika miradi na program zilizotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kutokana na ziara hizo Kamati iliweza kuwianisha taarifa zinazotolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi iliyopo kwenye maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** ziara hizo zilifanyika katika Mikoa miwili ambayo ni Arusha na Dar salaam kuanzia tarehe 11 – 20 Machi, 2024. Taarifa za kina kuhusu yaliyobainika katika ziara hizo pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa katika Taarifa za Bajeti mnamo mwezi Aprili na Juni, 2024.

### 2.1.3 Kupokea, Kuchambua na Kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kamati ilitekeleza jukumu la kuchambua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maoni na Ushauri na mapendekezo ya Kamati na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kwa Wizara ya Elimu,

Sayansi na Teknolojia (Fungu 46), Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96).

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za kina za Uchambuzi wa Bajeti za Wizara hizo na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano (15) wa uliomalizika Mwezi Juni, 2024.

**2.1.4 Kupokea na Kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2024)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa kupokea, kuchambua na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (julai – Disemba, 2024) za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46), Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96). Lengo la kufanya hivyo ilikuwa ni kuona mwenendo wa ukusanyaji wa fedha ili kuweza kuishauri Serikali ipasavyo hasa ikizingatiwa kuwa inategemewa kufika Disemba, 2024 ukusanyaji wa maduhuri na upatikanaji wa fedha uwe umefikia angalau asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

(a) **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji**

Katika Mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 677,299,142,074.83** hadi kufikia Disemba, 2024 kiasi cha **Shilingi 240,925,158,213.72** kimekusanywa sawa na **asilimia 36** ya lengo. Aidha, kwa upande wa Bajeti ya Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha **Shilingi 1,965,330,380,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2024 Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 842,096,352,364.70** sawa na asilimia **43** ya fedha zilizotengwa. Aidha, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **shilingi 545,729,298,548.72.** sawa na asilimia **41** ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebaini

kuwa mwenendo wa upatikaji wa fedha si wa kuridhisha kwani upo chini ya asilimia 50**.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) iliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 2,882,154,000.00** ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2024, Tume ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha **Shilingi 1,409,540,390.72** sawa na asilimia **49.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa upatikaji wa fedha ni wa kuridhisha kwa upande wa Tume ya ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18)

(b) **Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 8,001,600,000.** hadi kufikia Disemba, 2024 kiasi cha **Shilingi 3,478,400,192** kimekusanywa sawa na **asilimia 43.5** ya lengo. Aidha, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **shilingi 128,710,495,791.47** sawa na **asilimia 49.4** ya lengo, ambazo ni fedha za ndani. Wizara haikupangiwa fedha za nje. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa upatikaji wa fedha unaridhisha kwani upo kwa asilimia **49.4.**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Waziri wa Fedha aliahidi kutoa fedha za kutekeleza miradi ya Maendeleo kwa Wizara hii. Kamati imebaini kuwa, baadhi ya miradi ya maendeleo haijatolewa fedha na Serikali, hata hivyo Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inaendelea kufanyia kazi suala hili kwa kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili fedha hizo zitolewe kwa wakati. Ni Rai ya Kamati kuwa, Serikali itoe fedha katika Wizara hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.1.5 Kufuatilia Utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia matakwa ya Nyongeza ya 7(1)(d) Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya

Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ifuatavyo: -

***Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia***

**Mheshimiwa Spika**, katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati ilipokea, kuchambua na Kujadili taarifa za utekelezaji kama yafuatayo: -

**(i) Hali ya utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Mwaka wa masomo 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilianzishwa mwaka 2004 kupitia Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Sura Na 178 na ilianza rasmi kazi zake za kiutendaji mwezi Julai, 2005 kwa lengo la kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji na kukusanya mikopo iliyotolewa na Serikali tangu mwaka 1994/1995. Hata hivyo kwa sasa Bodi imeongezewa majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya kati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliarifiwa kuwa kwa Mwaka 2023/2024 kiasi cha **Shilingi Bilioni 743.3** kimekopeshwa kwa wanafunzi. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita 2021/2022 hadi 2023/2024 Serikali imeendelea kuongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu kutoka **Shilingi Bilioni 570** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi Bilioni 738,7** mwaka 2023/2024. Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi inazofanya za kuendelea kuwawezesha kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wa Elimu ya juu wanaopata mkopo waweze kupata elimu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo Kamati ilibaini mwenendo wa utolewaji wa Mikopo ni wa kuridhisha, Kuongezeka kwa bajeti ya fedha za mikopo kumewezesha kuongezeka kwa wanufaika wa mikopo ya ruzuku kutoka wanafunzi 177,615 hadi 224,056 hadi kufikia Juni 31 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 26**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji ili kujua hali ya upangaji wa mikopo kwa 2023/2024. Kamati ilielezwa kuwa, jumla ya wanafunzi 224,056 walipangiwa mikopo yenye jumla ya thamani ya **Shilingi Bilioni 743.2** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 13** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka 2022/2023 wakiwemo wanafunzi 79,133 wa mwaka wa kwanza na ongezeko la asilimia 8 ukilinganisha na waliopangiwa mwaka 2022/2023 na wanafunzi wanaondelea 144,923 sawa na **asilimia 12**.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa upatikanaji wa Ruzuku (SAMIA Scholarship) kwa 2023/2024 jumla ya wanafunzi 1,228 walipangiwa ruzuku zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 6.43.** Aidha, wanafunzi 918 waliopangiwa ruzuku ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 310 wanaoendelea. Hata hivyo, idadi ya wanufaika wanaoendelea na masomo imeshuka kutoka 636 waliopangiwa mwaka 2022/2023 hadi 310 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; kushindwa kukidhi kigezo cha wastani wa GPA ya 3.8

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini pia kuwepo kwa changamoto zingine zinazoikabili Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu zikiwemo: -

(a) Bodi kutegemea chanzo kimoja cha mapato ambacho ni ruzuku kutoka Serikali kuu tu;

(b) Ongezeko kubwa la wahitaji wa mikopo ukilinganisha na uwezo wa Bodi ya Mikopo;

(c) Kutokupata marejesho ya mikopo kwa walionufaika na wanaoweza kurejesha;

(d) Bodi kutokuwa na mamlaka ya kutumia fedha zinazotokana na marejesho ya Mikopo kutoka wa wadaiwa;

(e) Kutokuwepo kwa namba za NIDA kwa wanafunzi kuanzia kidato cha nne na cha sita ambapo zitasaidia kuunganishwa na mifumo ya Bodi ya Mikopo ili kuongeza urejeshwaji wa mikopo.

**(ii) Utekelezaji wa utoaji wa Mikopo katika Vyuo vya Kati kwa mwaka wa masomo 2023/2024;**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa lengo la kuanzishwa Mikopo katika Vyuo vya Kati ni kuwezesha kupata wataalamu na nguvu kazi ya taifa hususani katika soko la ajira la ndani na nje ya nchi na pia kupunguza tatizo la ajira kwa watu kujiari wenyewe.
**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2023/2024, Serikali ilipanga kutumia kiasi **Shilingi Bilioni 48** kwa ajili ya mikopo ya elimu ya wanafunzi wapatao 8,000 wanasoma kozi zenye uhitaji mkubwa. Aidha, hadi kufikia Juni, 2024 jumla ya wanafunzi 2,714 sawa na asilimia 34 ya lengo la stashahada walipangiwa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 7.4** ikijumuisha wanafunzi 2,538 wa mwaka wa kwanza na 176 wanaoendelea na masomo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mijadala ya Kamati kuhusu utekelezaji wa utoaji wa mikopo katika vyuo vya Kati kwa mwaka wa masomo 2023/2024, Kamati ilielezwa mwelekeo wa utoaji wa Mikopo katika Vyuo vya Kati kwa mwaka wa masomo 2024/2025 ambapo, Serikali imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 37.3** kwa ajili ya mikopo ya elimu ya wanafunzi wapya wapatao 7,000 watakaopata udahili na kusajiliwa katika kozi zenye uhitaji mkubwa zilizobainishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa utoaji mikopo ya elimu kwa wanafunzi mwaka 1994/1995, Serikali imeshatoa jumla ya **Shilingi Trilioni 7.2** ambazo zimewanufaisha wanafunzi 754,000. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, **Shilingi Trilioni 2.1** zimeiva (tayari kwa makusanyo) kutoka kwa wanufaika 448,824. Hata hivyo, Kati ya wanufaika 448,824, wanaolipa ni 226,292. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2023 wadaiwa wamerejesha kiasi cha **Shilingi Trilioni 1.34** sawa na **asilimia 64** ya **Shilingi Trilioni 2.1** zilizoiva.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada hizo Kamati ilielezwa kuwa, mwenendo wa urejeshaji katika kipindi cha miaka miwili iliyopita 2022/2023 – 2023/2024 umeendelea kuwa imara kutokana na

kuimarishwa jitihada za kukusanya mikopo iliyoiva kwa kuongeza kasi ya kuwasaka/kuwatafuta (tracing) wadaiwa sugu. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2019/2020 – 2023/2024).

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha jitihada za kuwabaini wanufaika waliopo kwenye ajira ya sekta rasmi na wale ambao wapo kwenye sekta isiyo rasmi. Kamati ilielezwa kuwa, jitihada zimefanikisha kuongeza makusanyo kutoka **Shilingi Bilioni 169.8** mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi Bilioni 177.6** mwaka 2023/2024 ni ongezeko la takiriban **Shilingi Bilioni 8** ambalo ni sawa na **asilimia 5.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Bodi, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zikiwemo:-

(a) Wanufaika waliopo Sekta Isiyo rasmi kutojitokeza kwa hiari kurejesha mikopo ;

(b) Baadhi ya Waajiri kutowasilisha makato sahihi na kwa wakati;

(c) Wanufaika kutokuwa na kipato cha uhakika ili kurejesha mikopo kila mwezi kama inavyotarajiwa;

(d) Mifumo ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutounganishwa na baadhi ya wadau muhimu kama NIDA na mifumo mingine ya kisekta kupitia Wizara ya ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; na

(e) Kukosekana kwa mfumo mmoja madhubuti wa utambuzi wa Kitaifa

**(iii) Hali ya Udahili wa Wanafunzi wa Vyuo vya Kati kwa mwaka wa masomo 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia taarifa hii Kamati ilielezwa kwamba Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Baraza

Sura ya 129 na marekebisho Madogo ya Mwaka 2021 kwa lengo la kusimamia na kuratibu taaluma zitolewazo na taasisi na Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi inajumuisha fani mbalimbali zikiwemo ufugaji, ukulima, uvuvi, usafirishaji, uhandisi, uganga, uuguzi, uhasibu, ununuzi na ugavi, biashara, ukutubi, uandishi wa habari, uanasheria, ulinzi na ukarimu. Aidha, Kamati ilitaarifiwa kuwa, moja ya jukumu la Baraza ni kuratibu udahili wa wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao mbalimbali vilivyofanyika baina ya Kamati na Serikali, Kamati ilielezwa kwamba malengo ya Baraza kwa mwaka wa masomo 2024/2025 ni kudahili jumla ya wanafunzi 263,000; ambapo wanafunzi wa Elimu ya Ufundi (TET) ni 180,000; na Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) ni 80,000.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Baraza lilipanga kuratibu udahili wa wanafunzi 250,000. Hadi kufikia Juni 2024, Baraza limeratibu na kuhakiki udahili wa Wanafunzi 206,617, wanaume ni 106,887 sawa na asilimia **51.7** na wanawake 99,730 sawa na asilimia **48.3** kwa ngazi ya Astashahada ya Awali (Basic); Astashahada na Stashahada katika fani za Sayansi na Teknolojia Shirikishi wanafunzi 27,140 wanaume 17,906 na Wanawake 9,23.

**Mheshimiwa Spika,** katika fani ya Afya na Sayansi Shirikishi jumla ya wanafunzi 63,366 ambapo wanaume ni 31,683 na wanawake 31,683, fani ya Biashara, Utalii na Mipango wanafunzi jumla ya wanafunziu 80,751 ambapo wanaume 37,600 ni wanawake 43,151, Shahada ya Awali wanafunzi 35,360 idadi ya wanaume 19,698 na Wanawake 15,662. Baraza limepata ongezeko la udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 171,581 mwaka wa masomo 2022/2023 hadi 206,617 mwaka wa masomo 2023/2024 sawa na **asilimia 20.4**. Aidha, udahili wa wanafunzi wa kike umeongezeka kwa **asilimia 6.5.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali la kuwa na ongezeko la udahili, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zinazoikabili NACTVET kama wadau wengi kushindwa kumudu gharama za kozi zitolewazo katika vyuo vya kati, kubadilika kwa vigezo vya udahili bila kufuata taratibu na kuzingatia hali halisi ya kujifunza kunaathiri idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa.

**(iv) Program ya Lipa Kulingana na Matokeo (Edecation Programme for Result (EP4R)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa lengo la kuanzishwa program hii ni kuimarisha matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya Elimu Awali, Msingi na Sekondari nchini. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa, programu hii imetoka na Serikali kupata fedha baada ya kutekeleza afua zenye kukidhi vigezo vilivyokubalika kati yake na Wafadhili.

Hata hivyo fedha zinazopatikana baada ya kushinda vigezo hivyo hutumika kutekeleza afua mbalimbali katika sekta ya elimu ikiwemo ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na ofisi za udhibiti ubora wa Shule na kuwezesha utendaji kazi katika taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** programu hii inafadhiliwa na Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa Sweeden- *Swedish International Development Cooperation Agency* (Sida); *Korean International Cooperation Agency (KOICA);* Ushirika wa Maendeleo ya Elimu Duniani - *Global Partnership for Education* (GPE) na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza *-The United Kingdom Foreign and Commonwealth Development Office* (FCDO) kupitia Programu ya Shule Bora ambao wanatoa usaidizi wa kitaalam (Technical Assistance).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba program hii inatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2026/2027. Thamani ya mradi ni dola za

kimarekani **Milioni 126.02** (Shilingi Bilioni 327.65) ambapo Sida – SEK **Milioni 750** (USD 69.22); KOICA – Dola za Kimarekani **Milioni 2**; GPE – Dola za Kimarekani **Milioni 54.8.**

Tangu kuanza kwa utekelezaji wa awamu ya pili ya programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023, Serikali imepokea jumla ya dola za Kimarekani **Milioni 33.75** sawa na **Shilingi Bilioni 91** ili kutekeleza viashiria vya programu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia program ya EPforR imetumia jumla ya **Shilingi 87,882,860,138.29** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu pamoja na kazi nyigine. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwepo kwa changamoto nyingine zinazoikabili programu hii kama baadhi ya shule kutokukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa wakati kutokana na ufinyu wa bajeti na kutozingatia miongozo na taratibu za ujenzi.

### (v) Mpango wa Elimu Changamani kwa vijana walio nje ya shule (IPOSA)

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya IPOSA (*Integrated Programme for Out-of-School Adolescents*) ni jitihada ya kipekee iliyofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, inayolenga kutoa fursa ya elimu na mafunzo changamani katika maeneo ya kisomo, ujasiriamali, stadi za maisha na ufundi wa awali kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule nchini. Programu hii imeandaliwa kuwawezesha vijana kupata stadi za kazi na maarifa yatakayowasaidia kujitegemea na kuchangia katika uchumi wa nchi na hivyo kupunguza makundi ya vijana hatarishi mitaani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kama nguzo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, IPOSA inashughulikia mapungufu ya elimu kwa vijana waliokosa fursa za elimu ya msingi na sekondari, huku ikitoa fursa za mafunzo kupitia walimu mahiri katika vituo vya shule za msingi na ufundi yaani, *Post-*

*Primary Technical Centres* (PPTCs). Utekelezaji wa program hii umefanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza imetekelezwa katika Mikoa 10 ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Shinyanga, Tabora, Kigoma; chini ya ufadhili wa UNICEF, PLAN International na CARE International. Awamu ya pili imetekelezwa katika Mikoa 5, Mikoa hiyo ni Pwani, Tanga, Simiyu, Manyara na Singida, ikijumuisha ufadhili wa KOICA tangu 2024. Hivyo basi, kufanya jumla ya mikoa 15 ambayo IPOSA inatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Chimbuko la programu hii ni utafiti uliofanyika mwaka 2015 kuhusu wanafunzi walio nje ya shule (*Out of School Children*). Utafiti huu uliofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ulibainisha kuwa zaidi ya watoto **milioni 3.5** wapo nje ya shule. Progamu hii ina lengo hasa la kupunguza idadi ya vijana wasiokuwa na stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa kuwapatia walengwa hao mafunzo yaliyojikita katika maeneo makuu manne ambayo ni Kisomo (*Literacy skills*), Ufundi wa awali (*pre-vocational skills)*, Ujasiriamali (*entrepreneurship*), na Stadi za maisha (*life skills*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu hii ya IPOSA, jumla ya dola za Kimarekani Milioni 2.5 (Shilingi bilioni 5,750) zimetumika, katika maeneo ya uanzishaji wa vituo, ununuzi wa vifaa, mafunzo ya wawezeshaji na kuendesha programu za mafunzo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado utekelezaji wa program hii unakumbana na changamoto zifuataizo:-

(a) Upungufu wa rasilimali fedha ambapo kwa kiasi kikubwa inasababisha program kutokuwafikia walengwa wengi zaidi;

(b) Upungufu wa wawezeshaji wenye uwezo na weledi stahiki;

(c) Changamoto za ufundishaji kutozingatia masuala mtambuka kama Jinsia;

(d) Ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia vya kisasa; na

(e) Vikwazo vya kiutamaduni, mila na kijamii huchangia kukwamisha ushiriki wa wasichana katika kujiendeleza kupitia programu hii.

**(vi) Utekelezaji wa Mtaala mpya katika programu ya shule za Amali.**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupokea taarifa hii Kamati ilitaarifiwa kwamba Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) inaendelea na utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023 pamoja na Mitaala ya elimu ngazi ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu. Maboresho ya Sera na Mitaala yamelenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, mwelekeo, maadili na ujuzi unaoakisi mahitaji halisi katika taifa na kuweza kushindana na kushiriki kikamilifu katika soko la ajira duniani. Hivyo, wahitimu wataweza kujitegemea na kutumia vema fursa zinazopatikana nchini hususani kumudu maisha yao ya kila siku, kujiajiri au kuajiriwa pale wanapohitimu mafunzo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023 utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ulianza mwezi Januari, 2024 kwa Darasa la Awali, la Kwanza na la Tatu kwa Elimu ya Msingi. Kwa upande wa Elimu ya Sekondari, utekelezaji ulianza kwa Kidato cha Kwanza Mkondo wa Amali.

**Mheshimiwa Spika,** Elimu ya Sekondari ya Chini imegawanyika katika Mikondo miwili ambayo ni Mkondo wa Elimu ya Jumla na Mkondo wa Elimu ya Amali. Mara baada ya wanafunzi kuhitimu Darasa la Sita watafanya Upimaji wa Kitaifa, na watapaswa kuchagua kujiunga kusoma Elimu ya Sekondari ya Jumla au ya

Amali watakapoingia Kidato cha kwanza. Mwanafunzi atachagua mkondo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake ya maisha.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mkondo wa Elimu ya Amali kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza ulianza kutekelezwa mwezi Januari, 2024. Utekelezaji huu ulianza kwa kuzitambua shule 101 zilizoonesha utayari wa kutoa mafunzo ya amali ambapo shule 96 za Sekondari zilibainika na kukidhi vigezo na kusajiliwa na NACTVET kufundisha Mkondo wa Elimu ya Amali. Kati ya shule 96 za Sekondari za Mkondo wa Elimu ya Amali zilizobainika, shule 39 ndizo zilizoanza na zinaendelea kutoa mafunzo ya amali. Shule 57 zilizoshindwa kuanza kutoa mafunzo ya amali kutokana na kutokukamilisha maandalizi ya muhimu hivyo, zilitegemewa kuanza kutoa mafunzo hayo Januari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa, licha ya dhamira njema ya Serikali ya kufanya maboresho ya Sera na Mitaala, bado utekelezaji wake unakumbana na changamoto zifuatazo:-

(a) Upungufu wa walimu wa kufundisha masomo ya Fani za Mkondo wa Amali ambapo Mahitaji ni walimu **620,** Waliopo **62** na Upungufu **558.** Aidha, Walimu wa Somo la lazima la Elimu ya Biashara Mahitaji **5,014,** Waliopo **939** na Upungufu ni **4,075;**

(b) Upungufu wa miundombinu ya Fani husika kama vile karakana, mashamba darasa na maabara kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo;

(c) Uelewa mdogo wa wadau wa elimu kuhusu umuhimu wa mafunzo ya Mkondo wa Elimu ya Amali kama vile wazazi, walimu, wanafunzi pamoja na wadau wengine; na

(d) Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa baadhi ya fani za Mkondo wa Elimu ya Amali.

### (vii) Ujenzi wa Vyuo 64 vya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA)

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza azma ya kujenga Vyuo 64 vya Ufundi Stadi katika Wilaya ambazo hazina Vyuo hivyo na Chuo kimoja cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Songwe. Mradi huu unatokana na agizo la Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akizindua chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera Oktoba, 2022. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kutoa fedha jumla ya **Shilingi. Billioni 100** kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo hivyo katika Wilaya ambazo zilikuwa hazina Vyuo vya Ufundi Stadi pamoja na Mkoa wa Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Ujenzi huu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatumia utaratibu wa "Force Account" ambapo inatumia Taasisi zilizo chini yake. Washauri Elekezi ambao ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (MUST), Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Chuo Kikuu Ardhi (ARU) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na utekelezaji unafanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara zilizopo katika Wilaya na Mkoa husika ambazo ni Vyuo vya Ualimu 5, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 23 na Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule 36 na VETA moja (1).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, katika bajeti ya mwaka 2023/2024 Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitenga kiasi cha **Shilingi Bilioni 100** ambazo zilipangwa kutolewa na Wizara ya Fedha katika awamu tatu kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo 64 vya wilaya na kimoja cha mkoa wa Songwe. Hadi kufikia tarehe 1 Oktoba, 2024 Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ilipokea kiasi cha **Shilingi 54,000,000,000/=** kutoka Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** katika mijadala ya Kamati kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu, Kamati haijaridhishwa na kasi ya utekelezaji wake kwani hadi wakati wa taarifa hii inawasilishwa

katika Kamati, VETA inaendelea na kazi ya utekelezaji wa ujenzi kwa **asilimia 35 tu,** kazi hizo ni pamoja na ujenzi wa kuta za boma na ufungaji wa hanam (lintel) katika majengo 6 pamoja na ukamilishaji wa misingi katika karakana 3 za kila Chuo cha wilaya unaendelea, ujenzi wa kuta za boma ufungaji wa linta katika majengo 17 na ukamilishaji wa Msingi katika karakana 7 kwa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Songwe na nguzo za chuma kwa ajili ya karakana zimepelekwa katika Vyuo ishirini na tatu (23) kutokana na upatikanaji wa fedha iliyokuwepo na zoezi la ufungaji wa vyuma unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa ikiwemo kukosekana kwa huduma muhimu (maji, umeme na barabara) katika baadhi ya maeneo ya ujenzi, ucheleweshaji fedha kutoka Wizara ya Fedha na ongezeko la bei ya malighafi za ujenzi.

**(viii) Utekelezaji wa Tahasusi mpya kwa kidato cha tano;na namna Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSB) na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) zilivyoshirikishwa katika uboreshaji wa tahasusi.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa iliyowaslishwa mbele ya Kamati ilieleza kwamba, moja ya hatua muhimu katika utekelezaji wa Sera na Mitaala iliyoboreshwa ni kuanzishwa kwa tahasusi mpya za kidato cha tano. Tahasusi hizi zimeundwa kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira, maendeleo ya teknolojia na malengo ya maendeleo endelevu ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inalenga kuwajengea wanafunzi msingi imara wa kuchagua fani zitakazowafanya kuwa raia wazalendo na wenye mchango katika maendeleo ya nchi. Aidha, kupitia tahasusi hizi, wanafunzi watapata fursa ya kujifunza kwa kina katika maeneo wanayoyapenda, hivyo kuongeza uelewa wao na kujiamini pamoja na ongezeko la vijana wenye ujuzi na maarifa ya kutosha ya kuendesha sekta mbalimbali za uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** ilielezwa kwamba, uandaaji wa tahasusi umezingatia malengo makuu ya elimu ya nchi, malengo ya elimu ya Sekondari Kidato cha 5-6, mahitaji ya jamii, falsafa ya elimu ya kujitegemea, mapendekezo ya wadau wa elimu yaliyotolewa wakati wa uboreshaji wa mitaala mwaka 2023, matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023, mahitaji halisi ya taifa, maendeleo ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya ulimwengu wa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** mchakato wa kuandaa Tahasusi ulifanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa Elimu pamoja na Wizara na Taasisi zinazoshughulika na Elimu kama vile OR-TAMISEMI, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Mamlaka ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA). Aidha, Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (TCU) na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu walishiriki kupitia mikutano ya Wadau wa Elimu ya Juu. Aidha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepanga kutekeleza tahasusi mpya kuanzia Julai 2025 badala ya Julai 2024 ili kutoa fursa ya kufanya maandalizi muhimu hususani, uandaaji na usambazaji wa vitabu vya kiada na kutoa mafunzo kabilishi kwa walimu. Vilevile, kuzipa shule muda wa kutosha kufanya maandalizi ya walimu pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kwamba, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imekamilisha maandalizi ya vitabu vya kiada kwa Kidato cha Tano na Viongozi vya mwalimu ambapo jumla ya nakala 158,701 ya vitabu na 33,000 ya viongozi vya mwalimu vimekwishakuchapwa. Vitabu hivi vinatarajiwa kusambazwa mwezi wa pili mwaka 2025. Mafunzo kwa walimu wa Kidato cha 5-6, hadi kufikia Julai, 2024. Taasisi ya Elimu Tanzania ilitoa mafunzo kwa walimu 2,324 ambapo mchanganuo wake ulikuwa kama ifuatavyo: Mkoa wa Lindi walimu 185, Dar es Salaam 758, Shinyanga 207, Mwanza 645, Geita 316 na Pwani wilaya ya Bagamoyo waliwezeshwa walimu 213.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na juhudi zinazofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa juhudi za

kuboresha Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 na kupata Toleo la Mwaka 2023 pamoja na Mitaala ya elimu kwa ngazi zote. Aidha, maboresho haya katika Tahasusi yanalenga kutoa elimu itakayomwezesha mhitimu kumudu maisha yake ya kila siku kwa kuwa mtaala umezingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea.

**(ix) Kushughulikia malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada za Afya katika vyuo vya kati**

**Mheshimiwa Spika,** Itakumbukwa kuwa ulitoa maelekezo kwa Kamati mbili za Kudumu za Bunge ambazo ni Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo kufanya kikao cha pamoja ili kushughulikia malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada za Afya katika vyuo vya kati.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa maelekezo hayo ulitokana na maombi ya Umoja wa Vyuo Binafsi vya Afya vya Kati Tanzania, *[Association of Private Health Colleges in Tanzania-(APHECOT)]* yaliyowasilishwa kwako. Umoja huo kwa mara ya kwanza uliomba kibali chako ili viongozi wake wakutane na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Kwa busara zako, uliridhia Kamati iliyolengwa ikutane na *APHECOT* ambapo siku ya Ijumaa, tarehe 17 Mei, 2024 Kamati ilikutana na kuanza kulifanyia kazi suala la malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili katika vyuo vya kati vya Afya.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao hicho, *APHECOT* waliwasilisha malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada za Afya katika vyuo vya kati kwa kada ya Fiziotherapia, Famasia na Uuguzi na Ukunga ambavyo vilitarajiwa kuanza kutumika katika Mwaka wa masomo 2024/2025. Kwa kuzingatia wigo wa wizara zinazohusika katika suala hilo, Kamati iliomba ridhaa yako ili kupata nafasi ya kukutana na Wizara ya Afya kwa pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kupata mtazamo wa Serikali kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mamlaka yako, ulielekeza kifanyike kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI

inayosimamia shughuli za Wizara ya Afya pamoja na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo inayosimamia shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kushughulikia malalamiko ya *APHECOT*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati mbili ulizozielekeza kukutana zilifanya kikao cha pamoja siku ya Jumatano, tarehe 5 Juni, 2024, Alhamis, tarehe 6 Juni, 2024 na Jumanne, tarehe 11 Juni, 2024. Katika vikao hivyo yaliibuka maazimio matatu ambayo yalitolewa kama ushauri kwa Serikali. Ushauri huo ni: -

(i) Kwa kuwa, vigezi vipya havikuonekana kama ni tatizo isipokuwa tatizo lilikuwa ni wadau kutokushirikishwa ipasavyo, hivyo basi, wadau washirikishwe na wapewe elimu ya kutosha kuhusu vigezo vipya vya udahili kabla ya kuanza kutumika katika Mwaka mpya wa masomo 2025/2026;

(ii) Kwa kuwa, moja ya sababu ya mkanganyiko ni NACTIVET kukasimu majukumu yake Wizara ya Afya, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) litekeleze majukumu lililopewa kwa mujibu wa sheria sura namba 129 ikiwemo majukumu lililoyakasimu kwa Wizara ya Afya; na

(iii) Kwa kuwa, imebainika kwamba, Wizara ya Afya imeshindwa kusimamia kwa karibu vyuo vilivyo chini yake, Wizara ianzishe chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya kati vya afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya ili kuwezesha uendeshaji bora wa mafunzo ya fani za kada ya afya.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa Taarifa ya utekelezaji wa ushauri uliotolewa kuhusu malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada za Afya katika vyuo vya kati. Tarehe 18 Oktoba, 2024 Serikali iliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati ikiwa ni sehemu ya maagizo yaliyotolewa ili yawasilishwe katika vikao vya Kamati vya mwezi Oktoba, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hiyo ya Serikali iligusia masuala yote yaliyoshauriwa na Kamati na kuonesha namna utekelezaji unavyoendelea. Utekelezaji huo ni kama ifuatavyo: -

(i) Uelimishaji na ushirikishwaji wa wadau kuhusu vigezo vipya vya udahili kabla ya Mwaka mpya wa masomo 2025/2026, Serikali kupitia Wizara ya Afya ilieleza kuwa itaandaa vikao vya wadau wa mitaala ya mafunzo kwa kila mtaala ili kupata maoni yao yatakayosaidia kufanya maboresho ya mitaala hiyo. Kwa kipindi cha Disemba, 2024 hadi Mei, 2025 wadau wataelimishwa kuhusu uandaaji wa mitaala na taratibu za kufuata iwapo mdau hajaridhika na maboresho yaliyofanyika kwenye mitaala. Aidha, Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Septemba, 2025 mitaala iliyohuishwa itasambazwa ili kuanza kutumika kwenye Mwaka wa masomo 2025/2026 utakaoanza mwezi Oktoba, 2025;

(ii) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) litekeleze majukumu lililopewa kwa mujibu wa sheria sura namba 129 ikiwemo majukumu lililoyakasimu kwa Wizara ya Afya, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilieleza kuwa jukumu la kuratibu utahini na mitihani linalotekelezwa na Wizara ya Afya, litekelezwe na taasisi husika za mafunzo na Wizara ya Afya imeelekezwa kuanzisha mchakato wa kuzijengea uwezo taasisi za mafunzo zilizo chini yake ili ziweze kuendesha mitihani yake zenyewe; na

(iii) Uanzishwaji wa chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya kati vya Afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Serikali kupitia Wizara ya Afya ilieleza kuwa imeanza mchakato wa kuanzisha chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya afya ili kuimarisha usimamizi wa mafunzo kwenye vyuo hivyo. Hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni pamoja na kuandaa rasimu ya andiko dhana la uanzishwaji wa chombo cha usimamizi wa mafunzo kwenye vyuo vya Afya vya

Serikali na kuundwa kamati maalumu ya kukusanya maoni yatakayowezesha uanzishwaji wa chombo hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali izingatie na kutekeleza ushauri uliotolewa kwa ajili ya kuboresha suala zima la elimu ya kada za Afya katika vyuo vya kati, kwani vyuo hivyo vimekua ni msaada mkubwa katika kuzalisha wataalam mbalimbali ambao husaidia kutoa huduma bora za Afya kwa wananchi katika ngazi zote za huduma za Afya nchini.

**(x) Hali ya Upatikanaji wa Vitabu vya kufundishia na kujifunzia**

**Mheshimiwa Spika**, ifahamike kwamba utekelezaji wenye ufanisi wa Mitaala unategemea upatikanaji wa nyenzo, vifaa na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia kulingana na mahitaji ya masomo na programu katika ngazi mbalimbali za elimu. Nyenzo hizo ni pamoja na vitabu vya Kiada na Ziada, kemikali za maabara, mitambo na karakana.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala iliyoboreshwa inasisitiza matumizi sahihi ya vitabu kwani ni nyenzo ya msingi katika kufanikisha maendeleo ya elimu. Aidha, vitabu vina nafasi kubwa katika kuhakikisha kuwa wanafunzi na walimu wanapata maarifa sahihi, ujuzi, na msaada wa kitaaluma unaohitajika kwa maendeleo yao ya kielimu na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba katika kipindi cha nusu mwaka 2024/2025, Taasisi ya Elimu (TET) ilipokea kiasi cha **Shilingi. 7,185,262,172** kwa ajili ya uandaaji wa vitabu vya Kiada na uidhinishaji wa vitabu vya ziada pamoja na kuchapa na kusambaza vitabu vya Kiada kwa ngazi ya Elimu ya Ualimu. Aidha, jumla ya vitabu **285** viliandaliwa vya Kiada na Kiongozi cha Mwalimu kwa Ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa II na IV katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kwa wanafunzi walio na wasio na mahitaji maalumu .

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imefanikiwa kuchapa na inasambaza jumla ya nakala **12,047,829** za Vitabu vya Kiada na Viongozi vya Mwalimu vya Darasa la Pili na la Nne vya Mtaala ulioboreshwa wa Mwaka 2023. Vitabu hivi vimeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, maandishi ya kawaida, yaliyokuzwa na Breli kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Jumla ya nakala **8,792,320** kati ya **9,902,102** sawa na asilimia **89** ya vitabu vya Elimu ya Sekondari vimepokelewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa pamoja na mafanikio ya Serikali ya kuhakikisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinaandaliwa, kuchapwa na kusambazwa kwa wakati, bado utekelezaji wake unakumbana na changamoto zifuatazo: -

(a) Kukosekana kwa mtiririko wa uhakika wa upatikanaji wa fedha za uchapaji na usambazaji wa vitabu;

(b) Ongezeko la wanafunzi linalopelekea kuchapa na kusambaza vitabu kwa uwiano wa kitabu kimoja wanafunzi watatu mpaka watano (1:3- 1:5); na

(c) Ukosefu wa miundombinu na mashine za kisasa nchini unaopelekea wazabuni wote wazawa wanaopata kandarasi ya uchapaji kufanya uchapaji nje ya nchi.

### 2.1.6 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kufuatilia utendaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na taasisi zake Kamati ilipokea taarifa zifuatazo: -

#### (i) Malengo na mikakati ya uendelezaji na uhimizaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) linatekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu matumizi na maendeleo ya Kiswahili nchini pamoja na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi

kwa mujibu wa Sheria ya ya Bunge Na. 27 ya mwaka 1967, pamoja na marekebisho yake ya mwaka 1983 na 2016.

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa iliyowasilishwa kwa Kamati, BAKITA ilieleza mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika matumizi na maendeleo ya Kiswahili. Mafanikio haya ni pamoja:-

(a) Kutengwa kwa Siku maalumu ya maadhimisho ya Kiswahili duniani ambapo Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limetenga tarehe 7 Julai, kwa kila mwaka na hivyo basi, Kiswahili kimeendelea kupata hadhi kubwa duniani;

(b) Kuongezeka kwa matumizi ya Kiswahili kimataifa ambapo lugha ya Kiswahili inafundishwa katika vituo na Vyuo mbalimbali duniani. Hadi kufikia Agosti 2024, vituo na Vyuo vimefikia 150. Fauka ya hayo, Kiswahili kinatumiwa katika matangazo ya idhaa mbalimbali za redio za kimataifa. Hadi Agosti 2024 kuna jumla ya redio na televisheni zipatazo 44. Kwa sababu hiyo, nafasi ya Kiswahili nje ya nchi inazidi kupanuka na kuongezeka kama utambulisho wa Mwafrika;

(c) Kuongezeka kwa Idadi ya watumiaji wa Kiswahili duniani ambapo hadi Agosti 2024 kuna wazungumzaji wa Kiswahili zaidi ya **milioni 500** duniani. Ongezeko la watumiaji wa Kiswahili linaenda sambamba na ongezeko la machapisho ya Kiswahili kwa upande wa isimu na fasihi na kumekuwa na chachu kwa waandishi wengi kuanza kuandika kwa Kiswahili; na

(d) Kuongezeka kwa matumizi ya Kiswahili Kikanda na hivyo, lugha ya Kiswahili imekuwa lugha ya mawasiliano mapana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, kwa sasa Kiswahili ni mojawapo ya lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lugha rasmi na lugha ya kazi katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa

Wazalishaji wa Almasi Afrika. Kuongezeka kwa matumizi hayo kumesababisha kuongezeka kwa huduma za tafsiri na ukalimani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kasi ya uendelezaji na uhimizaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi ni wa kuridhisha kwani hadi wakati taarifa hii inawasilishwa katika Kamati, BAKITA ilikuwa imefanikiwa kuwasajili wakalimani **145** wa lugha mbalimbali kupitia mifumo ya kielektroniki ambao wanatumiwa katika mikutano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa mikutano hii ni ya Umoja wa Afrika na Kamisheni zake, Bunge la Afrika, SADC, Umoja wa Wazalishaji Almasi Afrika, na Taasisi za Serikali na binafsi

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo kwa mafanikio mbalimbali ya Baraza la Kiswahili Tanzania, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

(a) Kutokana na Ukosefu wa rasilimali fedha, Baraza linashindwa kuwa na vituo vya kimkakati vya kusimamia kukua na kuenea kwa Kiswahili na utamaduni wake kwa ufanisi; na

(b) Kuwepo kwa upungufu wa watumishi ambapo hadi Agosti 2024, kuna watumishi 43 kati ya Ikama ya watumishi 85 na hivyo kufanya upungufu wa watumishi 42. Idadi ya watumishi waliopo ni ndogo ikizingatiwa kuwa majukumu ya Kiswahili kwa sasa ni makubwa na yanazidi kuongezeka kulingana na kasi ya kuenea kwa Kiswahili duniani.

**(ii) Ujenzi wa Miundombinu ya Akademia ya Chuo cha Michezo Malya**

**Mheshimiwa Spika,** ilielezwa kwamba, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kilianzishwa mwaka 1979 kwa malengo ya kutoa mafunzo kwa wataalamu wa michezo na kusaidia katika kuwaendeleza vijana na kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya

tafiti mbalimbali za kimichezo na kutoa ushauri wa kimichezo kwa wadau mbalimbali. Chuo kipo Wilaya ya Kwimba umbali wa kilometa 120 Kusini mwa Jiji la Mwanza na kimesajiliwa mwaka 2010 na Baraza la Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTVET).

**Mheshimiwa Spika,** katika mijadala ya Kamati kuhusu ujenzi wa miundombinu ya Akademia, Kamati ilielezwa kwamba, ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya inatokana na dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza michezo nchini. Akademia hii inatarajiwa kuwa ya kisasa na ya aina yake katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa ajili ya maendeleo ya michezo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 6 Julai, 2023 wenye jumla ya ya gharama ya **Shilingi 31,520,000,000.** Kazi za ujenzi zinasimamiwa na Mshauri Elekezi Kampuni ya Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam ijulikanayo kwa jina la ARU Built Environmental Consulting Company Ltd. (ABECC). Aidha, ujenzi wa kituo mahiri cha michezo umeanza kwa hatua za ujenzi wa majengo yanayohusisha darasa, bwalo na hosteli ambapo hadi sasa umefikia **asilimia 15.2**.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia nzuri ya Serikali ya ujenzi wa miundombinu ya Akademia. Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa utolewaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa Akademia hii si wa kuridhisha na hivyo kusababisha kutokukamilika kwa mradi huu kwa wakati na kutokutimia kwa azma ya Serikali ya kuendeleza michezo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ni matumaini ya Kamati kwamba fedha hizo zitatolewa kikamilifu na kwa wakati ili kuwezesha kukamilisha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kamati yangu itaendelea kufuatilia kwa ukaribu suala hili ambalo kimsingi linalenga kuboresha ustawi wa michezo nchini.

### (iii) Mpango wa kuwezesha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kuwa na vyanzo vya mapato endelevu

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Utamaduni ulianzishwa na Serikali mwaka 1998 kwa kushirikiana na Serikali ya Uswidi. Kutokana na kuhuishwa kwa Mfuko wa Utamaduni mwaka 2020 na kupanua majukumu yake katika Sekta ya ya Sanaa, kwa lengo la kutekeleza Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997. Serikali ilianzisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kwa Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini (*Trustees' Incorporation Act*) 2002 (CAP. 318 R.E. 2002), lengo la kuanzisha Mfuko huu ni kuinua ubora wa kazi za utamaduni na sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara, kutengeneza ajira pamoja na kuchangia katika pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliarifiwa kuwa tangu kuanzishwa kwa mfuko huu sehemu kubwa ya mtaji wa Mfuko unatokana na bajeti ya Serikali, kwa mwaka 2023/2024 Serikali ilitenga bajeti ya **Shilingi 1,600,000,000** na kwa mwaka 2024/2025 Serikali imetenga **Shilingi 3,000,000,000** ongezeko la **Shilingi 1,400,000,000** sawa na **asilimia 87.5.** Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara inaendelea kufanya ushawishi kwa Serikali ili iweze kuongeza bajeti ya Mfuko kwa ajili ya kuwakopesha wadau wa utamaduni na sanaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji ili kujua kuhusu mkakati wa Mfuko kuwa na vyanzo vya mapato endelevu. Kamati ilielezwa kuwa kupitia sheria ya COSOTA ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura Na. 218, inaelekeza asilimia 10 ya kodi inayotokana na vibebeo vya kazi za ubunifu vilivyopo kupelekwa katika Mfuko wa Utamaduni na Sanaa. COSOTA imeanza kutekeleza sheria hiyo kuanzia mwaka 2023/2024 ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 84.798** zimekusanywa na zitawasilishwa katika Mfuko huo.

**Mheshimiwa Spika,** vyanzo vingine vya mapato ni pamoja na **asilimia tatu (3)** ya mapato ya ndani vinavyotokana taasisi zilizopo chini ya Wizara, maandiko mbalimbali ya miradi yanayowasilishwa kwa wafadhili wa kitaifa na kimataifa na ushirikiano baina ya wadau kama Bank ya CRDB na NBC. Kamati

inaipongeza Serikali kwa juhudi inazozifanya za kuendelea kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kutunisha mfuko huo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo Kamati ilibaini pia kuwepo kwa changamoto zinazoukabili mfuko huu ikiwemo:-

(a) Makusanyo madogo yatokanayo na tozo za hakimiliki na hakishiriki kutokana na kuwa vifaa vingi vya kubebea kazi za sanaa havipo katika orodha ya vifaa vinavyotakiwa kutozwa kodi;

(b) Makusanyo madogo ya mapato ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA,) Bodi ya Filamu Tanzania (BFT), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) kutokana na wasanii kutohamasika kujisajili kwa ajili ya kupata huduma;

(c) Mapato yanayotokana na uwekezaji wa asilimia mbili ni ya uwekezaji wa Mtaji wa Mfuko hivyo yanalipwa kwa kulingana na kiwango kilichowekezwa. Kutokana na kiwango kidogo cha mtaji wa uwekezaji pia kiasi cha gawio ni kidogo; na

(d) Wasanii kutorejesha kwa wakati mikopo ya mfuko. Mfuko ulitoa mikopo kwa miradi **45** yenye thamani ya **shilingi Bilioni 1.077** moja kwa moja kwa walengwa. Aidha, hadi mwezi Juni 2024 Mfuko ulitakiwa kupokea marejesho ya **shilingi milioni 540**. Hata hivyo, marejesho yaliyopokelewa ni **shilingi milioni 230** sawa na **asilimia 43** na kiasi kinachodaiwa ni **shillingi milioni 310 sawa na asilimia 57**. Kupitia mikopo iliyotolewa kupitia Taasisi za fedha, miradi **171** iliwezeshwa shilingi **Bilioni 3.1**, ambapo kiwango kilichorejeshwa ni **Shilingi Bilioni 1.58** sawa na **asilimia 96**.

**(iv) Maandalizi ya mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Mataifa ya Afrika (AFCON, 2027) na Mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ligi za Ndani ya Nchi (CHAN, 2025) hususani ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na ujenzi wa Viwanja katika Mkoa wa Arusha na Dodoma**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupokea taarifa hii Kamati ilitaarifiwa kwamba utekelezaji wa mradi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu katika Jiji la Arusha ni utekelezaji wa Ilani ya CCM chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuendeleza sekta ya michezo nchini, kukuza utalii wa michezo, kuitangaza nchi kimataifa na kuibua vyanzo vipya vya ajira na mapato kwa Serikali, pamoja na kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/2022 – 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kuwa, mradi huu ni utekelezaji wa maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Mataifa ya Afrika (AFCON, 2027) na Mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ligi za Ndani ya Nchi (CHAN, 2025) kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda. Ujenzi wa Uwanja huu katika Jiji la Arusha unatarajiwa kuwa chachu ya kuongeza utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027 katika nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilielezwa kwamba gharama za ujenzi wa mradi wote kuanzia mwanzo hadi kukabidhiwa kwa Mshitiri ni jumla ya **Shilingi 338,542,000,000.** Kazi za ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha unakadiriwa kufikia **asilimia 21** na muda uliotumika ni **asilimia 25**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu Arusha. Aidha, Kamati inasisitiza mradi huu ukamilike kwa wakati ili

nchi yetu iweze kutimiza vigezo vya FIFA na CAF kwa kukamilisha idadi ya viwanja vinavyotakiwa na CAF katika kuwa mwenyeji wa mashindano ya CHAN na AFCON.

**Mheshimiwa Spika,** katika mijadala ya Kamati kuhusu ujenzi wa Uwanja wa Dodoma Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya mchakato wa muda mrefu wa kumpata mshauri elekezi, hivyo basi, kuchelewesha kuanza kwa zoezi la utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa chimbuko la ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwa ni matokeo ya takribani zaidi ya miaka 17 uwanja haujawahi kufanyiwa ukarabati tangu umeanza kutumika, hivyo maeneo mengi yameharibika na baadhi ya mifumo ya kuendesha uwanja imeharibika na kupitwa na wakati. Fauka ya hayo, masuala mengine yaliyosababisha Serikali kufanya ukarabati mkubwa wa uwanja huu ni mabadiliko ya kanuni za uendeshaji wa mpira wa miguu barani Afrika na Duniani kote.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupokea taarifa ya ukarabati wa uwanja wa Benjamin Mkapa, Kamati ilijulishwa kuwa ukarabati wa uwanja utatumia jumla ya gharama ya **Shilingi 31,329,180,963.16.** Aidha, Kwa mujibu wa mkataba, ukarabati ulitarajiwa kukamilika tarehe 24 Agosti 2024, japo kuwa mpaka Kamati inapowasisha taarifa hii ukarabati haujakamilika na kuongezwa muda wa siku 152

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa licha ya dhamira njema ya Serikali, kasi ya ukarabati wa mradi huu umechukua muda mrefu licha ya fedha kutolewa kwa wakati. Ni rai ya Kamati kuwa, Menejimenti ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ihakikishe inasimamia kikamilifu ukarabati huu na uwanja ukamilike kwa wakati ili kuepuka gharama kubwa zisizo na ulazima. Aidha, Serikali iandae mkakati wa kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya Kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya uwanja wa Benjamin Mkapa.

**(v) Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo katika Shule 56 za Msingi nchini**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupokea taarifa hii Kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa mradi huu utagharimu jumla ya kiasi cha **shilingi 11,500,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya michezo katika shule kumi (10) za sekondari katika awamu ya kwanza kati ya shule 56 ili kutumika kuibua na kuendeleza michezo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa licha ya Serikali kuwa na nia njema ya kutenga fedha, bado utekelezaji wa mradu huu haujaanza kutokana na changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya kukarabatiwa kwa miundombinu ya michezo kwa shule zote 56 za michezo nchini. Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa mradi huu kwani hadi wakati taarifa hii inawasilishwa katika Kamati, Wizara ilikuwa imefanikiwa tu upatikanaji wa mshauri elekezi na kutangazwa kwa zabuni ya kupata Mkandarasi wa ujenzi.

**(vi) Matumizi ya Fedha zinazotokana na asilimia tano (5%) ya Michezo ya Kubahatisha (Sport Betting)**

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020, Serikali ilipitisha Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kupokea asilimia 5 ya mapato yatokanayo na michezo ya kubashiri matokeo (Sport Betting) inayosimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na jitihada zinazofanywa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwani limefanikiwa kuziwezesha timu za michezo mbalimbali za Taifa kushiriki mashindano makubwa ya kimataifa.

Mashindano hayo ya Kimataifa ni kama vile AFCON 2023 yaliyofanyika nchini Ivory Coast mwaka 2024, Olimpiki yaliyofanyika nchini Ufaransa mwaka 2024, Paraolimpiki yaliyofanyika Ufaransa mwaka 2024, Mashindano ya Africa (All

African Games) yaliyofanyika Ghana mwaka 2024 pamoja na mashindano ya wanamichezo wa mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu (Amputee Football) yaliyofanyika nchini Misri mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika,** katika majadiliano ya Taarifa hii, Kamati ilibaini kuwa mafanikio hayo yalitokana na Baraza la Michezo la Taifa kupokea jumla ya **Shilingi 7,221,935,855** kutoka Wizara ya Fedha ikiwa ni **asilimia 5** ya mapato yatokanayo na michezo ya kubashiri matokeo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2021/2022 hadi Septemba 2024/2025 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za michezo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Kamati ilibaini kwamba pamoja na shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia fedha za mfuko, bado, kuna changamoto ya mahitaji makubwa ya fedha za shughuli mbalimbali zinazohitaji kufadhiliwa kupitia Mfuko ukilinganisha na hali ya upatikanaji wa fedha.

**(vii) Mikakati Madhubuti ya kukuza Sanaa nchini, hususani tasnia ya Filamu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya uendeshaji wa Bodi ya Filamu iliyoeleza majukumu ya Bodi ya Filamu Tanzania kama yalivyoainishwa kwenye sheria ya Filamu na Michezo ya kuigiza Na 4 ya Mwaka 1976.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa juu ya shughuli zinazofanywa na Bodi ya Filamu Tanzania kuhusu mikakati madhubuti ya kukuza Sanaa nchini, ambapo ilielezwa kwamba Bodi inaanzisha Mifumo ya kidijiti (Digital Platforms) ili kuweka mazingira rafiki na wezeshi katika Tasnia ya Filamu, kuwepo kwa mchakato wa ujenzi wa studio ya Filamu na Jumba Changamani la burudani (Arts and sports Arena) utakaogarimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 450** ambazo ni fedha za mkopo kutoka Korea ya Kusini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, upo mkakati wa kutoa fursa kwa wadau wa filamu kujipatia kipato kwa kuuza filamu zao kwenye mashirika ya ndege hususan kimataifa, baadhi ya mashirika yaliyokubali kupokea filamu za kitanzania ni pamoja na Air Tanzania Company Limited (ATCL), Oman Air, Ethiopian Airlines, Emirates na Qatar Airlines.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto zinazoikabili Bodi zikiwemo:-

(a) Ukosefu wa studio ya kisasa kwa ajili ya kutayarisha filamu zenye ubora wa kushindana kimataifa;

(b) Filamu nyingi za kitanzania kukosa ubora unaokidhi viwango vya ushindani katika soko la ndani kitaifa na nje kimataifa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo taaluma sahihi katika sekta ya filamu, weledi mdogo wa mafunzo na wabobezi wa filamu wa kimataifa nchini; na

(c) Baadhi ya wadau wa filamu kutozingatia Sheria ya Filamu na Kanuni zake wakiwemo watayarishaji wa filamu na hivyo kuathiri mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Taasisi na utekelezaji wa mipango yake.

**(viii) Uboreshaji wa Shirika la Utangazaji la Tanzania – TBC**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa iliyoletwa katika Kamati inaonyesha kuwa, hadi kufikia Juni, 2024, usikivu wa redio za TBC kwa teknolojia ya masafa ya FM umefikia asilimia **85** ya Wilaya zote nchini na asilimia **65** ya wananchi wote. Kwa upande wa Televisheni hadi sasa TBC1, TBC2 na Tanzania Safari zinapatikana kwa asilimia 100 kijiografia kupitia teknolojia ya Satelaiti (Direct To Home - DTH). Aidha, kwa kutumia teknolojia ya mitambo ya ardhini, (Digital Terrestrial Transmission - DTT), wananchi wamefikiwa kwa asilimia **33** na asilimia **58** ya nchi imefikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini pia kuwepo kwa changamoto zinazoikabili Shirika zikiwemo:-

(i) Changamoto ya kukusanya na kuhifadhi maudhui ya kumbukumbu za matukio yote yenye maslahi ya kitaifa kwa njia ya sauti na picha jongefu;

(ii) Ukosefu wa vyanzo vya fedha vya uhakika, toshelevu na endelevu kwa ajili ya uwekezaji na uendeshaji wa miundombinu ya utangazaji;

(iii) Ongezeko la gharama za uendeshaji zitokanazo na ukarabati wa miundombinu (mitambo ya masafa ya kati iliyojengwa miaka ya 1980 na mitambo ya masafa ya FM iliyojengwa miaka ya 2000) ambayo imepitwa na wakati kutokana na mabadiliko ya teknolojia;

(iv) Uhitaji wa uwekezaji kwa ajili ya upanuzi wa usikivu wa redio pamoja na ujenzi wa studio mpya za redio na televisheni zinazoendana na teknolojia;

(v) Mahitaji ya rasilimali za kutosha ikiwemo watumishi wenye weledi na vipaji kuweza kuandaa maudhui na kuendesha vipindi; na

(vi) Mahitaji ya kuwa na chaneli mahsusi za kimkakati zinazohusiana na masuala muhimu katika nyanja za: Kielimu, kimataifa, kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 pamoja uchambuzi wake, Kamati ina maoni kwa mambo 10 kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mambo yaliyobainika wakati wa uchambuzi, Kamati inamaoni kama ifuatavyo:-

**3.1.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**(a) Changamoto za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**KWA KUWA**, uchambuzi umeonesha kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inakabiliwa na changamoto kama vile:

(i) upungufu wa bajeti unaosababisha idadi kubwa ya wanafunzi ambao wanastahili mikopo kushindwa kumudu gharama za masomo yao; na
(ii) ukosefu wa vyanzo mbadala vya mapato kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kusaidia idadi kubwa zaidi ya wanafunzi wanaostahili mkopo,

**NA KWA KUWA**, mfumo wa urejeshaji wa mikopo haujaimarika ipasavyo kutokana na:

(i) ukosefu wa mfumo rafiki wa ukusanyaji wa madeni,

(ii) utaratibu wa ukusanyaji wa madeni kutoka kwa walionufaika na mkopo kutohusisha matumizi ya mifumo ya NIDA,

(iii) uelewa mdogo wa umma kuhusu umuhimu wa kurejesha mikopo, jambo linalosababisha upotevu wa fedha zinazopaswa kurudi kwenye mfuko wa mikopo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) iongeza bajeti ya Bodi ya Mikopo ili kuhakikisha wanafunzi wote wanaostahili wanapata mikopo ipasavyo;

(ii) ifanye mabadiliko ya muundo wa Bodi ya Mikopo ili ifanye kazi kwa muundo wa Mfuko Endelevu wa Fedha (Revolving Fund) kwa lengo la kuwa na uhakika wa fedha kwenye Mfuko huo;

(iii) ianzishe mfumo madhubuti wa urejeshaji wa mikopo ambao utaunganishwa na mifumo ya NIDA pamoja na wadau wengine ikwa lengo la kupata taarifa za wanufaika kwa wakati na kwa usahihi;

(iv) iwezeshe vyanzo mbadala vya mapato kwa ajili ya ugharamiaji wa elimu ya juu kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine;

(v) iongeza juhudi za utoaji wa elimu kwa umma kuhusu wajibu wa urejeshaji wa mikopo kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji endelevu wa fedha za mikopo kwa wanaostahili.

**(b) Upungufu wa Walimu na Miundombinu ya kufundishia hasa kwa mkondo wa Amali**

**KWA KUWA**, shule za amali nchini zinakabiliwa na chagamoto za:

(i) Uhaba wa walimu wa Amali wenye sifa na weledi na ukosefu wa vyuo maalumu kwa mafunzo ya ualimu wa amali, ambapo mahitaji ni walimu **620**, waliopo **62** na upungufu **558**;

(ii) Uhaba wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia; na

(iii) ukosefu wa miundombinu sahihi kama vile maabara na warsha za vitendo,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inakwamisha na kuzorotesha elimu ya amali nchini pamoja na utekelezaji wa mtaala wa mafunzo ya amali katika shule za Serikali,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) iongeze bajeti ya kutosha ya kuajiri walimu wenye sifa na weledi wa masomo ya amali kulingana na mahitaji;

(ii) iwezeshe upatikanaji wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia katika shule za Amali,

(iii) iboreshe vifaa na miundombinu muhimu katika shule za Serikali ambazo zimeanza utekelezaji wa Mtaala katika Mkondo wa Amali,

(iv) iweke mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuandaa walimu wa masomo ya amali ili kuwawezesha wahitimu wa mafunzo hayo kusoma kozi hizo na kuajiriwa kama walimu; na

(v) ipange vyuo maalumu kwa ajili ya mafunzo ya ualimu wa Amali.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) Kutenga vyuo maalumu kwa ajili ya mafunzo ya ualimu wa Amali ili kuzalisha walimu wenye ujuzi wa kutosha katika sekta hiyo; na

(ii) Kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuajiri walimu wa Amali ili kupunguza uhaba wa walimu na kuboresha ufundishaji wa masomo ya Amali nchini.

**(c) Ucheleweshaji wa Uandaaji, Uchapaji na Usambazaji wa Vitabu Shuleni**

**KWA KUWA**, uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu vya shule unatekelezwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), lakini utaratibu uliopo kwa sasa Wizara ya Fedha inapeleka fedha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao nao wanapeleka fedha hizo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, jambo ambalo –

(i) husababisha ucheleweshaji wa fedha; na

(ii) huongeza urasimu wa kiutawala na kupunguza ufanisi wa utekelezaji wa jukumu hilo;

**NA KWA KUWA**, ucheleweshaji wa fedha na urasimu huo husababisha upungufu wa vitabu shuleni, hali ambayo:-

(i) inayoathiri ubora wa elimu;

(ii) inaongeza mzigo kwa walimu na wanafunzi; na

(iii) inachelewesha utekelezaji wa sera za elimu nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ipeleke moja kwa moja fedha za uchapishaji wa vitabu kwa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ili kuongeza ufanisi, kasi, na uwajibikaji katika uandaaji na usambazaji wa vitabu shuleni kwa wakati unaofaa.

**(d) Utekelezaji Usioridha wa Miradi wa Vyuo 64 vya VETA**

**KWA KUWA,** ujenzi wa vyuo vya Mafunzo ya Ufundi stadi ni muhimu katika kukuza maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, lakini utekelezaji wake katika Vyuo 64 vya VETA hauridhishi;

**NA KWA KUWA,** ucheleweshaji wa kukamilisha miradi hii :-

(i) unaleta athari kwa maendeleo ya ufundi stadi nchini;

(ii) unasababisha usumbufu kwa wanafunzi na watumishi katika vyuo hivyo; na

(iii) unachelewesha manufaa yaliyokusudiwa kwa Taifa kutokana na ujenzi wa vyuo vya veta,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba**,** Serikali -

(i) ihakikishe kuwa fedha za ujenzi wa vyuo hivi zinatolewa zote ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa,

(ii) iongeze juhudi za kuweka huduma muhimu za miundombinu kama maji, umeme na barabara kwa wanafunzi katika maeneo yote yenye vyuo vya VBeta vilivyojengwa; na

(iii) ichukue hatua za haraka kuhakikisha maeneo yote ya vyuo vya VETA ambayo hayana hati yanapatiwa hati kwa kufuata taratibu stahiki.

### 3.1.2 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**(a) Ukosefu wa vyanzo vya fedha vya uhakika, toshelevu na endelevu kwa ajili ya uwekezaji na uendeshaji wa miundombinu ya utangazaji - TBC**

**KWA KUWA**, kukosekana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya:-

(i) kuongeza usikivu wa redio;

(ii) ujenzi wa studio mpya za redio na televisheni, watumishi wenye weledi na vipaji wanaoendana na teknolojia;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaweza:

(i) kukwamisha lengo la Serikali kuwa na chombo bora cha utangazaji chenye manufaa kwa nchi; na

(ii) kupunguza uwezo wa TBC kufikia malengo yake ya kuwa chombo cha taifa kinachoelimisha, kinachochochea maendeleo na kinachowafikia wananchi wote kwa njia bora,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

(i) kutoa fedha za kutosha, kwa wakati, ili kuiwezesha TBC kujiendesha kibiashara na kupambana na ushindani wa kibiashara;

(ii) kuhakikisha kuwa minara ya Mawasiliano kwenye maeneo yenye changamoto za usikivu, hasa mipakani mwa nchi na maeneo hatarishi, inajengwa ili kuhakikisha huduma za utangazaji zinawafikia wananchi wote;

(iii) Kuwezesha ushirikiano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na TBC katika kuimarisha maudhui ya kipindi cha Safari Channel, ili kuboresha utoaji wa maudhui na kuongeza ufahamu wa utalii na maliasili ya nchi;

(iv) kuendelea kuajiri watumishi wenye vipaji maalumu ili kuifikia jamii kwa urahisi, na kuhakikisha chombo cha utangazaji kinakuwa na uwezo wa kutoa huduma bora na zenye ubora kwa wananchi.

**(b) Upungufu wa Fedha na Watumishi kwa BAKITA**

**KWA KUWA** BAKITA inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili wenye ujuzi wa lugha nyingine, jambo linalokwamisha juhudi za kuongeza kasi ya

ukuaji wa lugha sanifu ya Kiswahili na kuufanya kuwa lugha ya kimataifa katika sekta mbalimbali;

**NA KWA KUWA** tatizo hili linachelewesha juhudi za kuhakikisha Kiswahili kinakuwa na hadhi ya kimataifa na kuimarisha matumizi yake katika nyanja za elimu, biashara, na utamaduni.

**KWA HIYO BASI Bunge,** linaazimia kwamba, Serikali -

(ii) iliwezeshe BAKITA kuajiri wataalamu wa lugha ya Kiswahili wenye ujuzi wa lugha nyingine ili kuongeza kasi ya ukuaji wa lugha sanifu ya Kiswahili;

(iii) izingatie ahadi iliyotolewa kwenye Ilani ya CCM, aya 283(d), kuhusu kuimarishwa kwa mila, desturi, na tamaduni nzuri zinazojenga utaifa, kwa kuiwezesha BAKITA kuongeza wigo wa kuuelimisha umma kuhusu Kiswahili na utamaduni wetu; na

(iv) Serikali iiwezeshe BAKITA kufanya utafiti katika nchi ambako Kiswahili kinabidhaishwa ili kubaini fursa, manufaa, na namna ya kuongeza ushawishi wa Kiswahili kimataifa.

**(c) Mapato ya Makusanyo ya tozo ya hakimiliki kutokuwasilishwa COSOTA**

**KWA KUWA**, Serikali inakutana na changamoto ya kutokutolewa kwa fedha zote za makusanyo ya Tozo ya Hakimiliki kwa wakati, jambo linalosababisha ucheleweshaji katika utekelezaji wa malengo ya kuanzishwa kwa tozo hii;

**NA KWA KUWA**, athari ya changamoto hii ni kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kukuza na kulinda hakimiliki, jambo linaloharibu sekta ya hakimiliki na

kupunguza fursa za ajira kwa wasanii, wabunifu, na kuathiri maendeleo ya utamaduni na ubunifu nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa fedha zote za makusanyo ya Tozo ya Hakimiliki zitatolewa kikamilifu na kwa wakati, ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na kukuza sekta ya hakimiliki nchini.

**(d) Kutokamilika kwa Ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa**

**KWA KUWA** Uwanja wa Benjamin Mkapa ni moja ya miundombinu muhimu ya michezo nchini inayotumiwa kwa matukio ya kitaifa na kimataifa, lakini unakabiliwa na changamoto za matengenezo na usimamizi endelevu;

**KWA KUWA** uwanja huo pamoja na viwanja vingine vya michezo unahitaji matengenezo ya mara kwa mara ili kudumisha ubora wake wa kimataifa na kuimarisha maendeleo ya sekta ya michezo nchini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) ihakikishe ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa unakamilika ifikapo Aprili, 2025;

(ii) iandae mkakati wa kuanzisha chombo maalum cha usimamizi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na viwanja vingine vinavyojengwa na Serikali ili kuhakikisha vinatunzwa na kuwa katika ubora wa kimataifa:

(iii) Serikali iweke utaratibu wa sehemu ya makusanyo ya uwanja kubaki kwa matumizi ya uwanja huo (Retention) ili kurahisisha matengenezo ya dharura yanapojitokeza; na

(iv) iandae mkakati wa kuboresha viwanja vingine vya michezo ili kupunguza mzigo wa matumizi makubwa kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**(e) Kusuasua kwa Ujenzi wa Hostel na miundombinu ya Chuo cha Akademia ya Michezo Malya**

**KWA KUWA**, Taarifa za Serikali zimeonesha kuwa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kinakabiliwa na changamoto ya ucheleweshwaji wa fedha, jambo linalosababisha miradi kutokukamilika kwa wakati;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inasababisha kutokukamilika kwa mradi huu kwa wakati na kutokutimia kwa azma ya Serikali ya kuendeleza michezo nchini, hivyo kuathiri maendeleo ya michezo na vijana katika maeneo husika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa fedha zote zinazohusiana na mradi huu zinatolewa kikamilifu na kwa wakati, ili kuwezesha kukamilisha mradi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nakupongeza kwa kazi kubwa unayofanya ya kuliongoza Bunge letu vizuri. Namshukuru pia Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanazofanya.

**Mheshimiwa Spika**, Nachukua fursa hii kuwashukuru Mawaziri wa wizara mbili zinazosimamiwa na Kamati ambao ni Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) – Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mhe. Mhe. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) – Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha ninawashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati, ambao ni; Mhe. Omary Juma Kipanga (Mb) – Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi

na Teknolojia na Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb) – Naibu Waziri wa Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa Kamati. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara hizi mbili kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati na kurahisisha utendaji kazi.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Mussa Ramadhani Sima (Mb) kwa ushirikiano anaonipa mimi pamoja na Kamati kwa ujumla. Kipekee zaidi nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mzuri walionipa katika kutekeleza shughuli za Kamati na hivyo kurahisisha majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Nashon William Bidyanguze, - Mjumbe
7. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Esther Edwin Maleko, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mwanahamisi Kassian Said, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Dkt. Thea Ntara, Mb - Mjumbe
16. Mhe.Tunza Issa Malapo, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Rose Vicent Busiga Mb - Mjumbe
18. Mhe. Yahya Ally Hamis, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru sana Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Baraka

Ildephonce Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Pamoja nao namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, wakurugenzi wasaidizi na Sekretarieti kwa kuisaidia Kamati wakati wote na kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**
11 Februari, 2025

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni, na Michezo. Hoja imeungwa mkono.

Sasa tunaanza na uchangiaji, tunaanza na Mheshimiwa Jafari Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Gambo na Mheshimiwa Aloyce Kamamba ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwa taarifa zote mbili. Kwanza, niseme ninaunga mkono taarifa zote za Kamati, kwa maana Kamati ya TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), pamoja na Kamati ya Elimu, Utamaduni, na Michezo. Naunga mkono taarifa zote zilizowasilishwa na Wenyeviti, maoni pamoja na mapendekezo yote ambayo yamewasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya TAMISEMI imepata ridhaa ya kutembelea maeneo mbalimbali nchini, kukagua miradi ya maendeleo, hususan maeneo ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepeleka fedha za miradi ya maendeleo. Bila shaka Wabunge wataungana nami kwamba, maeneo mengi Mheshimiwa Rais amepeleka fedha nyingi za miradi ya maendeleo, na kazi kubwa inafanyika kwenye kila eneo ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, hatuna budi sisi kama Kamati kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya maendeleao na kutimiza yale maono, pamoja na wasaidizi wake wa maeneo hayo kwa namna ambavyo wanaendelea kusimamia hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pia shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na Naibu Mawaziri, kwa ushirikiano na namna ambavyo wanaendelea kusimamia dhamira na maono ya Mheshimiwa Rais, kuhakikisha fedha hizi zinakwenda kuwahudumia wananchi maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipowashukuru pia Makatibu Wakuu wa Wizara pamoja na Naibu Makatibu Wakuu. Pia, hata halmashauri ambazo Wakurugenzi wameendelea kusimamia fedha hizi kuhakikisha kwamba zinakwenda kutimiza yale malengo ambayo Mheshimiwa Rais amedhamiria kuwahudumia wananchi wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, yapo mambo kadhaa sisi kama Kamati tumeshauri, na tungetamani Serikali iweze kuyatilia mkazo ili kuweza kukidhi haja na maono ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tumeona fedha zinazokwenda kutekeleza miradi kwa upande wa *TARURA*. Fedha hizi hazitoshi na haziendi. Suala hili la *TARURA* lina sura mbili.

Kwanza lina sura ya fedha yenyewe ya bajeti ambayo imetengwa na Wizara, zaidi ya shilingi bilioni 883 ambayo waliomba watu wa *TARURA* ili kutimiza wajibu wao katika kutekeleza maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, lina sura ya pili ya fedha ya dharura, ambayo iliombwa ndani ya Bunge hili, zaidi ya shilingi milioni 326, kwenda kutimiza na kutengeneza barabara zilizokuwa zimeharibiwa na mvua upande wa *El-Nino*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikitiko ya Kamati, na ndiyo maana tumesema kwenye maoni na mapendekezo yetu, ni kwamba, hata ukiangalia la kwanza hili la fedha za bajeti, shilingi bilioni 883, mpaka kufikia Desemba, kwa maana ya Julai – Desemba, imekwenda 10% mpaka 11% peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shilingi bilioni 883 wamepeleka shilingi bilioni 92 peke yake! Maana yake unaweza ukaona kwamba maeneo mengi wakandarasi wameendelea kudai, na kiukweli *TARURA* imeshindwa kutimiza wajibu wake, kwa sababu fedha za utekelezaji wa miradi haziendi kulingana na tulivyopitisha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tulipitisha fedha hapa. *TARURA* walikuja wakaomba zaidi ya shilingi bilioni 326 kwa ajili ya miradi ya dharura, na dharura hii sisi Wabunge wote ni mashahidi, ilisababishwa na Mvua za *El-Nino* pamoja na Hidaya. Sasa, hii ni dharura, na tulitakiwa tuichukulie kama dharura, lakini unaweza ukaona, katika shilingi bilioni 326, fedha ambayo imekwenda ni shilingi bilioni 83 peke yake. Hawa watu hawawezi wakaendana na kasi hiyo ya udharura wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubaliane kwamba jambo ambalo lina udharura lazima tulichukulie kwa udharura wake, kwa kuona ule muhimu wenyewe. Huwezi ukawa na dharura ukai-*treat* kwa mwaka mzima. Tunakwenda mwaka huu, na mvua zinaenda kunyesha awamu ya pili, hatujapeleka fedha hizi ambazo *TARURA* waliomba, zaidi ya shilingi bilioni 326. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wetu kama Kamati ni nini? La kwanza, ndiyo maana tumependekeza Mheshimiwa Waziri, hasa Waziri wa Fedha, wapeleke kwanza fedha zilizopo kwenye bajeti, zaidi ya shilingi bilioni 883, ili watu wa *TARURA* waende kutimiza wajibu wao kwenye maeneo mengi, kwenye barabara ambazo zinaharibika, na waweze kulipa wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunapendekeza pia hii fedha ya dharura shilingi bilioni 326, haina haja ya kusubiri mpaka mvua zianze kunyesha awamu nyingine ya pili. Wapewe fedha hizi ili waende wakatimize kazi ya udharura. Shilingi bilioni 84 haiwezi kutosha, na ndiyo maana tukapendekeza kwamba, pamoja na hilo, ipo fedha ya *World Bank* kupitia *DMDP*, na tukasema fedha ile ilikuwa ni ya dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* wameomba zaidi ya shilingi bilioni 256, wakiwa wanaamini wakipewa fedha hizi, wakiunganisha na ile shilingi bilioni 83 angalau watakuwa na shilingi bilioni 340. Inaweza kusaidia na kutekeleza ilani kwenye maeneo mengi ya barabara za vijijini ambazo zimeharibiwa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha alione hili. Tunashukuru ametoa shilingi bilioni 83, lakini haitoishi. Tunaomba atoe fedha kupitia hii Miradi ya *DMDP*, hii shilingi bilioni 256. Wizara ilione hili; kama bado liko kwao, wapo kwenye mchakato wa manunuzi, waliharakishe ili angalau hawa watu wa *TARURA* wapate hii fedha shilingi bilioni 256, waende wakatekeleze wajibu wao katika maeneo mengi ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusiana na *DART* pamoja na *UDART*. Hapa kuna Wakala ambaye ni *DART*, lakini kuna mtoa huduma ambaye ni *UDART*. Hawa watu waliingia mkataba wa pamoja wa namna ya *UDART* kumlipa *DART* kwenye *Access Fee* ya barabara ambayo wanaitumia kutoa huduma ya mabasi. Kinachoshangaza, pamoja na makubaliano ya kimkataba, pamoja na sisi kama Bunge kupitisha bajeti iliyoletwa na Wizara

hapa ndani, kwamba *UDART* watamlipa *DART* na fedha ile ni sehemu ya bajeti ya Wizara iliyoleta, leo hii tunaingia kwenye mgogoro ambao hauna sababu kwa taasisi mbili za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani leo *UDART* wanasema hawawezi wakalipa fedha kwa *DART*, kwa sababu ambazo hazina msingi wowote. Ndiyo maana tumeshauri kwamba, kwa kuwa tulipitisha hapa, na Sheria ya Bajeti ikalinda bajeti ile tuliyopitisha ndani ya Bunge, tunawaomba watu wa *UDART* waendele kulipa fedha kwa mujibu wa utaratibu wa sheria tuliyopitisha ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aingilie kati. Asiruhusu huu mkanganyiko ukaenda kwa sababu hii ni sheria na tuliipitisha ndani ya Bunge. Hatuna sababu ya kuingiza mkanganyiko wowote, hasa kwenye taasisi mbili ambazo ni za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kwa sababu ya muda ni *NeST*. Tunakubaliana hapa, tulipitisha sheria wenyewe ndani ya Bunge mwaka 2023 mwezi wa 10. Sheria ambayo waliileta watu wa *PPRA* kupitia Wizara ya Fedha. Hatuna shaka juu ya utekelezaji, kwa sababu kiukweli inakwenda kusimamia utaratibu mzuri sana wa uratibu wa fedha zinazotumika kwenye maeneo ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria bila kuendelea kutoa elimu haitusaidii sana. Nichukue nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, aliona umuhimu huo akaunganisha semina ya Waheshimiwa Wabunge, Wakurugenzi, pamoja na watu wa *PPRA*, lakini bado tunaamini, kwa kuwa sisi tulipitisha sheria, *PPRA* wakaenda wakatengeneza kanuni na mwongozo, waende kwenye halmashauri zote na kwenye taasisi zinazotumia mfumo huu, watoe elimu ili angalau miradi ya maendeleo isiendele kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa tuliyoiona kwenye miradi ya maendeleo, ni kwa sababu, ucheleweshaji mwingi ni kwa sababu ya mfumo. Wakurugenzi wanatangaza, hakuna wazabuni, na wakati mwingine hakuna mafundi. Unakuta maeneo mengine elimu ya kuutumia mfuko wenyewe kwa wale wanaotakiwa kutangaza, hasa walimu wa shule za msingi na sekondari, hauko *stable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba watu wa *PPRA* kupitia Wizara ya Fedha (watu wa Hazina), wakazunguke maeneo yote watoe elimu, na ikibidi panapobidi wapitie upya kanuni pamoja na mwongozo mliotoa. Kwa sababu haiwezekani, Mheshimiwa Rais anapeleka fedha nzuri sana kwenye maeneo hayo, miradi inachelewa kwa sababu ya mfumo tulioutengeneza sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezi kutusaidia sisi kama nchi, kwamba tumetengeneza mfumo mzuri, na Mheshimiwa Rais anapeleka fedha, halafu sababu inakuwa ni mfumo unaotuchelewesha, miradi inashindwa kuanza kwa kutimiza malengo na dhamira ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu wa *PPRA* warudi, waweze kuona namna ya kupitia ule mfumo, na watoe mwongozo na kanuni ili angalau hili jambo lisiweze kujirudia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Chege. *NeST* bado ina tatizo kubwa sana kwani bado inadukuliwa. Kuna watu ambao wanadukua kiasi kwamba wengine wanaotaka ku-*submit* zile

*tender* zao hawawezi. Kwa hiyo, mtandao huu bado una matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo na ndiyo maana tumeendelea kusisitiza kama Kamati, na hata sasa hivi tunaendelea kusisitiza kama Wabunge. Hatuna shida na sheria tuliyoiunda sisi wenyewe, lakini shida ni elimu ambayo inatolewa na ndiyo inatusababishia miradi mingi ya maendeleo kukwama kutekelezwa kwenye maeneo haya ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya, niendelee kusema tena naunga mkono taarifa ya Kamati zote mbili. Ahsanteni sana, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege. Nilimtaja Mheshimiwa Mrisho Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kamamba na Mheshimiwa Saashisha wajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nashukuru sana kwa kweli kwa kupata fursa ili niweze kuchangia Wizara yetu ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache sana. Jambo la kwanza ni kuhusiana na ujenzi wa stendi ya Jiji la Arusha, na bahati nzuri, toka nimekuwa Mbunge nimeweza kuuliza maswali mara tatu yanayohusiana na ujenzi wa stendi hii. Swali la kwanza niliuliza tarehe 14/04/2021, nikauliza tena tarehe 04/09/2023 na tarehe 31/10/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, nilikuwa natamani nisome majibu ya Serikali kuhusiana na ujenzi wa stendi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa tarehe 14 mwezi wa Nne, 2021 majibu ya Serikali yalikuwa yanasema hivi, naomba niyanukuu kutokana na *Hansard* tuliyokuwa nayo:-

"Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Jiji la Arusha imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 30 katika eneo la stendi mpya itakayojengwa, itazingatia pia mahitaji ya wafanyabiashara wadogo kama machinga, stendi ya *taxi,* pikipiki, bajaji, ofisi za Polisi, Usalama Barabarani na maeneo ya huduma mbalimbali. Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayoendelea sasa ni taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa mradi huo. Mradi huo wa ujenzi wa stendi ya kisasa Jiji la Arusha utajumuishwa kwenye mradi wa uboreshaji miundombinu *(Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC))* utakaotekelezwa kwenye halmashauri 45 za Majiji, Manispaa na Miji nchini ambapo Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yalikuwa ni majibu ya Serikali ya tarehe 14/04/2021 ambayo yalituahidi kwamba mradi huu unakwenda kutekelezwa. Nikauliza swali tena tarehe 04/09/2023 na Serikali yetu ikaweza kutupatia majibu. Majibu ya Serikali yalikuwa ni kama ifuatavyo, na ninaomba ninukuu pia.

"Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mradi wa kuboresha miundombinu katika Majiji, Manispaa na Miji *(TACTIC)* awamu ya pili itatekeleza ujenzi wa stendi kuu ya kisasa ya mabasi katika eneo la *Bondeni City,* masoko mawili pamoja na bustani moja ya mapumziko kwa lengo la kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Jiji la Arusha na maeneo ya jirani. Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu imekamilika na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata mzabuni zinatarajiwa kukamilika mwezi Desemba mwaka 2023. Baada ya taratibu hizo kukamilika, utekelezwaji wa ujenzi kwenye maeneo yaliyoainishwa utaanza."

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Desemba, 2023 taratibu zitakamilika na ujenzi wa stendi utaanza. Hata hivyo, kwenye swali la nyongeza pia Serikali iliweza kutujibu, naomba ninukuu pia.

"Mheshimiwa Spika, kwanza, lini tunatangaza *tender* hiyo, kama nilivyosema, tupo kwenye hatua za utaratibu wa manunuzi na siwezi kuwa *certain* sana kusema lini, lakini Serikali tunahakikisha tu kwamba *by December* mwaka huu, yaani mwaka 2023 tutakuwa tumekamilisha taratibu zote za manunuzi na mkandarasi kwenda *site* kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu. Mheshimiwa Spika, pili..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii ya pili niiache kwa sababu haihusiani na stendi. Nikaja tena nikauliza mara ya tatu tarehe 31/10/2024, naomba pia nisome majibu ya Serikali.

"Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafanya upembuzi yakinifu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifanya 2023 ikamaliza, ikatuahidi, mkandarasi mpaka leo hajafika, lakini anatujibu tena hapa:-

"Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, na usanifu wa kimazingira katika eneo la *Bondeni City,* zabuni ya ujenzi wa stendi hii ikatangazwa tarehe 19/01/2024 (mwaka jana) kupitia mfumo wa *NeST* na hatua iliyofikiwa ni ya upembuzi *(due diligence)* kwa wakandarasi waliopendekezwa ili zabuni itolewe kwa mkandarasi atakayekidhi vigezo kwa utekelezaji. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mpango uliopo tathmini ya mradi imefanyika na kukamilika Julai, 2024, hatua ya kusaini mkataba itafanyika na ujenzi unatarajiwa kuanza ifikapo Januari, 2025."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la nyongeza wakatujibu tena, naomba ninukuu: "Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna uhitaji mkubwa wa stendi ya kisasa katika Jiji la Arusha eneo la *Bondeni City* na tayari Serikali imeshatangaza zabuni na imeshapata mkandarasi ambao waliomba. Hatua iliyopo sasa ni ya kufanya uhakiki wa maana *(due diligence)*.

Naomba tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini kwamba mpango wa Serikali ni kuanza ujenzi mapema iwezekanavyo Januari, 2025 na mkataba utasainiwa wakati wowote kati ya Novemba na Desemba mwaka huu 2024." Majibu yapo mengi naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niiulize Serikali, Desemba 2023 imepita, Januari 2025 imepita, leo tupo Februari, 2025. Ukienda pale Arusha eneo la *Bondeni City* ardhi ipo eka 30 na hati ipo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kafanya kazi kubwa ya kutuletea mradi wa *TACTIC* ili stendi iweze kujengwa katika eneo lile. Sasa hawa wataalamu wanaohusika na taratibu za manunuzi, kumpata mkandarasi ili aweze kwenda *site,* watuambie tatizo lao ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wa TAMISEMI yupo hapa ambaye sisi hatuna mashaka na usimamizi wake, nataka tujue kwamba mbona katika halmashauri nyingine na majiji mengine *tender* zimetangazwa, wakandarasi wamepatikana; kuna changamoto gani kwenye Jiji la Arusha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mtu anakwamisha, analeta uzembe, kwa nini Serikali haichukui hatua, kwa sababu lile ni Jiji la Kimataifa? Mheshimiwa Rais, kafanya kazi kubwa, kaleta pale *Royal Tour*, utalii sasa hivi umerudi katika mahali pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, kafanya kazi kubwa, ameleta pale wageni, mikutano kila siku na mji umechangamka. Ni aibu kutokuwa na stendi ya kisasa. Kwa hiyo, naomba Serikali ituambie katika haya majibu matatu waliyonipatia hapa Bungeni, lipi ni jibu la Serikali ili niweze kulichukua niweze kuwapelekea wananchi wenzangu katika Jimbo la Arusha Mjini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrisho Gambo. Nilimtaja Mheshimiwa Aloyce Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga wajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze Mwenyekiti wetu kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupitishwa na Mkutano Maalum kuwa mgombea pekee wa Chama Cha Mapinduzi, na Dkt. Nchimbi kuwa mgombea mwenza. Nawapongeza sana, na sisi Kakonko wametutendea makubwa, tunasubiri tu tarehe maalum tuweze kulipa deni letu kwa kumpigia kura za 'Ndiyo' Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mambo ni mengi, nitachangia mambo machache na eneo ambalo nitachangia sana ni ajira ya walimu. Naipongeza sana Serikali kwamba imefanya kazi kubwa ya ujenzi wa madarasa, ujenzi wa nyumba za walimu na kadhalika, lakini haijafanya kazi kubwa ya kuajiri walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa madarasa, uwepo wa nyumba za walimu, kwa hoja yangu ni mapambo. Kwangu mimi ninachoona ni muhimu kwa ajili ya utoaji wa elimu ni upatikanaji wa walimu. Napongeza sana kwamba kuna juhudi zinafanyika na usaili unafanyika, lakini usaili huu unafanyika kwa walimu waliomaliza mafunzo ya ualimu karibu miaka 10 iliyopita, lakini unafanyika sambamba na Mwalimu mwingine aliyemaliza masomo yake mwaka 2024 (mwaka jana), hii siyo sawa. Kwa hiyo, ninachoshauri, Serikali iajiri walimu. Narudia kusema, Serikali iajiri walimu. Nirudie tena nasema kwamba, Serikali iajiri walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ukweli kwamba walimu hasa katika shule za msingi hali siyo njema. Nawapongeza walimu kwamba unakuta wakati mwingine wapo walimu kwa 50% lakini wanafaulisha kwa 80%. Maana yake ni kwamba hawa walimu ambao ni wachache, wamelazimika kufanya kazi ya ziada ya walimu ambao hawapo. Nawapongeza sana walimu wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa usaili unafanyika na tuliwashawishi walimu kwamba someni sisi tutawaajiri, na bado tukawapelekea fedha za mikopo lakini sasa wana miaka 10 nyumbani, naiomba sana Serikali sasa ifanye kazi ya ziada, iwaajiri hao walimu hasa wale ambao walianza masomo na wakamaliza mafunzo siku nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katikati nadhani ilikuwa mwaka 2024, Wabunge walishauri kwamba kwa kuwa walimu wengi wapo mitaani, ni vizuri tuanze na wale walimu walioanza siku za nyuma. Hii itapendeza kwamba wale walioanza wa awali wawe wa kwanza kuajiriwa. Tunao walimu wa mwaka 2015, 2016, na 2017. Kwa nini wasianzwe hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia hata sisi Wabunge kuwa na majibu sahihi kwa wananchi wetu. Muda mwingine unaombwa Mbunge, usaidie kupata ajira, lakini muda mwingine huna jibu sahihi. Tungekuwa na uhakika kwamba waliomaliza labda 2015 au 2016 watakuwa wa kwanza kuajiriwa, hii itatusaidia hata katika majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nirudie kushauri kwamba tuanzie kule kwa wale walimu walioanza 2015 au 2016. Pale tutakapoishia ajira nyingine ikiingia tutaanzia pale ambapo tuliishia kuendelea mbele. Kutokuwaajiri walimu hawa wakati huo wana mkopo, lini sasa fedha hizi za Serikali zitarudi? Maana yake kama walimu tumewapa mkopo, hawajaajiriwa, uwezekano hata wa kupata mkopo maana yake hizo fedha ambazo tuliwapa siyo rahisi kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana walimu hao ambao walianza mapema waajiriwe na fedha ambayo Serikali iliwakopesha iweze kurudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kwenye eneo la kuwarudisha vijana ambao waliacha shule za sekondari kwa sababu mbalimbali. Wapo watoto wa kike ambao waliacha shule kwa sababu ya ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa nafasi tena kwa vijana hawa, lakini shida iliyopo kwangu, naona kwamba ni shida kwa sababu wameangalia tu watoto wa kike, lakini hawaangalii watoto wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa kiume kuna uwezekano mkubwa wakawa na changamoto nyingi. Hawa ndio wanaofanya biashara stendi, hawa ndio wanakwenda kwenye uvuvi, hawa ndio wanaokwenda kwenye kuchunga ng'ombe lakini hawajapewa nafasi sambamba na watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, nafasi inayotolewa kwa watoto wa kike itolewe vilevile kwa vijana wetu wa kiume. Hawa watoto wa kike ambao tayari wana Watoto, unamrudisha shuleni, alikuwa peke yake, sasa ana mtoto, akienda shule huyu mtoto anamwachia nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwe na uangalizi wa ziada kuona kwamba ni kwa kiasi gani tutamsaidia huyu binti ambaye ana mtoto, lakini anarudi shuleni. Hiyo iende sambamba na kuwatafuta waalimu maalum wa kuja kuwasaidia hawa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana wetu walikuwa na changamoto peke yao, sasa wana Watoto, kwa hiyo, inafaa kuwe na uwezekano wa kuwa na walimu maalum wenye saikolojia ya watu wazima, wanaojua changamoto mbalimbali

zinazowakabili ili kuweza kuwahudumia hawa watoto na vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa sababu ya muda, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Kamamba. Nilimtaja Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga wajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba za Kamati hizi mbili ambazo zipo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mahususi kwenye hoja iliyopo Mezani, ninaomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mchengerwa yupo hapa. Tuna mradi wetu wa Soko la Kwasadala, humu ndani kama ni kurudia, nadhani nimeshasema zaidi ya mara 10. Sasa hivi wapo Arusha wamejifungia wanafanya marekebisho madogo, nisaidiwe kusukuma tuanze kujenga soko hili la Kwasadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni sambamba na soko la Mula na lenyewe walishatangaza mkandarasi amepatikana, lakini nimeambiwa kulikuwa na changamoto za kitaalamu, na lenyewe nisaidiwe kusukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni yale maombi maalum niliyompelekea Mheshimiwa Waziri yanayohusu shule chakavu 77. Nashukuru ameanza na Nalutu na nyingine lakini naomba tusaidiwe sana ni hizi shule zimejengwa muda mrefu. Watoto wetu karne hii kukaa kwenye shule chakavu ndani ya Jimbo la Hai, jimbo la mjini, siyo heshima. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimekuwa nikisema hapa kwamba ile mikopo ya 10% ya halmashauri tumefanya

marekebisho ya sheria kuingiza kundi la vijana na kuongeza umri kutoka miaka 30 mpaka miaka 45. Naomba sana, kwa kuwa Mama anazo fedha za kutosha, safari hii hebu tufunge macho tuongeze na kundi la akina baba, nao wakopeshwe. Hii 45 ukiangalia umri uliobaki ni kidogo sana, tufungue na wanaume wote waweze kukopeshwa. Nilishasema tena hapa, wanaume wengi wanapata matatizo ya kisaikolojia kwa kukosa hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie moja kwa moja kwenye mchango wa Kamati yangu ya TAMISEMI. Mimi ni Mjumbe wa Kamati hii na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu mjanja, anatusaidia tunaweza kutekeleza majukumu yetu vizuri. Nampongeza sana Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na wasaidizi wake wote. Wameweza kutupa nafasi, tumetembea karibu mikoa yote Tanzania na Halmashauri zake. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mpo vizuri kwenye majimbo yenu, tumepita huko, kazi imefanyika, majengo yamejengwa, barabara zimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani wananchi huko wanasema kile ambacho kimefanyika kwenye Mkutano Mkuu wa CCM, hivi hakuna namna nao wakaitwa mahali ili waseme Rais wao ni Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi siku ya Ijumaa nilikuwa kwenye ziara pale Rundugai, *clip* ninayo, mwananchi mmoja akasema, Mheshimiwa Mbunge huna namna ya kushawishi nchi yote tukae sehemu moja na sisi tutoe azimio, tuseme Mama Samia, tumemaliza hiyo kazi? Kwa hiyo, nilitaka niwaambie, Watanzania wapo kule wanatusubiri tupeleke jina la Mama Samia, wakamalize shughuli yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa niwapongeze sana akinamama Wabunge mliopo humu. Huu moto mliouwasha humu ndani, niwape taarifa umehamia kule nje. Akina mama wanasema safari hii tumepata Mama mwenzetu, tunataka tuwafundishe Watanzania akina mama wanaweza. Kwa hiyo, na

akina mama kule mtaani wanasema, "sisi tunatembea na Mama Samia Suluhu Hassan." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa taarifa yenu na sisi wababa tulishasema zamani, huyu ni mama yetu, hatuna wasiwasi, wababa tupo hapo nyuma yenu. Akina mama kuna msemo zamani ulikuwa unasema eti, akina mama hawapendani, lakini safari hii si tumeshauvunja! Akinamama wanapendana kuanzia huku Bungeni na kule nje na sababu tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona treni hapo, tunapanda treni kama tupo Uturuki. Tunatoka Dar es Salaam, asubuhi tupo hapa. Tunaona Bwawa la Mwalimu Nyerere, Naibu Waziri Mkuu ametuambia hapa linakabidhiwa muda siyo mrefu, tunaona majengo kila mahali. Hivi Watanzania tunataka nini? Huyu mama tunataka tumpe nini? Huyu mama anatudai, na haki yake ni kura za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo madogo. Makubwa yalishafanyika. Haya ninayotaka kueleza ni madogo tu na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aelewe, ni madogo madogo, makubwa yameshafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasubiri kwenda kumaliza kazi. *TARURA* amesema Makamu Mwenyekiti wetu mchangiaji wa kwanza, sisi tunamwomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, kazi kubwa ilishafanyika, aachilie fedha kwenye eneo hili, kazi ikakamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu barabara zimechongwa za kutosha kwa kweli, lakini sasa kuna changamoto wakandarasi wameanza kukimbiza, hawapewi fedha, na sisi tunamsemea Mheshimiwa Waziri wetu wa TAMISEMI, anajitahidi sana. Niseme kwamba Wizara ya Fedha hebu ijitahidi itoe hizi fedha kazi ikafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine hapa, tulipata mafuriko, nami nikapata mafuriko kule kwangu. Daraja la

Mkwarungo halipitiki, madaraja mengine kule Sonu, wananchi wanalalamika. Tunaomba fedha zile za *TARURA* ambazo ni shilingi bilioni 443 zilizopangwa ziende zote. Zimepelekwa shilingi bilioni 92 badala ya shilingi bilioni 443. Hizi fedha zilizobaki, au nimsindikize Mheshimiwa Mchengerwa twende wote pale Hazina tukakae hapo. Sasa naomba sana, tafadhalini sana, hizi fedha ziende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mahsusi niseme pale kwetu Hai, ardhi imekuwa ni ndogo sana kiasi kwamba tunayoitegemea kiwango kikubwa ipo kwenye mashamba ya ushirika. Naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, waitazameni Wilaya ya Hai wakijua haina ardhi kubwa, ardhi imekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maeneo ya ushirika yaliyopo pale ni kwa nini tusiyaweke kwenye Mfumo wa *PPP,* kama ambavyo tumefanya pale Karikoo? Tumefanya tathmini, *evaluation* ya ardhi, tukaithaminisha ile ardhi yetu, tukasema hii ardhi ni shilingi bilioni 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatafuta mwekezaji kwa Mfumo wa *PPP*. Tunamwambia njoo wewe na bilioni zako 13; za kwetu 13 za ardhi, za kwako 13 za uwekezaji, tunajenga hoteli. Pale mwisho wa siku kwenye *turnover* ya mapato tunagawana. Hiyo ndiyo njia sahihi ya kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara ya Kilimo kufanya utafiti, ni namna gani sasa Wilaya yetu ya Hai, yale maeneo madogo tunaweza tukayatumia, tukaweka mazao ambayo yanaweza kuongeza pato la Wananchi wa Jimbo la Hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba jambo hili ni mtambuka. Migogoro ya ardhi, na huu ni utapeli mwingine umeingia. Nasemea kwenye Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili Waziri alewe. Siku hizi limekuwa ni jambo la kawaida mtu kwenda Mahakamani, anachukua mmiliki ambaye

ni *fake* anamweka. Yeye anasimama upande huu, wewe unashangaa unaletewa *notice* unaondolewa kwenye eneo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sisi ni wahanga kwenye eneo hili. Nina watu wengi sana ambao wamenyang'anywa nyumba zao kwa namna hiyo. Watu ambao wamezeeka, wagonjwa, yatima, wajane na ambao wanaishi nje ya Tanzania, imekuwa ni utamaduni wa kawaida jamaa anaenda pale anatengeneza, anaangalia huyu mtu yupo Bunge, safari hii ana miezi mitatu yupo pale Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachokifanya ni nini? Anatengeneza mmiliki hewa, anaenda naye Mahakamani, kesi inakimbizwa haraka haraka, wewe unashaanga unaletewa *notice* ya kuondoka nyumbani. Hili jambo linaumiza Watanzania wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hizi zinazohusika zikae chini, ikiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ardhi na Katiba na Sheria, mtazame jambo hili. Wazee wengi wanakufa kwa kihoro kwa kuondolewa kwenye nyumba zao na matapeli walioko kwenye simu, siyo hao; wamehamia kwenye ardhi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema *NeST* siyo tatizo, tatizo ni watumiaji wapewe elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saashisha. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Godwin Kunambi, ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote, kwa kweli wametuwakilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuona kwamba, sasa ipo haja ya kuongeza mafao au marupurupu kwa walimu. Alilizungumza hilo juzi tu kwenye mkutano, walimu wameshaanza kuandaa maua yake. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais ameona kwamba, kweli walimu ni watumishi ambao wanatakiwa wapate mishahara ya juu kuliko watumishi wote katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo, nawaomba wale wanaohusika waanze kuchakata, kufikiria. Kwa sababu Mheshimiwa Rais amesema sasa wao, Utumishi, Wizara ya Fedha, waanze kufikiria ni namna gani wataongeza ili Mheshimiwa Rais atakapowaita wawe na majibu, wasianze tena kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nirudi kwa pongezi nyingine. Ni juzi tu kuna watoto walitekwa, wale wanafunzi wadogo, wakapatikana. Nampongeza sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza kwa kufanya kazi ile ya kishujaa kuwaokoa wale watoto. Ingawa kuna watu wengine wameanza kubeza, eti kwa nini waliwaua wale majambazi? Wangewapiga miguuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi wale majambazi wangerudi ndani mara moja na kufyeka wale watoto, hao Polisi si tungewafukuza kazi. Kwa hiyo, tuwapongeze, lakini tusibeze, tusilete mambo ya siasa. Wale watoto wameokolewa na wazazi wao wamefurahi. Namwomba sana huyo Kamanda wa Mkoa wa Mwanza aungane na makamanda wangine wakawatoe watoto wote, vijana wote waliotekwa ili wawapeleke kwa wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa hili la kwetu la *VETA*. Kuna *VETA* 64 mpya, mimi namwomba sana Waziri wa Fedha, mpaka sasa, hizi *VETA* zinatakiwa ziwe zimeshamalizika, lakini hivi ninavyoongea zinasuasua. Tulishawaambia wananchi huko, watoto wamejiandaa waende *VETA*, lakini bado hazijafikia kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, naomba unisikilize, *VETA* hizi 64 zinatakiwa ziishe. Sasa mimi ninaongea hapa jambo la msingi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu naona hapo sijui vipi? Naomba unisikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu hakikisheni hizi *VETA* zinakwisha. Wakati mwingine nashangaa, eti tunasema kuna *VETA* ya mfano. Kwa hiyo, hizi *VETA* nyingine ni za namna gani? Tunapojenga *VETA* sasa hivi zote ziwe *VETA* bora, kama ile tuliyoenda kuiona Kagera, *VETA* ya mfano, sasa hizi nyingine ni *VETA* za namna gani? Kwa hiyo, tunapofanya hiyo kazi, *VETA* zote ziwe na *uniformity,* zote zifanane ili kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, la *VETA* naona mmenielewa. Hilo la *VETA* limeeleweka, kwamba zijengwe kwa ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nije kwenye suala la madeni. Kuna viongozi wa vyuo vikuu wengine wamestaafu, wengine bado wapo kazini, fedha zao zote zimekaguliwa, lakini bado hawajalipwa mpaka leo. Mpaka nashangaa, jamani kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, hebu aende pale Utumishi akutane na Katibu Mkuu Utumishi, na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha. Siwafundishi kazi, lakini naomba hebu wakutane wamalize madeni haya ya hawa viongozi wa vyuo vikuu. Nilisema wakati fulani, hawa viongozi wa vyuo vikuu hawana kelele, na hawajui hata kulalamika, lakini tusichukue hicho kuwa ndiyo kigezo. Hebu tuwape stahili zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nije kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kuna watumishi walifanya kazi kipindi cha Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, walivyomaliza kufanya hiyo kazi walikuwa na kitu kinaitwa *HS (HandShake).* Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alisaini, hao ni wale Wakuu wa Wilaya. Sasa mpaka leo wale Wakuu wa Wilaya bado wanangojea zile fedha

zao ambazo waliahidiwa au zilishasainiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne. Hivi ni tabu gani inayofanya wasilipwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili nalo ni lake. Nilimwambia siku moja hapo vizuri, kwa upole, lakini leo nalisema kwa sauti. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, yaani mpaka wale watumishi wakajipa majina, wanajiita nyamakazi. Wanafanya kazi Wakuu wa Wilaya, hebu ile *handshake* yao muwape kwa sababu Mheshimiwa Rais alishaipitisha. Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia, analijua hilo, wala hana shida, ninyi hapo katikati kwa nini mnambwelambwela? Naomba mwasaidie hao Wakuu wa Wilaya ili waweze kutulia kule, waweze hata kufanya shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ukishamaliza, ukitoka hapa, kama huna shughuli nyingine ya kufanya, ukapewa ule mzigo wako, kidogo unaweza ukafanya kitu, lakini sasa hivi wapo kule nje masikini ya Mungu, wengine wala hata hawajui wafanye nini? Hebu Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Utumishi na Waziri wa Fedha, hakikisheni sasa hili suala la *handshake* ya Wakuu wa Wilaya linafika mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara. Nilimtaja Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi na Mheshimiwa Zacharia Issaay, ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunijalia afya na kuweza kusimama hapa kuchangia katika hoja hizi mbili. Nitajikita zaidi kwenye hoja ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI kwa wasilisho zuri, amewasilisha vizuri na hayo ni maoni ya Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kuhusiana na masuala ya kutoka katika mkoa Wangu, na hususan katika Jimbo la Tabora Mjini, ambako kazi kubwa na nzuri Mheshimiwa Rais ameifanya. Mimi nikiwa ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, nimeona kwa macho namna ambavyo fedha nyingi zimekwenda katika miundombinu ya shule, hospitali na zahanati, zimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, haina mashaka yoyote ya kupongeza kazi nzuri na kubwa ambayo inafanywa na Mheshimiwa Rais kwa kupeleka fedha kwa wananchi na fedha ile ikawa na tija kwa sababu wanapata kile wanachokistahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa shule, hospitali na miundombinu mbalimbali katika nchi hii, changamoto hazikosekani na katika changamoto, sisi kazi yetu kubwa ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Pale ambapo tunaona kuna upungufu tunaomba watusaidie, ili wale wananchi waweze kupata kile wanachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kuhusiana na Kituo cha Afya cha Maili Tano, pale Tabora. Kituo hiki cha afya majengo yake siyo rafiki sana kwa sababu yalikuwa yanatumika na wale waliokuwa wanatengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapotaka kusema kituo cha afya, nami binafsi ninayetembea katika nchi kuangalia vituo vya afya vinavyojengwa, pale Kituo cha Afya cha Maili Tano bado hakijakamilika kuitwa kituo cha afya japokuwa kinatumika. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri naye yupo hapa, watusaidie kwenda kupeleka majengo yanayotakiwa ili kituo hiki cha afya kiweze kukamilika kuitwa kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hakuna jengo la mochwari. Huwezi kuwa na kituo cha afya ambacho hakina jengo la mochwari. Hakuna jengo la mionzi wala hakuna jengo la wagonjwa wa nje, la *OPD*. Tunaomba sana Serikali iweze kupeleka majengo haya ili kituo hiki cha afya kiweze kukamilika na wananchi hawa waweze kukitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashukuru sana, tulikuwa na ukosefu wa jenereta, Serikali imeahidi kupeleka jenereta ndani ya mwezi huu. Nafikiri kuanzia tarehe 15, au 16 Februari, 2025, jenereta litakuwa limefika katika kituo cha afya pale. Wananchi wataendelea kupata huduma ambazo zinatakiwa kwa sababu ya changamoto ya kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatuna jengo la kufulia. Naomba sana majengo hayo yaweze kukamilika, kama ambavyo Serikali imekuwa ikiahidi ili wananchi wale wa Tabora, kile kituo cha afya ambacho kinahudumia wakazi wengi wa maeneo ya kata zilizoko karibu, waweze kupata huduma bora na stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa hizi shule za *BOOST* na *SEQUIP,* bado sisi katika Halmashauri yetu ya Tabora Mjini tuna changamoto ya shule chakavu, hususan za msingi. Tumekuwa na shule chakavu nyingi sana, na kauli ya Serikali wakati wote tunapokuwa tunahoji na kuuliza, wamekuwa wakitoa kauli ya kwamba, Halmashauri zifanye kazi ya kukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo Halmashauri zinazoweza kufanya hayo, lakini kuna Halmashauri, hususan sisi wenye Mikoa ya pembezoni, ukimwambia mtu akarabati shule zaidi ya 14 zilizochakaa, ambazo zimejengwa tangu wakati wa mkoloni, hawatutendei haki. Naiomba sana Serikali, pamoja na kazi nzuri inayofanyika ya ujenzi wa shule mpya, hizi shule chakavu nazo zikafanyiwe ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema na ninazungumza tena, shule zimechakaa kiasi kwamba zikija kudondoka maafa yatakuwa ni makubwa kuliko hata tunavyodhani. Nikikwambia

katika Jimbo la Tabora Mjini tu, kuna shule karibia 14 zimechakaa kweli kweli na zinahitaji ukarabati wa hali ya juu ili hata unapoweka majengo mapya, basi yaendane angalau na hali halisi ya maeneo husika, ili yaweze kupendeza na kuendana na hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna shule ambazo zina watoto wengi sana, wengi mno! Kuna shule moja pale Tabora Mjini inaitwa Majengo, ina jumla ya watoto 2,525. Katika shule hii wananchi wamejitahidi, kuna maboma ambayo wamejenga pale zaidi ya matano. Unaiambia Serikali ya Halmashauri iweze kusaidia kumalizia hayo maboma, tunapata wapi hizo fedha? Kwa kipato gani ambacho Halmashauri zetu za pembezoni wanakipata? Kwa hiyo, lazima ifike mahali waangalie na mapato.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa, Mheshimiwa Subira. Taarifa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mchango mzuri kabisa wa kizalendo wa Mbunge huyu, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, nampa taarifa kwamba, Shule ya Msingi ya Puma, Jimbo la Singida Magharibi, ina wanafunzi zaidi ya 2,000 mpaka inasababisha watoto kusoma kwa *shift*. Sasa kwa kuwa Waziri wetu mchapa kazi yupo hapa, najua atakapokuja kutoa hitimisho atazikumbuka shule hizi zinazotajwa na Mheshimiwa Mwaifunga na hii ya Puma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unaipokea hiyo taarifa, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga?

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake kwa sababu ni changamoto kubwa sana kuwa na shule yenye watoto wengi, halafu madarasa hayatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi shule tano hapa katika Manispaa ya Tabora, zina changamoto kubwa sana. Naiomba Serikali itusaidie; kwanza, iende ikaongeze madarasa; na pili, yale maboma ambayo yameanzishwa na wazazi katika maeneo hayo, wayamalizie, ili watato wetu waweze kusoma kwa raha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Waziri wa TAMISEMI yupo hapa, anaelewa hiki ambacho nakizungumza. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, pamoja na kazi nzuri na kubwa anayoifanya, lakini watoto hawa wa Jimbo la Tabora Mjini wanahitaji kupata elimu bora, na elimu bora ni pamoja na majengo ambayo wanasomea. Kama ambavyo Mheshimiwa Rais anapambana kujenga majengo mengine mapya, haya ya zamani yafanyiwe ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba pia, katika ujenzi wa hizi shule mpya ambazo zinajengwa, ziangalie uwiano na wingi wa watu kulingana na Sensa ya Mwaka 2022. Unakuta kuna maeneo mengine shule zinapelekwa, lakini uhitaji ni mdogo kuliko kwenye maeneo mengine. Maeneo mengine watu ni wengi sana, watoto ni wengi sana na wengine mikoa yetu watu tunazaa sana. Kwa hiyo, unakuta *population* ya watoto ni kubwa kuliko ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema leo katika Mkoa huu upeleke shule tano, huu upeleke shule tano, wengine unatuumiza kuliko wengine, wanakuwa wanapata zaidi kuliko tunavyopata sisi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nashukuru. Ahsante sana, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

Nilimtaja Mheshimiwa Godwin Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Margaret Sitta ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja za Kamati zote mbili. Pili, namshukuru Mheshimiwa Rais na nina sababu ya kumshukuru. Wapo watu wanauliza maswali. Kwa nini, Wabunge tunashukuru sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuwa ninayo sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais. Naomba Wabunge wenzangu tunaposhukuru tutaje na mambo aliyoyafanya kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mlimba na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, zimejengwa shule za sekondari tisa; mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mlimba na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, zimejengwa shule za msingi 16 mpya bila michango ya wananchi; mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mlimba na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, vituo vinne vya afya vimejengwa bila michango ya wananchi na vinatoa huduma, na hivi punde, tunatarajia kujenga pale na Kata ya Utengule. Sasa kwa nini, nisishukuru kwa mambo makubwa namna hii? Ninayo mengi ya kushukuru, lakini itoshe tu kushukuru hayo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye changamoto. Bado kuna changamoto kubwa mbili kwenye Jimbo langu na wananchi wa Mlimba wamenisisitiza sana niliseme leo. Changamoto ya kwanza ni sekta ya miundombinu, hasa barabara za *TANROADS* na *TARURA,* bado wananchi wa Mlimba wameendelea kusisitiza jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la maji, hasa Mradi wa Mlimba. Ule mradi sasa umesimama na Waziri wa Maji, kama yupo, au Naibu Waziri wanisikie. Mheshimiwa Rais alikuwa na nia njema Kata ya Mlimba kuwatua akina mama ndoo kichwani. Mradi ule una thamani ya shilingi bilioni 7.4, sasa umesimama yapata miezi sita. Najua Mheshimiwa Waziri wa Maji

anafanya kazi nzuri, nadhani katika hili ataenda kukamilisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni barabara. Hapa namshukuru Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na amekuwa balozi wa wakandarasi wa ndani. Wapo wakandarasi wanafanya vizuri, lakini wapo wakandarasi wanatuangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo nitatoa mfano, mimi Jimbo langu la Mlimba tuna barabara ya lami pale inayojengwa kuelekea Makao Makuu ya Halmashauri. Barabara hii ilisainiwa tarehe 22 Mei, 2023, Mkandarasi ni *Mell Construction Company Limited.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi huyu alipaswa akamilishe kazi hii ya tarehe 23 Januari, 2024 lakini mpaka leo yapata miaka miwili mkandarasi huyu hajafanya kazi ile na hana sababu, hadai chochote Serikalini. Sasa huyu naomba ni-*load formal complains* kwa *PPRA,* nipeleke maombi yangu kwa njia ya mdomo kwa *PPRA* na *CRB* kama wananisikia huko walipo. Hatuna sababu ya kuendelea kuwa na wakandarasi wa namna hii, wanaokwamisha kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri katika hili pia kwa upande wako uchukue hatua mapema leo hii, ikiwezekana hata leo mkandarasi huyu asimamishwe ile kazi apewe mwingine na watu waendelee kupata huduma pale Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninavyoenda kumalizia, nataka nitoe elimu kidogo kwenye sekta mbili; Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi hasa kwenye eneo mahususi la ardhi. Kwa kuwa, namfahamu Waziri wa Ardhi, sasa hivi kaka yangu Mheshimiwa Ndejembi ni *transformative*, ni kijana ambaye anataka mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiwa Wizara ya Utumishi na Utawala Bora, akiwa anamsaidia Mheshimiwa Mama Jenista, nilishauri hapa kwa habari ya upungufu wa *OPRAS*. Ninaamini alimshauri vizuri Waziri wake, Serikali ikafanya mabadiliko, ikaachana na Mfumo wa *OPRAS* ikaja na *PEPMIS* na *PIPMIS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naamini leo ni Waziri kamili wa Ardhi na ni *transformative,* atakwenda kupokea haya ninayosema leo. Nampongeza yeye, Naibu wake, kaka yangu Mheshimiwa Pinda, Katibu Mkuu, pia na Kamishna Mathew, wanafanya kazi kubwa kwa Watanzania. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa naye ni *transformative,* katika hili atanisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri bado kuna obwe kwenye usimamizi wa watumishi wa Sekta ya Ardhi. Nashauri watengeneze kanuni au waangalie marejeo kwa mujibu wa sheria. Leo hii, mfano Afisa Ardhi wa Mlimba anapewa kazi na Mkurugenzi wa Halmashauri kama ndio kiongozi wake wa karibu anayemsimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamishna anampa maelekezo. Kwa hiyo, ana mabosi wawili, anafuata lipi? Sasa kuna mkanganyiko hapa, lazima huu utatuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine, kama Taifa mpaka leo hatuna *National Land Use Master Plan.* Mpango kabambe wa matumizi bora ya ardhi wa Kitaifa na kwa kuwa Waziri wa Ardhi ameanza kufanya matukio ya Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995, ninaamini atakwenda ku-*accommodate* ninachokisema leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa ni lazima *National Land Use Master Plan* (Mpango Kabambe wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi), ardhi yetu, hizi kilometa za mraba 645,000 zingepaswa kuwa kwenye *National Land Use Master Plan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya jumla itengenezewe utaratibu wake, ardhi ya hifadhi itengenezewe utaratibu wake na ardhi ya vijiji itengenezewe utaratibu wake. Halafu kwenye Halmashauri huku, Halmashauri zote ziwe na *document* mbili; *Land Use Master Plan,* yaani Mpango Kabambe wa Matumizi Bora ya Ardhi na *Infrastructure Master Plan. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kazi ya Halmashauri, sasa hapa wanaingia Waziri wa TAMISEMI. Halmashauri zako nchini hazizidi 20 ambazo zina *Land Use Master Plan*. Ukienda Majiji yote ya Tanzania ukiacha Jiji la Dodoma, Arusha ni *squatter city,* Dar es Salaam *squatter city*, Mbeya na Tanga ni *squatter city. Why,* na katika hili hatutaweza kuondoa migogoro ya ardhi katika nchi hii, kwa nini? Kwa kuwa, hatuna hizo *document* za *Land Use Master Plan na Infrastructure Master Plan,* na inawezekana kwa kutumia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma tulifanya hayo kwa mapato ya ndani. Dodoma imepangwa kwa eneo lote, ila imepimwa kwa 70% na ilifanyika kazi hiyo kwa miaka mitatu. Inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu, kazi ya Waziri wa Ardhi kama Waziri wa Kisekta ni kusimamia hiyo *instrument* ya *Land Use Master Plan*, halafu yeye anayokaa nayo kama ana *remote control* hapa, anamwangalia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Namtumbo pale, je anafuata kilichoelekezwa na Wizara kama Wizara ya Sekta? Hana sababu ya kusafiri sana. *National Use Master Plan* ndiyo mwarobaini wa migogoro ya ardhi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Godwin Kunambi. Nilimtaja Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze wajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kwanza niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia siku hii njema sana kwetu na wakati huu muafaka kwa ajili ya kulihutubia Taifa letu, na pia kujadili masuala ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani nyingine ni kwa Rais na kwa Serikali nzima ya Awamu ya Sita. Kwa namna ya pekee Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa sana, kila mmoja ni shahidi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za miradi kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri na timu yake kwa sababu ukizungumza TAMISEMI pia ni dude. Nchi nzima ndiyo TAMISEMI. Kila uendako hutaiacha TAMISEMI usiikute. Napongeza Kamati zetu zote mbili kwa ziara kubwa ziliofanywa mikoani, maana yake ni kwamba, tumefanya kupima utekelezaji wa Serikali kwa muda ule wote wa mwaka mzima wa kibajeti ambao unaisha mwaka huu tarehe 30 Juni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kwanza athari kubwa ya ukosefu wa fedha katika sekta hii ya *TARURA* nchi nzima. Wakati tunaanzisha *TARURA* tulikuwa na barabara chache sana, tukaanzisha *TARURA*, tukapanga mpango wa kuwapa bajeti, barabara nyingi zikafunguliwa na *TARURA*. Sasa hivi wamezidiwa, hawana fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza 20%, baada ya miezi sita ya mwaka wa bajeti, tunaiomba sana Serikali, hiyo ni namna ya kuongeza fedha za *TARURA,* na zitolewe kwa wakati kwa jinsi ambavyo zimeombwa ili kusaidia barabara hizi ambazo ni unganishi kutoka kwenye Tarafa mbalimbali katika Majimbo yetu lakini kwenye Kata mbalimbali kuja kwenye Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Miji kwa ajili ya kuwaunganisha wananchi na huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango au hali halisi ipo pale Mbulu. Eneo la Mbulu Mjini tuna mradi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa anisikilize. Tuna mita 600 zimedumu karibu mwaka na zaidi sasa. Mradi huu wa mita 600 una barabara ya kiwango cha lami, lakini pia una daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umekuwa kero sana kwa wananchi wa Mbulu, yaani hasa wakati wa masika Mji unagawanyika pande mbili; upande wa pili na upande mwingine hakuna mawasiliano ya kuvuka kwa ajili ya kiungo hiki cha daraja na hakina lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wangekuwa wamelipa hawa wakandarasi kwa muda wa miezi yote waliyokaa, wangeshamaliza huu mradi wa meta 600, kwani ni mradi mdogo sana. Sasa huu ni mfano tu wa katikati ya mji, vijijini kule hutakwenda, barabara zote zilizofunguliwa na *TARURA* zimekuwa na hali mbaya sana kutokana na matokeo ya mvua, na pia mvua za El Nino na baadaye masika yalipokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwamba, timu ipite nchi nzima itazame upya, ilipe madeni ya wakandarasi ili warudi *site,* waweze kurudisha barabara zetu katika hali njema kwa sababu kila Jimbo tulikopita hata kwenye Kamati moja kwa moja barabara za *TARURA* zimekuwa na hali mbaya. Hali hii inasababishwa na upatikanaji wa fedha za bajeti ya kawaida na bajeti ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi uliopo Mbulu Mjini ni mradi wa fedha za Jimbo. Mradi wa fedha za Jimbo Mheshimiwa Waziri na timu yako ni mradi ambao Mheshimiwa Rais ameuanzisha mpango wa kila jimbo kuona sehemu gani muhimu sana utengewe fedha. Kwa sababu hiyo basi, mradi huu unapokaa wa mita 600 ndani ya miezi sita ama nane athari ni kubwa sana ya ucheleweshaji wa malipo kwa sababu baadaye tunaletewa bili ya ucheleweshwaji wa malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ambao unagharimu shilingi milioni pengine 600, kwa vyovyote vile katika ucheleweshaji na gharama za ucheleweshwaji unaweza ukaenda zaidi karibu ya shilingi milioni 800 ama shilingi bilioni moja kulingana na ucheleweshwaji. Angalieni athari ambazo tunapata kulingana na kucheleweshwa kwa *certificates* zisizolipwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hali ambayo siyo ya kawaida, kila mmoja au kila Mbunge katika Jimbo lake anajua kwamba athari za mabadiliko ya tabianchi imeleta hali mbaya sana ya maporomoko, makorongo na pia barabara nyingi kuharibika, na mwisho wa siku wananchi wanakosa huduma za kijamii za afya, elimu na huduma nyingine kwa ajili ya kutoka eneo moja kwenda lingine. Kwa hiyo basi, tunaiomba sana Serikali itazame upya eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni upungufu wa watumishi katika mamlaka ya *TARURA* ama wakala wa *TARURA* nchi nzima. Kila tulipoenda, upungufu umekuwa mkubwa. Kila tunapokaa kwenye mabaraza yetu na pia katika maeneo yetu, upungufu wa watumishi hawa ni mkubwa sana. Ombi langu ni kuwa, angalau tuanze kupunguza idadi hiyo ya upungufu wa watumishi katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuzungumzie suala zima la upungufu wa watumishi hawa kwa sababu kadri ambavyo kazi zinachelewa, ufuatiliaji unakosekana na watumishi ni wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine naomba nimkaribishe sana Mbulu Mheshimiwa Waziri Mchengerwa aone jinsi ambavyo athari tunaipata. Ametuahidi sana kwa muda mrefu pamoja na maeneo mengine, aone jinsi ambavyo tuna hali mbaya ya miundombinu ya barabara ya *TARURA*. Kwa sababu hiyo, tatizo hilo halipo kwake, ni nchi nzima na sisi tunaiomba Serikali fedha kwa ajili ya kufanikisha mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine ni ukamilishaji wa miradi viporo. Kamati yetu ilipotembelea nchi nzima, tumeona kumekuwa na miradi ambayo wananchi walianzisha kwa muda mrefu na sasa ni zaidi ya miaka nane hadi 10 kuna zahanati, kituo cha afya, nyumba ya mwalimu, jengo la ofisi ya kijiji na mambo kadhaa. Nguvu hizi za wananchi zinakosa kutoa huduma kwa sababu ya muda, lakini pia na fedha za umaliziaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni nini? Tunapopanga bajeti ya mwaka huu tutakaouanza, keshokutwa Serikali ione umuhimu mkubwa sana wa kutenga fedha kukamilisha miradi iliyoanzishwa na wananchi ili iweze kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi na ili tuweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Tunaishukuru sana Serikali, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi ilipata fedha awamu ya kwanza katika vyuo vya kwanza nchini tukafanya ukarabati na ujenzi wa majengo mapya. Mpaka leo ni miaka sita hatujapata fedha za kukamilisha yale majengo yaliyochakaa ambayo hayafai kwa matumizi pamoja na miundombinu mbalimbali inayohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa shule ya ufundi tunayoenda kuijenga kule Mbulu, lakini chuo kile tusipotenga fedha hali itakuwa mbaya sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, kwa sababu ya hali hii tunayoiona, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, naiomba Serikali, jambo hili la usaili wa vijana waalimu limeiathiri sana familia zetu kwa sababu wazazi wanatoa fedha vijana wanaenda kwenye usaili, lakini nafasi ni 100, wanaoitwa ni 1,000 na mwisho wake watoto wanarudi nyumbani hawajafanikiwa. Kama mwalimu aliandaliwa kuwa mwalimu, jambo hili halina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mamlaka yako na kwa ushauri wa Bunge hili, tuondoe suala hili la usaili kwa waalimu. Wote tulioko hapa, tupo hapa tumefundishwa na Walimu wa *UPE*, wengine leo ni Madaktari, Maprofesa, wenye *degree,* lakini mjue kwamba waalimu ndio waliotufikisha hapa. Aliandaliwa kuwa Mwalimu, kama kuna sababu ya usaili, basi tukafanye usaili kwenye vyuo vyetu kama kweli hao waalimu hawajaandaliwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wanafunzi kuitwa 1,000 kwa nafasi 100, vijana wamepigika mikopo waliyokopa wakati wanasoma vyuo, haijalipwa. Saa hizi wanakopa tena nauli ya kwenda kwenye usaili siku tatu, nne mpaka wiki. Nadhani jambo hili kwa namna ya pekee wazazi wameumia. Tunaiomba Serikali itazame upya, iondoe suala hili la usaili kwa waalimu ili walimu wetu waende kwenye ajira kwa namna ambavyo itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%, naomba tuendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilimtaja Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Nashon, na Mheshimiwa Hamisi Taletale ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo Mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, pia nawashukuru wananchi wa Urambo kwa jinsi ambavyo wananipa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara ambayo inasimamia shughuli zote za TAMISEMI kuanzia Waziri mwenyewe, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote, na Wakuu wa Idara wote, wanafanya kazi kubwa. Hii Wizara ina kazi nyingi sana, tunawaombea kila la heri ili kazi ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nichukuwe nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu kwa kazi kubwa aliyofanya. Kwetu Urambo kama alivyofanya kwingine, tumepata shule nyingi za msingi, za sekondari, na tumepata hospitali. Kwa kweli tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijikita zaidi sasa hivi kwa upande wa elimu, kwa kweli kutokana na wingi wa shule tulizopata mpya, tunahitaji waalimu wengi zaidi kama walivyosema Mwenyekiti wetu ambaye nampongeza, amesoma kwenye taarifa yake kwamba tunategemea kupata waalimu zaidi ya 500. Sasa hivi tunao waalimu 273,736, lakini kutokana na taarifa niliyoisikia leo, tunategemea kupata zaidi ya 500,000 kutokana na wingi wa shule zilizojengwa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wingi wa waalimu, Serikali ilidhamiria tangu mwanzo kwamba kutokana na idadi kubwa ya waalimu lazima wawe na chombo kinachohudumia waalimu na ndiyo maana wakaja na *Tanzania Teachers Service Commission (TSC)* ambayo ilianzishwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sheria yao ambayo ninayo hapa, Kifungu cha Tano kuanzia (a) mpaka (l) ni majukumu ambayo wamepewa *TSC* pamoja na kuajiri, kusambaza, kuwapa mafunzo. Walijua kwamba idadi hii kubwa, inahitaji chombo maalumu cha kuwahudumia, ndiyo wakaunda *TSC* na ikawapa majukumu makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, je, Serikali ilikaa na kutathmini kwamba hiki chombo kikubwa walichokiunda kinafanya kazi iliyokusudiwa? Nina wasiwasi sana, kama tathmini haijafanyika, tuiombe Serikali ifanye tathmini ya chombo hiki, kwani ni kikubwa lakini utashangaa, sehemu nyingine kuna Ofisa wa *TSC*. Sitaki kutaja hapa, lakini ukinibana naweza kukutajia. *TSC* maeneo mengine yanakuwa na wafanyakazi wawili, au mmoja. Kweli inatimiza wajibu iliyopewa kutokana na sheria hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoa wito kwa Serikali, wafanye tathmini ya chombo hiki ambacho ni muhimu sana kutokana na idadi kubwa ya waalimu waliopo na idadi kubwa tunayotegemea kupatikana kutokana na Mheshimiwa Dkt. Samia alivyofanya ya kuongeza shule nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nataka waangalie kama majukumu yanatimizwa, pia waangalie hasa wanavyopeleka watendaji kazi kwenye Wilaya wanafanya kama ilivyokusudiwa? Kwa sababu ilitegemea kuwe na mtu wa *TSC* ambaye anafahamu vizuri sana masuala ya watumishi, halafu anayefahamu sana masuala ya waalimu na sheria pia. Je, wapo kama ilivyokusudiwa? Kama haikukusudiwa, basi waangalie waone jinsi gani tunavyoweza kuboresha *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia na idadi ya fedha, kiasi cha kinachopelekwa hakiendani na makusudio ya kuiunda hii *TSC*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kabisa, ili kweli wafanyakazi wafanye kazi vizuri; waalimu waliopo vijijini, waliopo mjini wafanye kazi vizuri, lazima wahudumiwe kikamilifu. Waalimu wengi wanalalamika kutokana na kutokupata haki zao kwa wakati lakini chombo hiki kipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti nataka niulize swali moja. Ukiangalia kwa upande wa afya, wale Makatibu Afya waliopo kwenye hospitali wanaangalia vyote, wanaangalia utumishi wa Madaktari, wanangalia upatikanaji wa dawa, wanaangalia kila kitu, lakini kwa nini yule Katibu wa *TSC* pale amebanwa? Kwa hiyo, nilikuwa natoa wito kwa Serikali kuiangalia *TSC* upya ili ifanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kwa mambo mengine. Pia namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia kwa jinsi ambavyo ametupa barabara kwa kupitia *TARURA*, *TANROADS*, na kadhalika, kwa leo nijikite zaidi kwa *TARURA*. *TARURA* inafanya kazi nzuri sana kutokana na viongozi wote, Mkuu wa Idara, watumishi wote na kadhalika, lakini fedha ndiyo shida. Tunaiomba Serikali yetu iwape fedha *TARURA* watengeneze barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru *TBC*, juzi ilitoa taarifa ya Urambo tena nikashtuka kweli, wakaonesha barabara zilizopo vijijini zilivyoharibika. Ahsanteni sana *TBC*. Sasa naiomba Serikali kwa kupitia Wizara hii ya TAMISEMI itusaidie fedha ziende zikatengeneze barabara za vijijini ambazo mvua imeharibu kiasi ambacho sasa hata kupeleka tumbaku sokoni au kupeleka mahindi na bidhaa nyingine itakuwa shida kwa sababu barabara hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naliomba kwa niaba ya wananchi wa Urambo mpaka sasa hivi, nadhani pengine tumebaki sijui Wilaya ngapi, sisi ambao Mkuu wa Wilaya yupo ndani ya Halmashauri ya Wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kuna Waziri alikuwa anajibu swali. naomba lile jibu alivyojibu akawapa matumaini wananchi wa Urambo kwamba tujengewe nasi Ofisi ya Mkuu wa Wilaya peke yake tena ya ghorofa, za kisasa na Ofisi ya Halmashauri ambayo ilijengwa mwaka 1974 ijengwe upya ili nasi twende na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nisingependa kumaliza kabla kulizungumzia ni suala la watumishi kudai haki zao. Imekuwa tatizo sasa hivi waalimu wakistaafu wanastaafu kabla hawajarekebishiwa madaraja yao na kwa msingi huo, hata kufanya mahesabu ya *pension* inakuwa ni vigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba wafanyakazi warekebishiwe mishahara yao kabla hawajastaafu ili waweze kupata *pension* wanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Sitta. Nilimtaja Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, Mheshimiwa Hamisi Taletale, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, ajiandae.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa nafasi hii uliyonipa. Kabla ya yote, naomba niwashukuru Wenyeviti wote wa Kamati zote mbili kwa uwasilishaji mzuri walioutoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuteuliwa au kuchaguliwa kwa kura nyingi na Chama Cha Mapinduzi ili kuweza kupeperusha bendera kwa Uchaguzi Mkuu huu wa Mwaka 2025; na kwa kumteua Dkt. Nchimbi kuwa Mgombea Mwenza. Tunayo imani kubwa atakwenda kutupatia ushindi Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kuteuliwa kuweza kupeperusha bendera kwa ajili Urais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda, naomba niende kwenye eneo moja ambalo kwa kweli naona kama bado kuna shida. Naomba kuipongeza Serikali chini ya Mheshimiwa Rais wetu kwa kuweza kujenga shule nzuri za sekondari na kwa kuweza kujenga vyumba vya madarasa katika shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yale maeneo ya shule za msingi yaliyojengwa vyumba vizuri vya madarasa, yako madarasa mengine ambayo ni yale ya zamani. Sasa unaweza ukaona kwamba ni kama kumekuwa na ubaguzi kidogo. Wanafunzi wangependa kutumia vile vyumba ambavyo ni vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niishauri Serikali, irudi kwenda kuangalia na kukamilisha madarasa ambayo yapo ni mazuri, mengine ni katika shule zile ambazo ni za zamani kabisa ambazo sisi tulisoma kule, ambazo bado hazijaangaliwa. Naomba sana niliseme hilo kwa sababu linaleta shida kidogo kwa wanafunzi. Pia kwenye miundombinu ya madarasa, sakafu na hata usafi wenyewe wa hayo madarasa, bado ni shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanapotoka huko kwenye shule za msingi, wanapokwenda sekondari ambapo kule wanakuta madarasa ni mazuri, sehemu ya kujifunzia ni nzuri na sehemu ya kukaa ni nzuri, basi wawe wameanzia huko chini. Ninayo imani Serikali yetu sikivu italiona hilo kwamba nalo ni muhimu liende kufanyiwa kazi, likiwa ni sambamba na vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye nyumba za walimu. Kule kwenye vijiji shule zilikojengwa kidogo afadhali, kwamba, vijiji vile vina nyumba kwa maana ya wananchi kuweza kuwakodishia walimu kwa maana ya kupanga. Sehemu ambayo shule shikizi zimejengwa ni maeneo ambayo kidogo yako pembezoni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule ambako wananchi wa maeneo yale, nyumba zao kwa kweli haziko katika hali nzuri, kiasi kwamba walimu hawawezi kupanga kwenye zile nyumba. Kwa kweli mazingira ni magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iwekeze kwenye eneo hili, ipeleke fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu ili walimu hawa waweze kufanya kazi katika mazingira yaliyoboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda kwenye shule moja, na shule ile ni shikizi ambayo sasa imeshasajiliwa. Shule ile imejengewa madarasa saba, lakini bahati mbaya hakuna nyumba za walimu, na pale ni sehemu ambayo wananchi wake ni watu wa hali duni kidogo ambao nyumba zao kwa kweli ni za hali ya chini sana. Walimu wamejiazimia vyumba hivyo hivyo ambavyo ni madarasa, wamekata *partition* ili waweze kujikimu katika kuishi. Sasa hiyo siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Mheshimiwa Rais, madarasa ni kwa ajili ya wanafunzi kusomea na walimu kufundishia. Sasa hilo likikaa hivyo haliwezi kuwa zuri, lakini wanafanya hivyo kwa sababu ya dharura na kwa sababu

hakuna nyumba za walimu. Naomba Serikali iweze kuliona hilo na hivyo ipeleke fedha kwa ajili ya nyumba za walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu *TARURA*. Unafahamu kabisa kwamba kwenye zile barabara za *TARURA* ndiko mazao yanakotoka. Sasa zisipotengenezwa vizuri, maana yake mazao hayawezi kutoka kule vijijini kuja mjini. Kwa hiyo, wananchi wale kila wanachokifanya kwa ajili ya kujikimu, kwa maana wamepata mazao yao, lakini yanashindwa kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, *TARURA* wameweza kujenga baadhi ya Barabara, lakini wameishia kwenye *culvert*. Sasa ni vema fedha ipelekwe ili kusudi ikamilishe eneo hilo. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamelalamika sana, nami nalalamika, naomba kwa kweli eneo hilo lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwenye Kituo cha Afya cha Nguruka. Mheshimiwa Waziri anajua, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda pale Nguruka. Aliona Kituo cha Afya cha Nguruka ni chakavu, na aliahidi kwamba Mheshimiwa Rais amekwisha ahidi shilingi milioni 500 pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize hili, Mheshimiwa Mchengerwa, peleke shilingi milioni 500 kwenye Kituo cha Afya Nguruka. Nimekutaja ili uweze kushtuka... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nashon.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naona umeshawasha *mic*. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamisi Taletale. Mheshimiwa Hassan Kungu na Mheshimiwa Mwantumu Zodo, mjiandae.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima siku ya leo. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuongoza vyema nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Yanga kwa suluhu yake ya jana. Najua kaka yangu Mwigulu atakuwa amefurahi angalau kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze na Wizara ya Michezo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwanza kwa kuileta hii sekta ya habari kwenye Wizara ya Michezo. Pia, kwa kutuletea Mheshimiwa Waziri ambaye ana taaluma ya michezo kidarasa, kaka yangu, baba yangu Mheshimiwa Prof. Mwaluko Kabudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kitu kikubwa sana kinakuja kwenye nchi yetu, hii Michezo ya *CHAN* na *AFCON*. Leo hii Uwanja wetu wa Arusha una 24%. Sijui Wizara mnatuambia nini kwenye hizi asilimia ilhali tayari michezo iko usoni? Mheshimiwa Rais ametoa fedha, lakini tunaanza kuona vitu vinasuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isimame ituambie, nini kinasuasua? Sisi kama Kamati tumeweza kuwasukuma, na *of course* tumeenda pale kwenye viwanja, lakini mpaka sasa hivi tuna 24%. Ukimwuliza Mheshimiwa Waziri, ametuhakikishia kwamba ndani ya mwaka huu tunakwenda kukamikilisha vile viwanja. Tumeona mashindano ya hapa katikati, yamepelekwa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Uwanja wetu wa Taifa wa Benjamin William Mkapa, yaani haujakamilika. Tukienda kwenye vyoo, juzi Prof. Kishimba alikuwa anazungumza, vyoo vya Uwanja wa Mkapa ni *Hip Hop* kama Naibu Waziri wake. Kwa hiyo, tuangalie, kama tunataka utaratibu wa kupokea watu, Mheshimiwa Rais anaonesha uwezo wa kutoa fedha kwenye

Wizara hii, lakini kama tunataka kubadilika, basi tuwe wepesi, tuipunguze ile hali ya pale Kiwanja cha Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea zaidi, naomba kwanza nimpe pole Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Wanasema, kufiwa na mzazi hakuna umri. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kaka yangu Aldolf Mkenda pole sana. Sisi kama Kamati na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla tunakupa pole kwa kuondokewa na mzazi wako. Pia hili liende kwa kaka yangu Mheshimiwa Tarimba Abbas. Nampa pole vilevile kwa kumpoteza mzazi wake. Kupoteza mzazi, hakuna umri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwenye sanaa. Leo hii unawaona wasanii wakiona kuna jambo la chama wanakuja wenyewe kwa gharama zao. Yote hii ni kwa sababu ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa yale ambayo ametufanyia. Mimi ni mmoja wa wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nizungumze, kuna begi limetoka, ninamaanisha fedha ambazo zipo kwenye mirabaha. Hizi fedha ni nyingi kuliko miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba fedha hizi zigawiwe haraka kwa sababu wasanii wanataka kuona na kula matunda ya Mheshimiwa Rais wao ambaye leo hii wanatoka kifua mbele kuja kumsemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kidogo...

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa kaka yangu Mheshimiwa Taletale,

anavyochangia mchango wake, ni mzuri sana. Kwa kweli sasa hivi wasanii wanajitahidi sana hasa wa Kimila, wa Kisukuma. Kwa hiyo, Serikali ione kila sababu ya kuwawezesha, maana wanaimba vizuri nyimbo za Mheshimiwa Rais na kwa kweli wanaipa *support* sana Serikali yetu. Nilitaka kumpa taarifa hiyo tu kwenye mchango wake.

**MWENYEKITI:** Unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Maganga?

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante babu yangu wa Kisukuma. Nimepokea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwa kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa. Leo hii tumepata matatizo ya mvua kwenye Kata yetu sisi ya Kiloka. Kuna Barabara ya Kiroka kwenda Mfumbwe daraja limevunjika tangu mwaka 2024 mwanzoni mpaka leo *TARURA* hawajasema chochote. Hali imekuwa ni mbaya. Ile barabara ilikuwa ndiyo chanzo cha watu kutoka kupishana kidogo na barabara yetu ya Bigwa Kisaki, lakini leo hii daraja limevunjika, hatuoni lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Elimu, kaka yangu Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda kwa kuniletea fedha ya kujenga shule ya sekondari na ufundi kwenye Kata yetu ya Tomondo, lakini kwenye hili tunaomba tupate walimu wa ufundi na vifaa ambavyo vitakwenda kuboresha kwenye ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa kifupi sana, tunaona mabadiliko kwenye sekta ya elimu na tunaiona dhamira yake Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Tunaona kabisa kwamba tunakwenda kwenye elimu ambayo kile alichokisema Mheshimiwa Rais wetu ndicho tunachokwenda nacho. Sasa basi, sisi changamoto yetu kubwa ni walimu. Kila mtu akisimama hapa ni walimu. Sasa hatujui walimu wapo TAMISEMI au wapo kwenye Wizara yetu ya Elimu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya machache, nami naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Hassan Kungu. Mheshimiwa Mwantumu Zodo na Mheshimiwa Deo Sanga, mjiandae.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie Wizara hizi mbili. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja za Wizara zote mbili, lakini pia nawapongeza Wenyeviti wote wa Kamati hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa katika Mkutano Maalum wa Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea pekee wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nataka nielekee kwenye eneo la michezo, lakini mwishoni kama muda utaruhusu nitagusia elimu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tupate maendeleo ya michezo nchini na duniani kote ni lazima tuwe na vitu vitatu. Jambo la kwanza ni miundombinu ya michezo kwa maana ya viwanja na kadhalika. Jambo la pili, ni kuzalisha wataalam watakaofundisha michezo, na jambo la tatu ni kutengeneza wanamichezo wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili, kwenye eneo la miundombinu ni lazima kama Serikali tuwe na mkakati madhubuti ambao utakuwa na *time frame,* ambapo tutaweza kuweka miundombinu nchi nzima. Kwa sasa tunao uwanja mmoja tu. Tunao Uwanja wa Taifa ambao umekidhi vigezo vya kucheza michezo ya Kimataifa. Tunaamini sisi sote uwanja ule uko katika ukarabati mkubwa ambapo unachukua takribani zaidi ya shilingi bilioni 31. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumefikia kule? Ni kwa sababu uwanja ule unakosa matengenezo ya mara kwa mara na unakosa ukarabati wa mara kwa mara. Ni lazima tuwe na mkakati, ama Wizara kupitia Serikali tutengeneze kitu ambacho kitaweza kuwa kinabakiza sehemu ya fedha inayopatikana kupitia ule uwanja ili sasa kukitokea kuharibika katika uwanja ule, basi ukarabatiwe kwa haraka *(retention)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefikia kukarabati kwa fedha nyingi kwa sababu ya kulimbikiza matatizo, kwa sababu fedha zote zinazoingia zinakwenda kwanza Serikali Kuu, *then* kukitokea uharibifu, inatakiwa liandikwe dokezo, nani asaini, nani asaini, nani asaini mpaka ije ipatikane hiyo fedha, tayari uwanja ule unakuwa umeshaharibika zaidi. Kwa hiyo, kuwa na *retention* ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kutengeneza wataalam wa kufundisha michezo, ni lazima tuweke mikakati ya kuwa na vyuo vya kutosha ambavyo vitafundisha michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa Mbunge alisema hapa, Chuo cha Malya kinakwenda kwa kusuasua. Chuo cha Malya ni mkombozi wa michezo Tanzania, kwa sababu, ndiyo chuo pekee kinachofundisha waalimu wa kwenda kufundisha michezo kwenye majimbo yetu na wilaya zetu. Kwa hiyo, ni lazima kiishe kwa haraka zaidi na hatimaye twende kuinua michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la wanamichezo, hili ni lazima lifundishwe shuleni, nyumbani na kwenye maeneo mengine. Ni lazima Serikali iwe na mkakati kama vile ilivyokuwa Serikali ya China. Serikali ya China imeweka mkakati. Tangu mwaka 2016 Rais wake alizindua mkakati ama programu ya michezo inayoitwa *The Fifty Point Plan*, ambapo *plan* yao ni kwamba ifikapo mwaka 2050 waweze kushiriki Kombe la Dunia la *FIFA* na waweze kutwaa lile Kombe la Dunia la *FIFA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika mkakati ule wamejiwekea mikakati kadhaa ndani yake. Mmojawapo, wamejiwekea mkakati wa kujenga shule 20,000 kwa ajili ya kufundisha michezo tu, hususan mpira wa miguu. Pia, wamejiwekea mkakati wa kujenga viwanja 70,000 ambavyo ni kwa ajili ya soka pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 2016 hadi mwaka 2020 tayari zile shule zimeshaanza kufundisha michezo. Wanalenga mwaka 2050 wacheze Kombe la Dunia na watwae ubingwa. Wamejiwekea hiyo *timeframe* ili waweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara, maana kupitia Wizara ya Michezo, tayari kuna mkakati wa shule 56 ambapo shule zile zinakwenda kujengwa kwenye kila mkoa shule mbili kwa ajili ya michezo. Je, kama Tanzania kwenye zile shule 56 tunayo *timeframe,* kwamba mwisho mwaka fulani shule hizi zitakuwa zimekamilika zote na zitakuwa tayari zimeanza kufundisha michezo hiyo?! Ni lazima tuwe na *timeframe*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikienda kwenye suala la elimu, ni kama ilivyokuwa tu kwenye michezo. Ili tuweze kuwa na maendeleo kwenye elimu, ni lazima tuwe na miundombinu ya elimu ya kutosha, tuwe na wataalam wenyewe wa kufundisha elimu yenyewe, kwa maana ya walimu, na ni lazima tuwe na watu ambao wanakwenda kupata ile elimu yenyewe, kwa maana ya wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la miundombinu, nampengeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli kwenye eneo la elimu sekondari tulikuwa tuna shida kubwa sana ya shule, lakini hivi sasa hakuna mwanafunzi ambaye anakosa kukaa darasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, upande wa elimu msingi nilikuwa naiomba sana Serikali, utaratibu ule ule uliotumika kwenye elimu sekondari, basi utumike na kwenye elimu msingi ili shule zetu ziweze kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuhusu wale wazalishaji ama wataalam wa elimu, kwa maana ya walimu, naipongeza Serikali, tumezalisha walimu wengi sana nchini, lakini baada ya kuzalisha walimu wengi nchini, je, tumewaajiri ili waweze kwenda kufundisha elimu sawasawa? Naomba walimu wa kutosha waajiriwe na shule zetu ziweze kupata walimu wa kutosha na hatimaye vijana wetu wapate elimu sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Kungu. Nilimtaja Mheshimiwa Mwantumu Zodo. Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha wajiandae.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kusimama mchana huu kuchangia hoja za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kuwa mgombea pekee wa Chama cha Mapinduzi, nafasi ya Urais mwaka 2025 kwa kura nyingi za kishindo alizopata kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwekeza na kujenga kwenye miradi mingi Tanzania; miradi mikubwa na miradi midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja zetu za Kamati hasa Kamati ya TAMISEMI. Kwenye

taarifa yetu ya Kamati, tumeeleza hoja nyingi, lakini moja kati ya hoja ambazo tumeeleza, mimi nitachangia hoja chache. Hoja ya kwanza kabisa ni kuhusiana na Shirika la Elimu Kibaha. Kwenye taarifa yetu tumeeleza vizuri dhumuni hasa la kuanzishwa kwa shirika hili ambalo toka zamani ilikuwa ni kuja kutoa elimu kwa ajili ya kuendelea na mapambano ya mambo matatu: umaskini, maradhi na ujinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya bado yapo, hayajaisha, lakini cha kusikitisha, Shirika hili lilikuwa linataka kuvunjwa. Hata hivyo, Kamati yetu ilimshauri Mheshimiwa Waziri, tunaomba hebu ajaribu kuangalia tena Shirika hili lisivunjwe, isipokuwa changamoto zilizopo kwenye Shirika hili zijaribu kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Mheshimiwa Waziri hoja hii aliichukua na ataifanyia kazi. Moja kati ya taasisi zilizopo kwenye Shirika hili ni pamoja na Chuo cha Afya Kibaha. Chuo hiki miundombinu yake ni chakavu sana, sana, sana. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anatokea Mkoa wa Pwani. Kwa hiyo, sina shaka anakijua vizuri sana Chuo hiki. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa yupo hapa, hebu atafute fedha ili wakafanye ukarabati kwenye Chuo kile cha Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo kile ni kati ya vyuo bora Tanzania, na wanafunzi wanaoomba kila mwaka kujiunga na chuo kile ni wengi. Wanaomba zaidi ya wanafunzi 5,000 lakini kwa kuwa uwezo wa Chuo bado ni mdogo sana kutokana pia na miundombinu, wanafunzi wanaochukuliwa pale ni 100, hivyo wanafunzi zaidi ya 4,000 wanakosa nafasi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atafute fedha kwenda kukarabati chuo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa chuo kile bado kipo TAMISEMI, bado hakijahama popote. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa TAMISEMI atafute fedha. Chuo kile kile bado kina eneo kubwa, kina ekari karibia 4,000, lakini kipo mjini sana. Ekari zile

4,000 ni pori. Kama ukipita pale Kibaha, ile stendi mpya, pori lote lile la kushoto ni eneo la chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lile ni *very prime*. Kwa hiyo, kwa sababu sasa zile hati hati za kufutwa kwa lile Shirika la Elimu Kibaha, hawajapata bado kibali cha kutumia yale maeneo yao, namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kukaa na kushauriana, Shirika la Elimu Kibaha wapewe kibali cha kutumia yale maeneo yao kwa sababu, kwa mfano kama lile eneo la mbele wanaweza wakatafuta wawekezaji na sasa hivi pia kupitia hii njia ya *PPP* wanaweza wakawekeza, kwani eneo lile ni *prime* sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nyuma ya chuo wanaweza wakatumia pia kwa ajili ya matumizi mengine na hata kwa baadaye sasa wanaweza wenyewe wakapata fedha yao kwa ajili ya kuendesha chuo na kufanya mambo mengine kama ukarabati mdogo mdogo wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Utumishi wa Umma, Hombolo kipo nacho TAMISEMI. Chuo kile nacho kina changamoto nyingi. Kwanza kabisa hakina watumishi wa kutosha. Pili, nyumba za watumishi; Kamati tulifaya ziara pale tulikuta nyumba ni moja tu ya *two in one*. Kwa hiyo, watumishi hawana makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, barabara ile ya kuingia chuo ni mbaya sana na barabara ile ni kilometa 24 tu. Kwa hiyo, namwomba pia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, na kwa sababu pia barabara ile nafikiri ipo *TARURA* na *TARURA* ipo TAMISEMI, hebu Mheshimiwa Waziri ajaribu kutenga bajeti kwa ajili ya barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kuna changamoto za chuo kile cha Hombolo. Chuo kile kinadahili wanafunzi zaidi ya 6,000 sasa hivi, lakini *capacity* ya *hostel* za chuo ni wanafunzi 1,200 tu. Kwa hiyo, wanafunzi wanaokaa ndani ya chuo ni kama 20%, 80% yote wanakaa nje ya Chuo. Kwa hiyo, niendelee pia

kumwomba Mheshimiwa Waziri kuwekeza nguvu kwenye Chuo kile hasa kwa ujenzi wa *hostel* na jengo la utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Zodo. Nilimtaja Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge na wa mwisho kwa wachangiaji ambao ni Wabunge atakuwa Mheshimiwa Kumba Ndulane.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona na kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wana-CCM wenzangu nchini Tanzania kwa maamuzi mazuri waliyoyafanya ya kumteua na kumchagua Mwenyekiti wetu na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumpa kura nyingi sana za kuongoza 2025/2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Wana-CCM kwa kumpa Dkt. Nchimbi kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kuwa mgombea wa Zanzibar 2025/2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wengine wanasema hamkufanya vizuri. Mimi nadhani nafasi zipo kule, sisi wana-CCM tumeamua kwa kauli moja. Wale ambao wanashauri vingine, vipo vyama kule bado havijateua, waende wakashauri huko. Sisi kwa kauli moja Wana-CCM tumeamua kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiye atakuwa Rais wetu kwa sababu ya mambo makubwa aliyowafanyia Watanzania hii Awamu ya Sita. Amefanya mambo makubwa ambayo hayajapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo yaliyofanyika na watu wengine, lakini Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan

amefanya mambo makubwa. Waheshimiwa Wabunge hapa mmesema miundombinu mbalimbali kama afya, elimu na kadhalika. Mambo ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu ambao wamejizima *data* wanasema kila kitu tunasema amejenga Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hivi hawaelewi kwamba mwenye fedha, mwenye idhini hapa ya kila kitu; Waheshimiwa Wabunge wanachangia na wanatoa maombi hapa kwa Waheshimiwa Mawaziri ambao wapo hapa; na cheni ya mnyororo sisi ndiyo kiungo, tunawaambia Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Mawaziri wanamwendea *boss* Mheshimiwa Rais ndiye anayefanya shughuli hizi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukikuta kutoka kule Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji anamwambia Diwani, Diwani ananiambia mimi Mbunge, mimi naiambia Serikali, ndiyo Waheshimiwa Mawaziri wapo hapa na ndiyo sasa inafika kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, mambo yote anayefanya ni Mheshimiwa Rais. Wasijizime *data* kwamba kila kitu tunasema amefanya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ndio jemedari anayefanya mambo yote hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, anafanya kazi kubwa sana pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote katika Wizara ya TAMISEMI. Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge sisi wote hapa umeona Mheshimiwa Mchengerwa anafanya kazi kubwa, na huo ndiyo ukweli. Amekuwa akifika katika maeneo kuangalia shughuli zinavyoendelea pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wenzake, tunampongeza sana. Aendelee kuchapa kazi, tunamwamini, achape kazi pamoja na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri zilizofanywa, ombi langu ni kwamba, yapo maboma ambayo wananchi wamejenga. Sasa nizungumzie kwenye Jimbo la Makambako. Upande wa afya lipo boma la kule Mkolango, naomba sana

tupate fedha tuweze kuwapelekea hao watu kule Mkolango, boma hili walishajenga, limeshaezekwa na limebakia tu kumalizia. Pia, lipo boma lingine la zahanati katika Kata ya Mjimwema, Mtaa wa Mjimwema nalo limefikia hatua wananchi wamefanya, tunaomba Serikali iweze kunena. Lipo boma lingine pale Kivavi, tunaomba na yenyewe zahanati hiyo iweze kumaliziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine linamwendea Mheshimiwa Prof. Mkenda, anafanya kazi kubwa sana. Alipokuja aliwaambia wananchi wa Wilaya ya Njombe hususan Mji wa Makambako, Halmashauri ya Makambako kwamba zipo fedha ambazo atatupatia za kujenga shule ya ufundi. Nimekuwa nikiwasiliana naye, fedha hizo tunazisubiri kwa hamu. Tunaomba fedha hizo ziende kwa wakati ili wananchi waweze kupata shule ya ufundi katika ukanda ule, kwani itawasaidia sana wananchi wa Jimbo la Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo ombi lingine kuhusu Hospitali yetu ya Halmashauri. Kutoka Mjini Makambako kwenda mahali ilipojengwa hospitali ni kilometa nane, na barabara siyo nzuri sana. Tunaiomba Serikali itutengee fedha kwa ajili ya kujenga barabara ya lami kutoka Makambako kwenda pale Mlowa ambapo ipo Hospitali ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miji ile 45 ambayo tulipata awamu hii ya 2025/2026 ya kujengewa soko, stendi na lami tunaomba tuongezewe. Tulipewa kilometa 20, lakini awamu ya kwanza wamesema watatupatia kilometa tano. Tunaomba tuongezewe kilometa mbili ziwe saba ili kusudi tuweze kufika kule kwenye Hospitali hii ambayo nimekuwa nikiizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine katika Mji wa Makambako kuhusu fidia ambayo imezungumzwa kwa muda mrefu kwenye suala la umeme wa upepo. Wananchi wa Makambako wamekuwa wakizuiliwa kwa takribani miaka zaidi ya 16 hadi 18. Katika maeneo yao hakuna kitu ambacho wanakifanya, na wanasubiri kulipwa fidia katika maeneo yao kwa ajili ya umeme wa upepo. Tumekuwa tukiahidiwa kwamba

watalipwa mwezi huu au mwezi huu. Tunaomba sasa mwaka huu angalau Serikali ione namna ya kuwalipa fidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la soko na stendi. Namwomba sana Mheshimiwa Mchengerwa, wananchi wanasubiri kwa hamu. Katika miji ile 45 na Makambako ipo, soko na stendi na eneo ambalo tunajengewa la *garden*. Unajua *garden* ni muhimu sana kwa mjini kwa watu hasa wenye *stress* na kadhalika, na nini, waende mahali ili waweze kutulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa soko na kutupa hiyo stendi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, ahsante sana.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote. Wachape kazi, mambo ni mazuri, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Kumba Ndulane na baadaye Mheshimiwa Waziri wa Elimu ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunakaribia kukamilisha kazi yetu, tutaendelea hadi tuweze kumaliza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye Enzi na Utukufu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge hili Tukufu kwa mwaka huu 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupitishwa kwa kishindo na Wajumbe wa Mkutano Maalum wa CCM kuwa ni

mgombea pekee wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kama Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, nasema kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan hatukumpitisha kwa sababu tu ndiye Rais aliyepo madarakani, wala hatukumpitisha kwa sababu ni Rais mwanamke kwamba tuna hamu ya kuendelea kuongozwa naye, bali tumempitisha kwa kazi kubwa za kishindo za utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo mojawapo ambalo linanifurahisha katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni katika vile vipaumbele alivyovitaja kwenye kutengeneza uchumi shindanishi, uchumi shirikishi na uchumi fungamanishi. Jambo hili limetekelezwa kwa kishindo na Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, kupitia *TARURA* nimeona jambo hili la kuhakikisha wananchi wanashiriki katika kujiletea maendeleo yao, nalo limefanyiwa kazi kwa kupitia kile kilichoitwa *Samia Bond* au *Infrastructure Bond*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI anisikilize kwa makini. Nina ushauri kidogo kuhusiana na jambo hili la *Infrastructure Bond* au *Samia Bond* kama ambavyo *CRDB* imeiita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposhauri tutumie *Infrastructure Bond* ili kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wao wa kushiriki katika ujenzi wa miundombinu hatukumaanisha fedha itoke kwa *Commercial Bank*. Jambo hili tulitamani lifanywe na *TARURA* yenyewe kwa kushirikiana na *BoT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la hili jambo ni kuhakikisha tunapunguza madeni kwa wakandarasi ili kuwawezesha kuwa *liquid* kwa kupitia Benki Kuu na *TARURA* wenyewe, wakusanye hizi fedha za wananchi wenyewe wazipeleke kwenye *BoT*. Ile fedha

irudi kwa *TARURA* kuweza kutengeneza barabara zetu na kuwalipa wakandarasi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hii inapotoka kupitia *Commercial Bank,* shilingi bilioni 150 ambayo inamfanya *banker* ampe mkandarasi, ile *advance payment* mara anapoonekana ame-*win tender* kule *TARURA,* tunamwongezea mzigo mkandarasi wa ndani kwa sababu *Commercial Bank* inamtoza riba kwa fedha ambayo inampa. Kama fedha hii wananchi wangeipeleka *BoT* kama *bond* nyingine ambazo zinawekwa *BoT, then* ikirudi kupitia *TARURA* inaweza kuwasaidia wakandarasi wazawa kuliko ambavyo imepelekwa kwenye *Commercial Bank*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana suala hili la *Infrastructure Bond* lifanyiwe marekebisho, lisipitie *Commercial Bank* kwa sababu tunawaongezea mzigo wakandarasi wa ndani na wala haliendi kwa maana pana ya kutatua changamoto ya madeni mengi ambayo Serikali inayo kwa wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lingine ni kwamba tunayo *Fuel Levy* ambapo Serikali inakusanya *almost 1.5 trillion per year.* Kwa hiyo, tunapochukua zile *bond,* wananchi wakiweka *BoT,* ile *Fuel Levy* inaweza ku-*service* ile *bond* kwa maana ya zile *interest* kila baada ya miezi sita ambayo mwananchi anapaswa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *Fuel Levy* inakwenda kurudisha ile *interest* ya *six months* ambayo mwananchi anatakiwa akalipie, lakini siyo kuchukua shilingi bilioni 150 *of which is very minimum amount of money* kuiingiza kama *Infrastructure Bond.* Jambo hili hatulifanyi sawasawa na lengo linalotakiwa kuhakikisha wananchi washiriki kwa upana wake, katika uchumi fungamanishi na uchumi shirikishi. Haiwezekani kupitia utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana *TARURA,* jambo hili wakalibadilishe. *TARURA* na *BoT* washirikiane kukusanya fedha kutoka kwa wananchi na zirudi kama *Infrastructure Bond.* Ninachoweza kusema ni nini? Tumeshuhudia na hapa Waziri

wangu Mheshimiwa Lukuvi ni shahidi, wananchi kibao wanarudi na fedha zao *BoT* wakitangaza *bond.* Maana yake fedha za wananchi zipo ambazo zinaweza kuingia kwenye *Infrastructure Bond,* lakini utashangaa tunakwenda kuji-*confine* kwenye *Commercial Bank* kumrudishia mzigo mkandarasi wa ndani. *This is not fair.* Tunaomba tulirekebishe. Ilani ile ya Chama cha Mapinduzi ilikuwa na dhamira njema, tusilipeleke jambo hili kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge. Tunamalizia na Mheshimiwa Kumba Ndulane, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika taarifa zote mbili za Kamati zilizotolewa leo hii. Kwa hakika Wenyeviti wetu wamefanya kazi nzuri ya kutengeneza ripoti nzuri na kuzisoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, nitangulie kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kupitishwa na Chama chetu cha Mapinduzi kuwa mgombea pekee wa nafasi ya Urais katika uchaguzi utakaofanyika mwezi Oktoba hapa nchini. Kwa hakika hii nafasi hatukumpa kwa upendeleo, kwa kweli tumempa kwa sababu ya vigezo vya msingi ambavyo amevifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu amefanya juhudi kubwa za kuhakikisha kwamba nchi yetu inapiga hatua katika sekta zote zikiwemo hizi ambazo zimezungumzwa leo hapa na Wenyeviti wetu wa Kamati. Kwa kweli kazi imefanyika kubwa. Nami napenda nitoe ushahidi katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini na Wilaya yetu ya Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika sekta ya elimu tu, mwaka huu vijana wetu wa elimu ya sekondari wamefanya vizuri sana. Wale waliomaliza mwaka 2024, tumetokomeza zero kwa kiwango cha kutosha. Mwaka juzi tulikuwa na *zero* 137, mwaka huu tumepata *zero* 82 tu, lakini kwa mara ya kwanza katika Wilaya ya Kilwa tumetoa *division one* ya *point* saba kutoka shule ya Sekondari ya Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kijana wetu anaitwa Sylivatory Gustavu Mangosongo amepata *division one* ya *point* saba kwa mara ya kwanza katika Wilaya ya Kilwa. Kwa hiyo, hii inatokana na juhudi ambazo zimefanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita ikiongozwa na Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia na Mawaziri wa Wizara za kisekta ambazo leo zimezungumzwa hapa, tukianzia na Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza Mawaziri wote lakini, sana nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya uwekezaji katika sekta ya elimu na sekta zote ambazo zimezungumzwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, napenda kubainisha baadhi ya maeneo ambayo naona yanapaswa kuongezewa nguvu ili kuhakikisha kwamba sekta hizi ambazo zimezungumzwa leo katika taarifa mbalimbali ambazo zimetolewa ziweze kuwa na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu, ningependa kuiomba Serikali kuongeza juhudi za kuajiri walimu wengi ili waweze kutosha kufundisha vijana wetu na kuwawezesha kupata maarifa kwa sababu kuna upungufu mkubwa wa walimu. Kwa Wilaya ya Kilwa peke yake, kuna upungufu wa mamia ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kumekuwa na changamoto katika usimamizi wa taratibu za uhamisho. Leo ukienda katika Halmashauri zote za Wilaya, kuna upungufu mkubwa wa walimu unaotokana na kwamba walimu wakishaajiriwa tu, baada ya

mwaka mmoja au miaka miwili, wengine wanatoa sababu za kuugua na kadhalika. Waliajiriwa wakiwa hawana magonjwa wala nini, lakini wakishapata ajira, basi wanatafuta sababu mbalimbali kama za ugonjwa ili kuhamia kwenye Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji. Kwa hiyo, naomba Serikali idhibiti hili jambo ili basi hata kule kwenye halmashauri za wilaya tuwe na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la ujenzi wa nyumba za walimu, madaktari, ma-*nurse* na wote ambao wanahusika na hizi sekta ambazo nimezitaja. Nyumba ni tatizo, hivyo, baadhi ya walimu wanalazimika kukimbia maeneo mbalimbali ya kule vijijini kwa sababu hali ya maisha ni ngumu, hata makazi ya uhakika hakuna. Kwa hiyo, nilifikiri pia Serikali pamoja na kwamba imefanya kazi kubwa kwenye miundombinu ya madarasa, maabara na kadhalika, basi iangalie pia katika hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye usimamizi wa miradi kumekuwa na shida na changamoto kubwa, kuna wakati niliwahi kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa TAMISEMI, kuna shule yangu pale inaitwa Namatungutungu, ile shule kwa kweli fedha zilikuja shilingi milioni 560 mwaka 2023, lakini mpaka hapa tunapozungumza ule mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na timu nyingi za uchunguzi zilizoletwa, hatujapata matokeo, hatua muhimu hazijachukuliwa juu ya wale waliohusika na ufisadi katika ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali irudi ikaangalie kwenye zile taarifa ambazo zimetolewa na zile timu, basi watupe majibu na wachukue hatua madhubuti katika kudhibiti masuala kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa *VETA* sasa hivi umesimama. Ulianza mwaka 2023, tukapewa matumaini utaisha ndani ya mwaka mmoja, lakini haujakamilika pale Namatungutungu katika Kijiji cha Njia Nne. Naomba Serikali

kuangalia suala hili kwa makini na kuweka fedha za kutosha ili kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye zahanati na nyumba za waganga, jambo hili pia liangaliwe. Kuna maboma mengi ambayo hayajakamilika, hivyo katika bajeti ijayo, naomba Serikali waangalie waweze kuleta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara za vijijini, kwa kweli barabara zangu zote katika jimbo zima zina hali mbaya. Juzi tulifanya tathmini, jumla ya kilometa 162 zimeharibiwa vibaya sana, madaraja yamevunjika, na mwisho wa siku hizo barabara hazipitiki. Kwa maana hiyo, zimesababisha ugumu katika utekelezaji wa miradi mingine kama ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hali ya maisha imepanda kwa sababu watu wanatumia bodaboda tu na vyombo ambavyo havina uhakika, lakini pia usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara umekwama au unafanyika kwa kuchelewa sana, na kwa maana hiyo hali imekuwa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iziangalie barabara kutoka Kipatimu mpaka Pungutini, barabara kutoka Namayuni mpaka Namakolo - Mt. Kimwaga mpaka Kandawale - Njinjo mpaka Kandawale na hadi Ngalambi, na pia Kinjumbi hadi Mteramboko. Juzi tumefanya tathmini na watu wa *TARURA* zina jumla ya gharama ya shilingi bilioni 9.87 inahitajika kwa ajili ya matengenezao ya hizo barabara ambazo zimekufa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kumba Ndulane. Sasa namkaribisha Waziri wa Elimu, baadaye atafuatiwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii nami niweze kuchangia kwenye hoja iliyoletwa hasa na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, naomba nilishukuru Bunge lako Tukufu na Wabunge wote kwa namna mbalimbali waliyotufariji wakati wa msiba wa mama yangu mzazi, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwashukuru sana Wabunge wote waliochangia na hasa Kamati yetu. Tumepitia taarifa yao, tumeangalia maazimio, sisi tuko tayari kufanyia kazi. Kwa kweli wanatuongoza vizuri sana. Niseme kweli kabisa, Kamati yetu hii ya Elimu, Utamaduni na Michezo, wanatusimamia kweli kweli, lakini wanatusimamia vizuri na hasa kipindi hiki cha mageuzi makubwa ya elimu hapa nchini. Kwa hiyo, tunapenda sana kuwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la mageuzi ya elimu, suala moja ambalo limezungumzwa hapa na ambalo Mheshimiwa Rais alizungumza wakati anazindua Sera ya Elimu na Mafunzo, ni suala la walimu. Mheshimiwa Rais, alizungumza na ninadhani walimu wote nchini walimsikia, alisema katika mageuzi haya katika mduara huu katikati wako walimu. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuwa na walimu wa kutosha, na pia alizungumzia maslahi ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi kupitia wenzetu wa TAMISEMI na Utumishi, kasi ya kuajiri walimu imeanza kushika mwendo. Tunakwenda vile kwa sababu tunakubaliana na Wabunge wote, na kama alivyosema Mheshimiwa Rais wetu kwamba lazima tuongeze idadi ya walimu, na nilirudie tena, hili walimu wote hapa nchini walisikie. Alisema ni muhimu sana kuangalia maslahi ya walimu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, walimu wote hapa nchini wanasikia, na wengi wamenitumia *message* kwamba tuwasilishe shukrani zetu kwa Rais wetu kwa sababu anaonesha kujali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili la walimu, kuna suala moja ambalo ningependa nilifafanue, limezungumzwa hapa kwamba katika kuajiri walimu tuchukue aliyekaa mtaani muda mrefu zaidi au tuchukue ambaye amemaliza karibuni? Tuajiri tu bila kufanya usaili na mtihani au tuwalete wale walimu tuwapime tuangalie ni walimu gani ambao sasa hivi ni bora kufundisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala kubwa linazungumzwa, lina maumivu yake makubwa tunalielewa. Tunaelewa umuhimu wa watu waliyosomea ualimu kupata ajira, na tuna uchungu kwamba tungependa wapate ajira. Tunaelewa umuhimu wa wanafunzi kupata walimu bora, na tungependa wanafunzi wapate walimu walio bora na siyo tu bora walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kuhakikisha kwamba walimu wanafanyiwa usaili, wanafanya mtihani, wala siyo ya Tanzania tu, iko katika nchi nyingine kama Ghana na nchi nyingine ambazo zimepiga hatua kubwa sana katika maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufikirie, wewe tunataka kwenda kumchukua mwanafunzi ajifunze Kiingereza, tunamtaka Mwalimu anayeweza kusema Kiingereza vizuri akafundishe. Wote wamesoma darasani, vyuo hivyo hivyo, na wakati wanasoma kwenye vyuo wamepishana. Kila wakifanya mtihani kuna aliye bora zaidi na ambaye siyo bora kama wengine, japo wote wamefaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengine wamemaliza miaka kumi iliyopita, mwingine amemaliza juzi. Ukiangalia maslahi ya yule mwanafunzi, utagundua unahitaji mwalimu bora. Ukiangalia huyu amekaa sana mtaani miaka kumi, kweli unaweza kutaka

kutumia Mwalimu aliyekaa miaka kumi? Kwa hiyo, mageuzi haya ya elimu yanahitaji tuwe na walimu bora ili tuweze kufanikisha malengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa wito kwa walimu wote waliosoma popote walipo, umekaa miaka kumi endelea kujiendeleza kwa sababu ukiitwa ukasailiwa, Mwalimu wa Kiingereza, natoa mfano wa Kiingereza, tukikuta huwezi kuongea Kiingereza, hatuwezi kukuajiri kwa sababu umekaa miaka kumi mtaani, itatuuma sana; lakini inauma zaidi kumpelekea wanafunzi Mwalimu ambaye kwa kweli hajaandaliwa vizuri. Suala hili ni la kisera, lipo katika sera kwamba utaajiriwa kwa kupitia mchujo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ukumbuke, walimu wanaoomba ajira ni wengi kuliko fursa zilizopo. Sasa unawachaguaje? Tuchague vipi walimu hao? Vigezo kwamba wamekaa muda mrefu zaidi; na hata waliokaa muda mrefu zaidi tunaweza tukaajiri wote? Kama hatuwezi kuwaajiri wote, walipokuwa wakikaa darasani walikuwa wanafahamiana, kuna waliokuwa wakishika nafasi ya kwanza kila siku na mwingine anashika nafasi ya mwisho, lakini kafaulu, na wanajua. Halafu wanakuja kuangalia aliyekuwa wa mwisho ameajiriwa, wanauliza, hivi nyie mnaajirije watu? W*here is the meritocracy* katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa usaili huo, tunachukua wale ambao mwenyewe ukijua kwamba hapa nimesailiwa bwana, hapa nimeboronga, unajua hukujuariwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wito wangu, watu waendelee kujiendeleza. Kwa kweli hali ni ngumu, lakini vilevile tunaangalia sana maslahi ya hawa wanafunzi ambao wanakwenda kufundishwa wapate walimu bora na siyo tu bora walimu. Kwa hiyo, kwamba una Cheti cha Ualimu, ni jambo moja. Siyo kwa nchi hii tu, nenda Ghana, nadhani hata Japan na nchi nyingine wanafanya hivyo. Hatuwezi kupenda kujilinganisha na

nchi nyingine, lakini tukashindwa kuchukua maamuzi magumu kwa ajili ya kuendeleza elimu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende katika mageuzi ya elimu hapa. Labda niongeze moja kuhusu mageuzi ya elimu. Haya ni maono ya Mheshimiwa Rais wetu, kila mmoja anafahamu, na bahati nzuri wakati wa uzinduzi tulionyesha *documentary* ya jinsi alivyokuwa anatoa maagizo tangu mwanzoni kwa sababu watu wanazoea, ukisema Rais wetu kafanya kazi nzuri, wanasema, hapana mnasifia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi upo. Hata pale ambapo hatuna Ushahidi, si kazi yake; wote tunafanya kazi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kwenye hili ni maono yake *personal*. Yeye mwenyewe alianza kulisema mapema kabisa hata mwezi mmoja haujapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nieleze katika mageuzi ya elimu ambapo pengine tutapata muda wa kuyazungumza sana. Sasa hivi tunaelekea katika kujenga *Polytechnics.* Mtakumbuka vitu hivi vilianza kutoweka duniani, China hawakuviondoa, tunaanza mchakato na Katibu Mkuu sasa hivi anakamilisha kujenga *Polytechnics* ambazo zitakuwa ni *High School* za ufundi za miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga moja Mwanza, nyingine tutajenga Kigoma, tutajenga nyingine Mtwara, tunajenga nyingine Zanzibar kwa utaratibu maalumu kupitia mkopo kutoka China. Nyingine tunajenga Morogoro kupitia Korea; nyingine tumekamilisha hapa Dodoma na ujenzi utaendelea, na hayo ni maelekezo ya Rais wetu ili wale wanafunzi wanaosoma mafunzo ya amali ambayo sasa hivi tunatekeleza kwa awamu, kama mnavyofahamu mwaka 2027 ndiyo utakuwa ni mwaka ambao tutaanza kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anasoma miaka kumi, anaposoma shuleni. Anaenda katika mkondo wa amali, akimaliza *form four, form five* na *form six* yake ni miaka mitatu na *diploma* ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna maandaalizi kwamba akitoka pale, *Diploma* yake atakwenda kuchukua Mwanza, Kigoma, Mtwara, Morogoro, au hapa Dodoma chuo chetu cha ufundi tumekamilisha au ataenda kuchukua Zanzibar. Hiyo yote ni kazi ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kidogo kuhusu *VETA*. Wakati wote tunaangalia changamoto, tuangalie na mafanikio. Hizi changamoto tulizoziona zimezungumzwa, sisi na Wizara ya Fedha tunafanyia kazi tutazikwamua. Tuko *very confident,* tutasonga mbele na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu yuko hapa, lakini yale tuliyofanikiwa tusisahau kuyazungumza sana, kwamba sasa hivi tumemaliza *VETA* za ngazi ya mikoa, Simiyu, Geita, Njombe na Rukwa na mmeziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *VETA* nzuri sana. Tunajenga pale Songwe; sasa hivi tusisahau kuangalia *VETA* ambazo zimeshaanza kufanya kazi zinavyokwenda vizuri kadiri kazi inavyokwenda. Kwa hiyo, zile changamoto nyingine ambazo tumeziona, watu wamezungumza ni changamoto ambazo zisije zikasababisha watu wakasahau mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, sisi wenyewe tunaweza kwenda kwa wananchi, tukawaeleza changamoto mbalimbali, lakini tukasahau kuwaeleza kwamba uamuzi wa kujenga *VETA* 64 kwa kila Wilaya ni jambo la kushangilia. Hata kama kutakuwa na mkwamo kidogo, tunatarajia kumalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi ya kuzungumza, lakini nami ningependa kuipongeza sana na kuishukuru Kamati yetu na sisi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tunaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Sasa nimkaribishe Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa ruzuku ya uhai, lakini kutujalia afya ya leo kupokea Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge, kwa taarifa yake nzuri na tunayapokea mapendekezo yote ambayo yametolewa na Kamati, ambayo imekuwa inatusimamia vizuri kuhakikisha kwamba sekta hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inafanya kazi kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru sana Mheshimiwa sana Shaban Hamisi Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki kwa mchango wake mzuri kuhusu suala la michezo na wasanii; na hivyohivyo Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu Mbunge wa Tunduru Kaskazini kwa hayo aliyoyaeleza kuhusu sekta ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, ilimpendeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 8 Desemba, 2024 kuunda Wizara mpya ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa kuiondoa Idara ya Habari kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kuiunganisha na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake, lakini kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Tumeshuhudia mambo makubwa katika sekta hiyo ambayo yameifanya Tanzania kuaminiwa kuwa mwenyeji na mshiriki wa Mashindano ya *CHAN*, lakini kuwa mwenyeji na mshiriki wa Mashindano ya *AFCON* mwaka 2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuliarifu Bunge lako kwamba Tanzania, mwezi huu sisi tulikuwa tayari kabisa kuwa wenyeji na washiriki wa mashindano ya *CHAN,* lakini tulishukuru Shirikisho la Michezo la *Africa*, *CAF* kwa maamuzi yake ya kuyapeleka mashindano haya hadi mwezi wa Nane kuanzia tarehe 02, mashindano ambayo sisi Tanzania, Uganda na Kenya tutakuwa wenyeji na tutashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko sababu za msingi kabisa ambazo ningependa wote mzifahamu, hazitokani na Tanzania lakini hali halisi ya maandalizi yanapokuwa ya nchi tatu, lazima wote mwende pamoja. Hamwezi kumwacha mwingine nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, watu wa Afrika Mashariki, tujipongeze, wenzetu wote walioandaa mashindano ya *CHAN* walipewa miaka miwili kuyaandaa kama ambavyo sisi tumepewa miaka miwili kuyaandaa ya *AFCON,* lakini kwa *CHAN* tulikuwa tumepewa miezi mitano. Sasa ndani ya miezi mitano huwezi kufanya maandalizi. *Cote d'Ivoire* walipewa miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu wako watu wanaodhani kwamba limefanyika kwa sababu ya uzembe, hapana. Uhalisia unahitaji maandalizi zaidi ya miundombinu ya wachezaji ili kuhakikisha Tanzania tunakuwa siyo tu wenyeji wa *CHAN,* lakini pia washiriki wa *CHAN* na siyo ikiwezekana; tuingie fainali na tuchukue kombe la *CHAN* ili libaki hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa katika miundombinu ya michezo kama ilivyoelezwa na Kamati, nasi hatuna budi kumshukuru sana kwa fedha nyingi ambazo ametoa kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vipya, lakini pia kwa ajili ya ukarabati wa Kiwanja cha Benjamini Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba ujenzi wa uwanja wa Arusha ambao mpaka sasa mkandarasi ameshapewa

malipo ya awali ya shilingi bilioni 92.7 unaendelea vizuri. Ndiyo, umefikia 25%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba mpaka itakapofika Desemba mwaka huu, majukwaa yote tayari yatakuwa yamekamilika na kufikia Juni, 2026 ujenzi wote utakuwa umekamilika, na ujenzi wa Uwanja wa Arusha unaendana na kujenga Mji mpya wa Arusha unaozunguka uwanja huo. Kwa hiyo, utakuwa siyo uwanja tu lakini pia litakuwa ni eneo la biashara, litakuwa ni eneo la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa Uwanja wa Benjamini Mkapa, naishukuru Kamati ya Bunge kwa ufuatiliaji wa karibu kabisa wa ukarabati wa Uwanja wa Benjamini Mkapa, na ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati, maelekezo mliyotupa kwamba ifikapo mwisho wa mwezi huu wa Nne, ukarabati wa uwanja uwe umekamilika, utakuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tumefikia 80%. Tumefanya ukarabati mkubwa, viti vyote 60,000 vitabadilishwa, na vilivyopo kwa utaratibu utakaopangwa vitapelekwa katika maeneo mengine. Tayari taa 320 za kisasa zimeshafungwa kwa kiwango cha *FIFA,* yaani Daraja A na mfumo wote wa maji, umeme, TEHAMA, ulinzi na zulia la eneo la riadha limeshabadilishwa. Yamebaki maeneo kama hayo ambayo Mheshimiwa Taletale ameyaeleza ya vyoo na mambo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka kuwahakikishia kabisa kwamba, Uwanja wa Benjamin Mkapa utakuwa tayari kwa mujibu wa maagizo ya Kamati ya Bunge, nasi tuko tayari kwenda na ninyi kwa tarehe iliyopangwa ili tuweze kuona kazi kubwa iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uwanja wa Dodoma ambao umekuwa kizungumkuti kwa muda mrefu, nataka niwaambie sasa, Alhamisi ya wiki hii tarehe 13 Februari, 2025

tunasaini mkataba wa kuanza kujenga Uwanja wa Dodoma utakaojengwa katika eneo la Nzuguni. Mkandarasi amepatikana, na fedha ya kuanza ujenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Waziri wa Fedha, ndugu yetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, ameshaiandaa *check* kwenye *exchequer* inayokuja ya kuhakikisha kwamba uwanja huo unanza kuajengwa. Utakuwa ni uwanja wenye uwezo wa kubeba watazamaji 32,000 kwa wakati mmoja. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameifanyia Tanzania mambo makubwa na ameifanyia Dodoma mambo makubwa. Kwa ujenzi wa uwanja huu, ni kweli sasa Dodoma ni Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zinaendelea. Pale pale katika uwanja huo mkubwa utakaojengwa, tunajenga kituo cha michezo changamani *(Sports and Recreation Center),* ambacho kimefikia 67%. Kwa hiyo, michezo kama *Basketball, Handball, Netball* na uogeleaji itafanyika pale, pia na burudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hilo litakuwa na uwanja huo mkubwa, lakini pia na kituo changamani *(Sports and Recreation Center)*. Wakati huo huo maendeleo mengine yanafanyika katika viwanja vingine vyote ambavyo vitatumika na *CHAN* na *AFCON*. Mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri, kila wiki tunafuatilia maendeleo ya ujenzi wa viwanja hivyo na ukarabati wa viwanja hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumzwa na Kamati na wachangiaji, ni kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya. Ninavyozungumza hapa, tayari Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametuletea taarifa kuwa *exchequer* ya shilingi 1,500,000,000 imetoka kwenda Chuo cha Malya, kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya, kimejipanga kutoa mafunzo ya Wandishi wa Habari ya

Michezo *(Media and Sports Journalism)*. Kwa hiyo, nawaomba watu wote wanaopenda kuwa wachambuzi wa michezo na wanaoandika habari za michezo kutumia fursa hii sasa ili kwenda kujifunza *Media and Sports Journalism* kule katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya.

*(Hapa kengele ililia kuashira kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako nimalizie moja. BAKITA wanafanya kazi kubwa sana na sasa tumeanza mchakato wa kuiunda upya BAKITA ili ifanane na majukumu iliyopewa ya kukipeleka Kiswahili duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, BAKITA wamefanya kazi kubwa sana, naomba nieleze. Wametoa Kamusi ya Kiswahili kwa Shule za Msingi. Kamusi hii ni Kamusi muhimu sana. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wahamasishe shule za msingi zote zipate nakala ya Kamusi hii ya Kiswahili kwa Shule za Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamusi hii ni ya aina yake kwa sababu kila neno imekupa jinsi ya kulitumia katika kila sentensi. Nimeongea hapa na Waziri wa TAMISEMI, naye ataizungumzia. Kamusi hii ni muhimu sana na ni vizuri sana wote wawe nayo. Kuhusu bei, tutatafuta bei ambayo TAMISEMI watamudu kuzinunua zote. Kwa hiyo, tutakaa tuongee ili TAMISEMI wazinunue zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mimi nina hakika kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa kuipa BAKITA fedha ambayo imetoa Kamusi hii ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ninamaliza nalo kuhusu Kamusi, ndugu zangu Watanzania, nchi ya jirani ndiyo inayonunua Kamusi kutoka Tanzania kuliko sisi wenyewe. Ndio

wanaonunua Kamusi kwa mwaka takribani nakala 50,000 mpaka 100,000. Sisi tukiuza 100 tunamshukuru Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuhamasishe matumizi ya Kamusi, tuhamasishe kununua Kamusi ili Kamusi yetu itumike pia na watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwepo mengi sikujua, kumbe muda unakwenda kasi. Basi mengine niyabakize *Inshallah* katika vikao vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha, baadaye Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, atamalizia.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada ambazo zipo Mezani. Nifanye mambo mawili; la kwanza, ni kupongeza Taarifa za Kamati zilizowekwa Mezani, na kwa niaba ya Wizara niseme tumepokea maelekezo na mapendekezo ambayo yamewekwa kwenye taarifa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa niaba ya Bunge Zima ambayo yameungwa mkono na Bunge Zima, ni maelekezo ambayo Serikali haina pingamizi nayo na hii ndiyo kazi ambayo tumeendelea nayo mara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala hapajatokea ulegevu katika eneo lolote. Nilisema katika kipindi kilichopita na ninarejea tena kusema, kilichojitokeza ni kweli bajeti yetu imeathirika katika kipindi cha kuanzia mwaka 2024 na 2025. Kwa kuwa bajeti imeathirika, Serikali imekuwa ikipambana kuhakikisha kwamba, shughuli zote hazikwami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano michache, mwaka 2024 katika muda ambao Bunge litakumbuka, tulipitia muda ambao barabara zote za *TARURA* na *TANROADS* zikiwa zimeharibika. Hii iliathiri sana bajeti yetu na mtiririko wake wa

kawaida. Kama vile hiyo haitoshi, tulipitia kipindi ambacho mgao wa umeme ulienda kutunyemelea katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge litakumbuka mgao wa umeme ulishashika kasi yake. Tulikuwa na njia mbili za kushughulikia jambo hilo, ambapo ilikuwa ama tutafute mitambo ya dharura ya kukodi au tuharakishe ukamilishaji wa bwawa la umeme. Ilifika wakati tulikuwa tunalipa *certificate* zaidi ya shilingi bilioni 400 kwa mwezi kwenda kwenye mradi mmoja wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya aina hiyo siyo ndogo, na huwezi ukafanya hivyo bila kuathiri bajeti, maana yake kikapu ni kile kile. Tulikuwa tunagusa hapa, tunagusa hapa, ili tutekeleze lile badala ya kukodi mitambo. Jambo lile limefanyika kwa haraka na mradi ule umekamilika. Sasa sisi ndani ya Serikali tulijua inawezekana tukapoozesha mahali, lakini baada ya mradi ule kukamilika, tumepumua na ndiyo maana unaona sasa tunarejesha kasi ya utekelezaji wa shughuli hizo nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kule *TARURA*, fedha hizi ambazo tumezitoa hivi juzi, ni vile tu wakandarasi walikuwa *site* na walikuwa wanadai. Kwa hiyo, tumepeleka na zimekwenda kulipa madeni. Hivi sasa pia tunapeleka tena na hicho ndicho ambacho tunakubaliana na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujakaa tu tukaacha, lakini tulisema kwenye hili ambalo tunaweza tukatatua kwa kukamilisha bwawa letu wenyewe, fahari ya Watanzania, tulisema tu tufunge mikanda, tutabanabana, kuna sehemu pata-*slow,* lakini tutakamilisha, na jambo hilo limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, utakumbuka pia maelekezo ya Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema tumeshaumia sana katika kutekeleza *Lot* mbili za reli, twendeni tujibane kuhakikisha reli inaanza kufanya kazi. Hata hilo, tulijibanabana kuhakikisha linakamilika, na yenyewe

imeshaanza kufanya kazi kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma. Hata hiyo, tulijibanabana na kufunga mkanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, pia tulikuwa tunakimbizana na Daraja la Kigongo – Busisi. Kazi ilikuwa inaendelea na ilishafanyika kwa kiasi kikubwa, ilikuwa inakaribia kumalizika lakini na kwenyewe tulisema tuikamilishe ili wale wananchi wasipate shida. Hivi tunavyoongea, Waziri wa sekta aliniarifu kwamba alitembelea pale, *almost* imeshakamilika. Nadhani inaweza ikazinduliwa muda wowote kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimkakati, kuliko kugusagusa kaeneo haka na haka halafu utumie mitambo ya dharura, tuliona tufunge mikanda ili tuwe na miradi ambayo imekaribia kukamilika ili tuhesabu hii imekamilika na hilo Rais wetu amefanya na limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia hata Mama yangu na rafiki yangu kipenzi sana Mheshimiwa Dkt. Ntara, akisema hata masuala ya *VETA*. Hata hili suala la *VETA* inawezekana Serikali kwa kuwa na matumaini na matarajio makubwa zaidi na yenyewe imetupa shida ya kuweza kuhakikisha kwamba labda *speed* ikawa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya ni zile zile tangu Uhuru, zinaongezeka kidogo kidogo, lakini kama mpaka Serikali ya Awamu ya Sita imekuta kuna mikoa na wilaya zaidi ya 60 hazina *VETA*, na Serikali ikaamua kuzijenga zote kwa mpigo. Mimi ninadhani haipaswi kunyooshewa kidole, bali inatakiwa kutiwa nguvu na kupongezwa. Tumekwenda kuzibeba wilaya na mikoa yote iliyosalia kwa mpigo na fedha zinakwenda, siyo kwamba tumeacha tu hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya sasa ya msukosuko wa kiuchumi duniani, kila jambo ni kipaumbele na kila jambo linahitaji fedha. Tumekwenda kubeba tarafa zote ambazo tangu Uhuru hazijawahi kuwa na vituo vya afya na baadhi ya

kata ambazo zilikuwa zinahitaji vituo vya kimkakati, tumekwenda kuzibeba zote kwa mpigo. Kama hiyo haitoshi, tumekwenda kuweka kila jimbo lipate kituo cha kimkakati na fedha hiyo itatoka kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kikapu ni kile kile, unaweza ukaona kwamba Serikali ina nia ya dhati sana kuhakikisha inatekeleza masuala ambayo Watanzania wanahitaji, sambamba na Wabunge ambao ni wawakilishi makini wa wananchi wanavyoshauri humu ndani ya Serikali. Hatujafanya makusudi kwenye jambo lolote, na wala hatujalegalega kwenye jambo lolote. Tumeongeza kasi na nguvu na tunafanya kwa jitihada kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemshuhudia kwamba mama yetu ni mama jemedari sana. Kwa mazingira ya dunia inayopitia ya kiuchumi, kila mchumi angemwelewa kwamba, "ninaondoa hii miradi kwa sababu dunia inapita kwenye msukosuko." Tena siyo Tanzania inapitia, ni dunia nzima inapita kwenye msukosuko. Fuatilieni nchi za jirani, nchi zote za *SADC* na *EAC,* fuatilieni na mnitajie nchi moja inayotekeleza miradi mingi na mikubwa ya kimkakati na yenye mtawanyo kama Tanzania inavyotekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kujibu kwamba fedha zitatoka ama hazitatoka? Fedha zitatoka na hiyo ndiyo kazi niliyotumwa, na bado naipenda. Fedha zitatoka zinazokwenda kwenye vituo vya afya na vituo hivi vyote ambavyo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameahidi kwenda kwenye kila jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia fedha ambazo zimetajwa kwenye sekta ya elimu, kwa upande wa miundombinu, maboma ya madarasa na mitaala mipya, zitatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakamilisha taratibu, na keshokutwa kuna andiko ambalo tutalitoa, ambalo ninyi wenyewe mtatufungulia twende kutekeleza haya mambo ambayo mmeishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za maeneo mengine ambazo zimeongelewa, na kwa ajili ya muda sitataja zote. Nikimaliza kikao hiki, na hata asubuhi nilikuwa na kikao na wenzetu ambao tunashirikiana nao *DMDP* na maeneo mengine, tumekuwa na vikao ambavyo tunakamilisha taratibu za kuweza kutoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wajue nia ya dhati ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan haijabadilika, na tena anatekeleza kwa nguvu zaidi. Nia ya dhati ya Serikali ya CCM kuendelea kujitambulisha kupitia kutekeleza mambo ambayo yanawasaidia wananchi kupiga hatua katika shughuli za maendeleo, haijabadilika na inatekelezwa kwa nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tutaendelea kutoa taarifa kwenye Kamati jinsi ambavyo tunatekeleza haya mapendekezo ambayo yametolewa na Bunge lako Tukufu. Yote tunakwenda kuyatekeleza na tunaongeza kasi zaidi kwa sababu tumeona jinsi ambavyo wawakilishi makini wa wananchi wa Tanzania, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jinsi wanavyosimama kidete kuisimamia Serikali na kutetea maslahi ya wananchi ili kuweza kuhakikisha kwamba Tanzania inapiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko *committed* na hii kazi. CCM inaiweza, Mheshimiwa Dkt. Samia anaiweza na sisi wasaidizi wake tutakuwa naye bega kwa bega ili kuweza kuhakikisha kwamba hakuna jambo ambalo linarudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunamalizia na Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Baadaye nitawaita Watoa Hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu linapita

katika mageuzi makuu ya utekelezaji wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ikiwa ni ndoto za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyesema: "Uhuru bila kujitegemea hasa kwenye mambo ya msingi, unaweza kutumika vibaya kama silaha ya kutuangamiza na ukawa ni uhuru bandia." Waziri wa Fedha ameshazungumza hapa kwa kina, na hili pia nilitamani Waheshimiwa Wabunge watuelewe kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, miradi mikuu ya kimkakati ambayo Serikali imeamua kuifanya yenyewe, pamoja na mambo yale ya msingi ambayo Baba wa Taifa alituusia kwamba haya siyo ya kuwaachia wengine wayatekeleze, ni sisi Serikali kujipanga na kuyatekeleza wenyewe. Hii ni pamoja na chaguzi zetu. Tumejionea Uchaguzi Mkuu huu unaokuja, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Serikali imefanya yenyewe kwa 100% na fedha hizo zimetafutwa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua vita ya mapambano dhidi ya ujinga, umaskini na maradhi, imeshika kasi sana chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia na chini ya wasaidizi wake wa karibu ambao ni wawakilishi wa wananchi, Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo imefanyika ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Unapoizungumzia TAMISEMI, unaizungumzia Nchi, Wabunge, Wakuu wa Mikoa 26, Wakuu wa Wilaya 139, Wakurugenzi kwenye Halmashauri 189, Wabunge wa Majimbo 215 na Wabunge wa Viti Maalum, jumla 393. Unawazungumzia Maafisa Tarafa 570, Watendaji wa Kata 3,958, Wenyeviti wa Vijiji 12,333, Wenyeviti wa Mitaa 4,269 na Wenyeviti wa Vitongoji 64,274.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema niyaseme haya kwa sababu kila Mheshimiwa Mbunge hapa ni shahidi. Kazi iliyofanywa kwenye majimbo haya 215 yaliyopo Tanzania Bara ni kubwa sana. Kazi kubwa sana imefanyika kwenye kila halmashauri, wilaya na mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukiri, tunazungumza hapa ukarabati na ujenzi wa majengo mbalimbali ya miundombinu kwenye sekta za afya, elimu na miundombinu ambayo Wabunge wengi wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zilizojengwa, vituo vya afya, ujenzi wa hospitali za halmashauri haukujengwa kwa bahati mbaya. Ni kwa sababu kwanza, kumekuwa na dhamira ya dhati kutoka Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia ya kwenda kuwahudumia Watanzania wa kawaida kabisa kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mafanikio haya ya Serikali ya Awamu ya Sita, hayawezi kuzungumzwa bila kutaja wawakilishi wa wananchi (Wabunge) ambao wamefanya kazi kubwa sana ya kuishauri Serikali, kutoa maoni, maelekezo ambayo Serikali imekwenda kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliposomwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wabumbe walikuwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu na Wajumbe wengine, wakaamua. Hawakuamua kwa bahati mbaya, ni kwa sababu kazi imefanyika katika kila kona ya nchi yetu. Pia, hii ndiyo sababu tunayo miradi inayoendelea katika maeneo ya majimbo yetu. Kila kona ya nchi hii na kwenye kila tarafa, ipo miradi inayoendelea. Kama siyo mradi wa elimu, mradi wa afya; kama siyo ujenzi wa zahanati ni kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeona kwa kazi hii kubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge wameifanya, na kwa muda tuliobaki nao ni dhahiri kwamba, Viongozi Wakuu wa Nchi na Waheshimiwa Mawaziri hawatakwenda kila jimbo kukagua na kufungua miradi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue fursa hii, kuwapongeza watendaji ndani ya sekretarieti za mikoa, na halmashauri zetu. Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kwa sababu watendaji ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuanzia kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa

Halmashauri, Watendaji wa Kata na Maafisa Tarafa wamefanya kazi nzuri sana kwa Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawataja hawa kwa sababu Wizara zote hizi zinapokwenda kule zinawakuta watendaji hawa waliopo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Inapokwenda kutekelezwa miradi ya maji, utawakuta kule watendaji ndio wasimamizi na ndio wanaofanya kazi nzuri. Tunapokwenda kwenye miradi ya umeme, utawakuta Watendaji Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, ndio wasimamizi na wanaosaidia kuhakikisha kwamba fikra za Rais wetu zimetimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tunayo miradi mingi ambayo bado haijafunguliwa, na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge hawa wamefanya kazi nzuri, nichukue fursa hii kuwaelekeza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri, kuwapangia Wabunge hawa miradi yote ambayo haijazinduliwa, waende wakaizindue mara moja katika majimbo yetu yote 215. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi na Wakuu wa Mikoa waandae utaratibu ule ule, kama anakwenda Waziri, kama anakwenda kiongozi wa juu kabisa, waende wakazindue miradi hii, kwa sababu Wabunge hawa ndio waliosemea miradi hii hadi ikashuka kule kwenye majimbo yetu. Wabunge hawa wamefanya kazi kubwa na nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja hapa zimezungumzwa na Kamati na sisi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumezipokea hoja zote. Nikuhakikishie, tunakwenda kuzitekeleza hoja zote ambazo Kamati imeshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kuhusu Shirika la Elimu Kibaha. Tunatambua umuhimu na historia ya Shirika hili la Elimu Kibaha. Niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tayari tumeshapeleka maoni ya Wizara yetu kwa mwenye mamlaka kuona uwezekano wa kufanya mapitio upya, ili Shirika la Elimu

Kibaha liendelee kufanya kazi kwa misingi ambayo tutakwenda kufanya maboresho makubwa katika Shirika la Elimu Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu watumishi katika sekta ya ardhi. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari Serikali imeridhia watumishi wote katika sekta ya ardhi kurejea Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili waweze kusimamiwa vyema na Madiwani katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusu miradi ya Benki ya Dunia. Natambua ni fikra za Rais wetu kwenda kuboresha, kufanya miji kuwa majiji, na kupanua vijiji kuwa miji; na tunatambua kwamba miradi hii ya Benki ya Dunia yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.18, lakini tulikuwa na changamoto kidogo ndani ya Serikali, tumeshazikwamua. Niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kuwa wakandarasi wote kuanzia wiki ijayo wataanza kupata fedha za ujenzi wa miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu uharibifu wa barabara zetu. Kwenye miradi hii natambua wapo Waheshimiwa Wabunge ambao waliongoza kuhakikisha kwamba wanaleta ushauri wao ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hawa ni Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mheshimiwa Kanyasu na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao katika maeneo yao walifanya kazi nzuri ya kutushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwathibitishie kwamba utekelezaji wa miradi hii utaanza kabla ya kuahirishwa kwa Bunge, yaani kuanzia mwezi wa Tatu miradi yote ambayo ilikuwa imebaki, itaanza kutekelezwa. Ni wakati wenu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, ninyi mmefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Mambo ni mengi, tumepokea hoja hii ya Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, namwelekeza hapa Katibu Mkuu kuhakikisha kwamba, anapeleka fedha kwenye Kituo cha Afya cha Maili Tano, kama ambavyo kimewasilishwa. Tunatambua Mheshimiwa Kingu amezungumza kuhusu Puma, Katibu Mkuu alishatuelekeza.

Nawaelekeza TAMISEMI kuhakikisha kwamba, fedha hizo zinakwenda kuongeza madarasa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu Ngorongoro. Niwakumbushe wasaidizi wangu kwamba wahakikishe wamepeleka mabweni katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ngorongoro na kuhakikisha zahanati ambazo zilipaswa kujengwa zinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Waheshimiwa Wabunge walilalamika sana hapa kuhusu miundombinu, kila kona miundombinu. Naomba niwathibitishie, Mheshimiwa Rais wetu kupitia fedha za Miradi ya Benki ya Dunia, tayari ametukabidhi takribani shilingi bilioni 247. Fedha hizi, kwa vilio vya Waheshimiwa Wabunge, sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* tumepokea taarifa, waraka, kutoka kwenye kila Mkoa, maeneo ambako kuna changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, shilingi bilioni 247 zitakwenda kila jimbo la nchi hii kwa namna ile ile ambayo Mameneja wa *TARURA* kwenye kila mkoa wametuletea. Fedha hizi zitaanza kutumika kuanzia mwezi wa Tatu mwaka 2025. Kwa hiyo, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kuwa tunapeleka fedha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vituo vya afya, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshasema hapa kwamba, Ijumaa hii tutapitisha waraka ambao utaletwa ndani ya Bunge, na kuanzia wiki ijayo vituo vyote vya afya vya kimkakati ambavyo Mheshimiwa Rais aliwaahidi Waheshimiwa Wabunge, vitakwenda kwenye majimbo yenu. Tutaanza kutoa shilingi milioni 300, na pia tutakarabati zahanati na maeneo mengine ambayo yatakuwa yamebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mdogo, lakini nichukue fursa hii kuunga mkono hoja kama ilivyowasilishwa na Kamati na

Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Natambua inawezekana kabisa katika maeneo yetu kukawa na changamoto mbalimbali. Inawezekana kabisa Taifa letu ni changa, lakini lazima tukiri, Rais wetu amegusa kila kona ya nchi hii, kila sehemu ya nchi hii ameigusa, na mimi nina imani kwamba, Wajumbe hawatatuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hawa wamefanya kazi nzuri maeneo yote. Pengine Mheshimiwa Mbunge ambaye hatafanya vizuri itakuwa ni nongwa tu za Wabunge, lakini Wabunge hawa wamewasemea wananchi katika maeneo yao yote. Wamezungumza kero za wananchi, na Rais wetu ametekeleza zile hoja zote ambazo Wabunge hawa, Wawakilishi, walikuja hapa Bungeni wakawasemea wananchi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Watanzania, kama Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambayo 76% ya Watendaji, wako chini ya Ofisi hii ya Rais, TAMISEMI, basi, wahakikishe yale maelekezo ambayo yamebaki katika maeneo yao wanayatekeleza, ili Wabunge hawa watakaporudi kule majimboni wakute maeneo yao yote waliyoyasemea yamekamilika, ili wananchi waweze kuona umuhimu wa kuwarejesha Waheshimiwa Wabunge hawa ambao wamefanya kazi nzuri sana kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Kama isingekuwa Katiba na Kanuni ndani ya chama, mimi ninaamini Wajumbe wa Mkutano Mkuu huko kwenye majimbo wangewarudisha Wabunge hawa hata kabla ya uchaguzi, kwa sababu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita yametekelezwa na yeye mwenyewe Rais Dkt. Samia, na wapo wasaidizi waliofanya kazi hii ambao ni Wawakilishi wa Wananchi, Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, Waheshimiwa Wabunge, na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kutuhakikishia ushindi.

Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, aje kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu. Pia, nawashukuru sana wachangiaji wote waliochangia. Takribani wachangiaji wote waliosimama waligusia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo, wachangiaji wote walio kwenye orodha, wamechangia kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye hoja, kwanza namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Sisi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumepita maeneo mengi sana kwa sababu, tunagusa wananchi. Kwa hiyo, tumeona jinsi ambavyo miradi mingi mikubwa inatekelezwa kwenye maeneo mbalimbali, na kauli ya kinafiki na kauli ya ukweli ni rahisi sana kuijua kwenye nyuso za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye nyuso za wananchi wa Tanzania tumeona mioyo ya dhati ya upendo kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndiyo maana hata maamuzi ya Mkutano Mkuu yaliyofanyika ya kumpitisha yeye pamoja na mgombea mwenza hayana upinzani wowote kwa wananchi kwa sababu ya kazi zake ambazo amezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutembea kule na kujionea, tuna uhakika wa kwamba kazi ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imejiuza yenyewe. Hata uchaguzi wenyewe

hautakuwa mgumu kwa sababu tayari *impact* imeonekana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni fahari kwangu, kama Mwenyekiti wa Kamati, kuwa na Waziri anayeelewa kazi yake na ambaye ameweza kuelezea hapa mambo mbalimbali ambayo yanafanyika. Katika Kamati, hatupati ugumu wa utendaji wa majukumu yetu kutokana na umahiri wa Wizara hii inayoongozwa na Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa, Manaibu wake wote wawili na pia, Makatibu Wakuu na viongozi walioko kwenye Wizara hii. Tunapata urahisi kwa sababu, tunasikilizana, tunaelewana na ushauri wetu tukiutoa unakubalika. Tunaamini hayo yataendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha, wengi waliochangia wamezungumzia mambo ambayo tayari yameshapata maelezo ya kutosha ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo, kama nikirudia, nitakuwa narudia mambo ambayo tayari yameshasemwa na wakati mwingine naweza nikaharibu ule utamu ambao wameyatolea maelezo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati, tunaendelea kusisitiza kwamba, ikiwa mambo yote haya yaliyoahidiwa hapa yatatekelezwa, basi tuna uhakika kwamba, wananchi wataendelea kupata manufaa, wataendelea kufaidika na wataendelea kuipenda Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi, ambacho hakitarajii kuondoka madarakani siku za karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe na maneno mengi. Baada ya maelezo hayo ya kina na uhitimishaji wangu wa hoja ambayo niliitoa, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yake yawe Maazimio ya Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Wabunge wote wameafiki. Kwa hiyo, Taarifa hii ya Kamati pamoja na Mapendekezo na Maoni yake yote kwa sasa natangaza kwamba ni Maazimio ya Bunge letu.

Haya, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, ili naye aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. HUSNA Z. SEKIBOKO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuja kuhitimisha hoja yetu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye hoja, nitumie fursa hii kuungana na wachangiaji wote waliochangia hivi leo kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta zote za maendeleo nchini. Naomba nitumie muda mfupi kutoa mifano miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anaingia madarakani, aliikuta Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ikiwa na bajeti ya takribani shilingi bilioni 35, lakini tunavyozungumza, ameipandisha mpaka kufikia

takribani shilingi bilioni 285. Ongezeko hili ni kubwa, la makusudi na tunaiona *political will* kwa Mheshimiwa Rais katika kuleta mapinduzi ndani ya sekta ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa eneo la Bodi ya Mikopo peke yake nchini, mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, Rais alikuta bajeti ya takribani shilingi bilioni 400, lakini tunavyozungumza sasa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameipandisha bajeti mpaka kufikia takribani shilingi bilioni 800. Ni takribani mara mbili ya bajeti ambayo ameikuta. Ongezeko hili ni kubwa na tunaiona nia ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa dhati ya moyo Wangu, kwanza kuwashukuru wachangiaji wote ambao wamechangia katika hoja yetu ya Kamati katika maeneo mawili; kwanza upande wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na pili, upande wa Habari Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Kamamba, Mheshimiwa Dkt. Ntara, Mheshimiwa Hamisi Taletale, Mheshimiwa Kungu, Mheshimiwa Prof. Mkenda na Mheshimiwa Prof. Kabudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee sana nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Prof. Kabudi na Mheshimiwa Prof. Mkenda, kwa kutusaidia kutoa ufafanuzi wa kina kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli, wamerahisisha kazi yangu ya kuhitimisha hoja, na sitatumia muda mrefu sana kwa sababu mengi ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri, hawa wawili wameyatolea ufafanuzi. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninamshukuru sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, ameahidi kuendelea kutoa fedha. Kwa kweli, tuna imani kubwa na Serikali kwamba fedha ambazo zimeahidiwa zitatoka na zitakwenda kutekeleza mambo yote ambayo yamewekwa katika taarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambazo zimezungumzwa zaidi na Waheshimiwa Wabunge, hoja ya ajira ya walimu na sisi tunaiona na Mheshimiwa Profesa Mkenda ameitolea ufafanuzi, lakini Kamati tuna shauku ya kuona tunaanza ule utaratibu wa *internship* ya walimu ambao wamehitimu vyuo kwa muda mrefu, ili kuendelea kuwaimarisha walimu ambao wapo mtaani waweze kuwa bora na hata ikitokea *interview,* nao wawe katika nafasi nzuri ya kuweza kufaulu na kupata ajira kama ambavyo wanapata walimu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumziwa masuala ya maslahi ya Walimu na Wahadhiri. Sisi kama Kamati, tumeyaona na tungependa kuendelea kuishauri Serikali kama ambavyo ametamka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba, anakwenda kuboresha maslahi ya Walimu. Basi na sisi shauku yetu ni kwenda kuona kweli maslahi yametekelezwa na kazi kubwa tulionayo hapa ni kuwasilisha maoni ya wananchi kwa sababu, sisi ni wawakilishi wa wananchi katika nyumba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni kuhusu *VETA* yamefafanuliwa vizuri na Mheshimiwa Prof. Mkenda. Shauku yetu ni kuona kwamba, yanatekelezwa kama ambavyo yameahidiwa katika Bunge lako Tukufu. Miundombinu ya shule na vyuo vikuu vilevile tunaomba maoni yetu ya Kamati katika eneo hili yaweze kuzingatiwa, kama ambavyo yametolewa mapema asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifaa vya kufunzia na kujifunzia, maoni ya Kamati yamejitosheleza na tungependa tu Serikali iendelee kuyachukua na kuyafanyia kazi kama ambavyo yametolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Ujenzi wa Uwanja wa Dodoma na Uwanja wa Arusha, hili eneo ni mahususi kwa sababu, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Prof. Kabudi amefafanua kwa upana zaidi, lakini tuna shauku kama Watanzania kuwa wenyeji wa Michuano ya

*CHAN* na *AFCON,* tuna shauku siyo ya kushiriki, ila kwenda kwenye ushindani. Tunatamani kuona maandalizi yanafanyika vizuri, Timu yetu ya Taifa inaandaliwa vizuri na mwisho wa siku tuwe sehemu ya ushindani na siyo kushiriki, kama wenyeji wa michuano hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika maandalizi hayo viwanja, kama ambavyo amesema, vinajengwa na hali siyo mbaya. Ukarabati unafanyika Benjamin Mkapa na ujenzi unafanyika katika eneo la Arusha na hapa Dodoma tumesikia Mheshimiwa Waziri anakwenda kusaini mkataba. Yote hayo tuna imani yatafanyika katika muda uliopangwa, na mwisho wa siku sisi, tukiwa ni wawakilishi wa wananchi, tutafarijika katika utekelezaji wa maeneo yote hayo ambayo yamezungumziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa kuzingatia hoja zote ambazo zimezungumzwa hapa na kwa kuzingatia ahadi za Serikali zilizotolewa na viongozi, Waheshimiwa Mawaziri, ndani ya Bunge lako Tukufu, nashukuru sana kwa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwa mujibu wa kanuni.

Wanaokubaliana na Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo pamoja na Maoni na Mapendekezo yake kuwa sasa yawe ni Maazimio ya Bunge, waseme ndiyo na ambao hawakubaliani waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Wabunge wote wamekubali kwamba Hoja ya Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo sasa ni Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kukamilisha kazi za Kamati hizo na kwamba, sasa maoni na mapendekezo ya Kamati zote mbili yamekuwa ni Maazimio ya Bunge, nitumie fursa hii kuipongeza Kamati zote mbili chini ya uongozi wa Wenyeviti, Makamu Wenyeviti wao na Wajumbe wao wote, kwa namna ambavyo wamechambua mambo, kuishauri Serikali ipasavyo na baadaye kuja na taarifa hii ambayo leo imekuwa Maazimio ya Bunge.

Pia, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali yetu, kupitia Mawaziri hawa ambao wametoa maelezo, maana kwa utaratibu ulivyo, hata sisi Wabunge inabidi tukumbushane, mara nyingine tunakuwa tunachangia nje ya Taarifa ya Kamati, lakini unapokuwa na hoja ambayo unaona ni muhimu nje ya Taarifa ya Kamati unatakiwa uilete kwa maandishi hapa ili iweze kuingizwa na kuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge.

Kwa hiyo, nakumbusha, tuwe na utamaduni wa kusoma taarifa zetu ili tunapoona jambo muhimu halijaingia kwenye Kamati, labda wenzetu wamepitiwa, basi tuweze kulileta kwa maandishi na baadaye liweze kuingizwa iwe sehemu ya Maamuzi ya Bunge na iwe ni Maazimio. Isije ikawa baadaye tukailaumu Serikali kwamba pengine nimechangia, nimezungumza, lakini Serikali haijachukua. Utaratibu wetu ni kwamba, tuilete kwa maandishi ili iingizwe kama taarifa nyingine ambazo zimeletwa na Kamati.

Hata hivyo, nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri kwa namna ambavyo wametoa maelezo. Ukiona hivi, ujue kwamba, maamuzi au maazimio yaliyoletwa kutoka kwenye Kamati, tayari

wenzetu wa Serikali wameshatia sura na pengine yako ukingoni kukamilishwa.

Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kazi hiyo na ninaamini baada ya muda huu tulionao, tukielekea mwakani, Kamati zote mbili zitapokea na kuipongeza Serikali kwa kukamilisha Maazimio haya kwa namna ambavyo Mawaziri wametoa maelezo.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, niwatakie kila la heri, Serikali yetu, nikiamini kwamba, kazi zote hizi zinakwenda kukamilika chini ya usimamizi imara kabisa wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Baada ya maelezo hayo, sasa nina tangazo dogo kabla ya kuahirisha Bunge. Tuna wageni ambao wapo muda huu wa mchana, ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kuna wageni 12 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge, ambao hawa ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma na Kwaya ya Kitimtim kutoka Kanisa la *Anglican, Area D*, Jijini Dodoma, karibuni sana wanakwaya wetu kutoka hapa Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, niwatakie mchana mwema na siku njema. Ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.00 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 12 Februari, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*